# Nipashe

Jumanne Oktoba 18, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581102

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 70071 LIKE & FOLLOW

JACKPOT BABA LAO!
TZS. 374,935,160
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Ahukumiwa kunyongwa kwa kumuua mkata tiketi**

UKURASA 3



**MOBETO: MIMI NI CHOMBO**

UKURASA 27



Mhashamu Askofu Msaidizi wa Jimbo Katoliki la Singida, Francis Limu

# Askofu: Ndoa za jinsia moja janga

• **Asema** ni hatari kuliko corona akionya... *Endelea ukurasa 4*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

**SERIKALI YATOA HADHARI UGONJWA KIPINDUPINDU**

SERIKALI imetoa hadhari dhidi ya ugonjwa wa kipindupindu hasa katika mikoa na wilaya zinazopakana na Malawi...

**UKURASA WA 4**

**MSD KUIMARISHA UPATIKANAJI DAWA**

BOHARI ya Dawa (MSD) imebainisha mageuzi mbalimbali yaliyofanywa yakilenga kuimarisha upatikanaji wa...

**UKURASA WA 25**

**NMB YAWAPELEKA UTURUKI W'BIASHARA KIMKAKATI**

WAFANYABIASHARA 15 wanachama wa Klabu za Biashara za Benki ya NMB (NMB Business Club) waliagwa jijini...



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiangalia madawati alipokagua madarasa sita katika Shule ya Sekondari Irugwa wilayani Ukerewe yaliyojengwa kwa Sh. milioni 250. **PICHA: OWM**

## Othman ataka mageuzi ZRB kukusanya mapato

UKURASA 2



## Rais Samia atoa wiki mbili mbolea iwafikie wakulima

UKURASA 2

**MICHEZO** **WAPINZANI WA YANGA SHIRIKISHO HAWA** UK.32 **KATUNI** UK.6

# Rais Samia atoa wiki mbili mbolea iwafikie wakulima

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaomba wakazi wa Kigoma kuipa serikali wiki mbili itatue tatizo la upatikanaji wa mbolea na kutoa namba kwa wakulima waliojisajili kupata huduma hiyo.

Vilevile, amesema uboreshaji wa barabara nchini umeonekana kuongeza kasi ya ajali barabarani huku chanzo kikitajwa kuwa ni mwendo kasi, ulevi wa madereva na kupuuza sheria na alama za barabarani, jambo linaloisababishia serikali hasara na kupoteza nguvu kazi.

Amewataka watumiaji wa miundombinu hiyo kuwa makini na kufuata sheria kwa kuwa ni jukumu la kila mmoja kutunza na sio wizara kama jamii inavyodhani.

Akihutubia wananchi wa mjini Kasulu jana baada ya kufungua miradi ya maendeleo, Rais alisema baada ya serikali kuweka ruzuku kwenye mbolea, kumekuwa na mahitaji makubwa.

"Tunajua kwamba baada ya mbolea kutolewa kwa ruzuku mahitaji yamekuwa makubwa sana, mawakala ndani ya Kigoma ni wachache, ndugu zangu wana Kigoma, tupeni wiki moja, wiki mbili, tunakwenda kuongeza mawakala wa kutoa mbolea hapa Kigoma," aliahidi.

Rais pia alifungua barabara ya kiwango cha lami ya Kidawe-Kasulu yenye urefu wa kilomita 68, aliweka jiwe la msingi barabara ya Kabingo-Kasulu-Manyovu yenye urefu wa kilometa 260.6, kuzima jenereta na kuwasha umeme wa Gridi ya Taifa na kuzindua Chuo cha Ualimu Kabanga.

Kwa mujibu wa Rais Samia, serikali imejipanga kuufanya mkoa huo kuwa wa kimkakati kiuchumi huku akiwataka wananchi kufanya kazi kwa bidii ili kuwa na mchango kwenye mnyororo wa maendeleo.

"Ombi langu kwa wananchi wa Kigoma, tusaidiane kutunza majenereta yale ili wakati wowote yakihitajika yafanye kazi, lakini niwapongeze kwa kupata umeme, shughuli za kiuchumi sasa zinaendelea kukua, wananchi watajiajiri, wawekezaji wanaendelea kuja, utakuwa wa kimkakati kibiashara na uwekezaji," alisema.

Pia aliishukuru Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kuendelea kusaidia ujenzi wa miradi ya maendeleo ikiwamo mikopo ya riba nafuu ya Sh. bilioni 360.5 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami Kabingo-Kasulu.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema ujenzi wa barabara hizo utafungua fursa nyingi za kiuchumi na kijamii, ikiwamo usafirishaji wa watu na bidhaa, kukuza na kuchochea uzalishaji katika sekta ya viwanda, uvuvi, ufugaji na kilimo.

Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema ujenzi wa umeme wa Gridi ya Taifa umesaidia kuondoa gharama za uendeshaji kwa kuwa zilikuwa zinatumika lita za mafuta 12,000 sawa na Sh. milioni 144, huku Mji wa Kasulu pekee ukitumia Sh. milioni 36 kwa siku.

"Mheshimiwa Rais, mafuta peke yake kwa mwaka kwenye vituo hivi vya kuzalisha umeme wa jenereta ni Sh. bilioni 52, wakati mapato ni Sh. bilioni 14. Kwa hiyo, serikali ilikuwa inatoa ruzuku, tunatumia fedha nyingi kuliko mapato tuliokuwa tunapata," alisema.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda alisema serikali itajenga tawi la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS) na kwamba ekari 47.4 zimeshapatikana.



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ikiangalia Transfoma zitakazotumika katika mradi wa kuzalisha umeme wa JNHPP baada ya kuutembelea mradi huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Othman aitaka ZRB kufanya mageuzi ukusanyaji wa kodi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman amesema ni muhimu Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kuangalia pengo la kisera katika mfumo wa ukusanyaji mapato nchini na kuufanyia mageuzi sahihi ili kuongeza ufanisi na kukuza kiwango cha mapato visiwani humo.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na Kamishna wa ZRB, Ramadhani Juma Mwenda, aliyekwenda kujitambulisha na kubadilishana naye mawazo kuhusu masuala mbalimbali yanaoweza kuchangia ufanisi na kukuza kiwango cha mapato yanayokusanywa Zanzibar.

Othman alisema yapo maeneo mengi ya mapato yanayoweza kufanyiwa mageuzi zaidi ya kisera na kisheria na kuchangia kuongeza kiwango cha mapato yanayokusanywa kupitia vyanzo mbalimbali nchini. Alisema hatua hiyo pia itasaidia kuwapo vyanzo zaidi vya mapato vitakavyochangia kasi zaidi ya maendeleo ya nchi kutokana na kiwango kikubwa zaidi cha mapato kukusanywa.

Othman alisema yapo maeneo mengi ambayo baada ya mageuzi ya kisera na kisheria kufanyika yatatumika kukusanyia mapato zaidi na nchi ikaendelea kwa kasi kubwa kwa kiwango cha mapato yatakayopatikana kuliko ilivyo sasa.

Alisema kuna haja ya kuchambua zaidi viwango vya malipo vinavyotokana na ushuru wa stempu hasa katika kutofautisha mapato ya aina hiyo kupitia miradi mikubwa na inayoanzishwa nchini.

Pia alisema kuna fursa nyingi za mikopo na kifedha katika benki mbalimbali nchini zinazoweza kutumika kibiashara, lakini zinatumika zaidi kwa mikopo ya watu binafsi kuliko mashirika ambayo yanaweza kuwa na kiwango cha tija zaidi katika kasi ya ukusanyaji mapato nchini.

Othman alisema eneo la utayarishaji wa mikataba ya kibiashara kupitia watu binafsi, mashirika na taasisi ni muhimu kuangaliwa kwa kuwa linaweza kusaidia kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato na kuchangia kasi zaidi ya kukuza uchumi wa Zanzibar.

Alishauri katika jitihada za kuongeza kiwango cha mapato bodi hiyo iangalie uwezekano katika utaratibu wa benki za Kiisalamu kwa kuwa bado kuna changamoto kwenye eneo hilo na itakapotatuliwa itachangia kiwango cha mapato kuongezeka nchini.

Kamishina wa Bodi hiyo, Ramadhani Juma Mwenda, alisema ZRB inaendelea kufanya mageuzi katika mifumo yake ya ndani ya ukusanyaji mapato na kuchangia kuongeza kiwango cha mapato yanayokusanywa Zanzibar kupitia bodi hiyo.

Alisema kutokana na hali hiyo wamefanikiwa kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, mwaka huu Sh. bilioni 131 hadi 135.

Alisema jitihada kubwa imefanywa kudhibiti udanganyifu na uvujaji wa mapato na kutengeneza mazingira bora ya ulipaji kodi mbalimbali, jambo linalochangia kuongeza ufanisi na mafanikio zaidi ya kukusanya kodi.

## Serikali yatoa hadhari ugonjwa kipindupindu

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imetoa hadhari dhidi ya ugonjwa wa kipindupindu hasa katika mikoa na wilaya zinazopakana na Malawi kutokana na mwingiliano wa shughuli za kiuchumi na kijamii uliopo baina ya wananchi wa nchi hizo.

Hadhari hiyo imetolewa na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, baada ya Waziri wa Afya wa Malawi Oktoba 14 mwaka huu kutoa taarifa kuhusu kuwapo mlipuko wa ugonjwa huo katika taifa hilo.

Taarifa ya Waziri wa Afya Malawi ilibainisha kuwa hadi sasa ugonjwa huo umeshaenea katika wilaya 25 huku vifo 132 vikiripotiwa pamoja na maambukizi kwa watu takribani 4,604.

Kutokana na taarifa hiyo, Mganga Mkuu wa Serikali Dk. Sichalwe, jana alitoa taarifa, akitoa angalizo kuwa ugonjwa huo huambukizwa kwa kula chakula au kinywaji kilichochafuliwa na vimelea vya bakteria aitwaye 'vibrio cholerae'.

Alibainisha kuwa vimelea hivyo hupatikana kwenye kinyesi na matapishi ya mgonjwa wa kipindupindu au mtu mwenye maambukizi ambaye hajaonyesha dalili.

Alisema ili kuudhibiti ugonjwa huo usiingie na kuenea nchini, kila mmoja anapaswa kuzingatia kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka yaliyo safi na salama baada ya kutoka chooni na kumnawisha mtoto aliyejisaidia.

"Dalili kuu za ugonjwa wa kipindupindu ni kuharisha mfululizo kinyesi cha majimaji yanayofanana na rangi ya maji yaliyooshea mchele kisichotoa harufu, kutapika mfululizo, homa, kulegea, kupata kiu na kuishiwa nguvu, mgonjwa anaweza kupoteza maisha endapo hatapata huduma ya matibabu ndani ya muda mfupi," alitahadharisha.

Alisema mwananchi anapaswa kutoa taarifa na kuwahi katika kituo cha kutolea huduma za afya endapo atapatwa na ugonjwa wa kuharisha au kutapika, huku akisisitiza ujenzi wa vyoo, kuvitumia na kuviweka katika hali ya usafi nyakati zote ili vimelea vya ugonjwa visiingie kwenye mazingira ikiwamo maji na chakula.

Vilevile, alisisitiza kutolewa taarifa endapo kutakuwa na watu wenye dalili za kipindupindu katika jamii kwa kupiga namba ya simu 199 bila malipo.

## HABARI KITAIFA

# Ahukumiwa kunyongwa kwa kumuua mkata tiketi

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemhukumu kunyongwa hadi kufa mshtakiwa Hemed Ally baada ya kupatikana na hatia ya kumuua mkata tiketi, Farihani Maluni eneo la Sharifushamba, Ilala jijini Dar es Salaam na kumfukia mbele ya nyumba aliyokuwa amepanga.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Joyce Minde, baada ya mahakama hiyo kuridhika na ushahidi wa mashahidi 12 wa upande wa mashtaka na vielelezo vilivyowasilishwa katika kesi hiyo ikiwamo hati ya amri iliyotolewa ya kufukua mwili huo.

Hakimu Joyce alisema ushahidi uliotolewa umeegemea ushahidi wa kimazingira, lakini mahakama imethibitisha Ally alikuwa na nia ya kuua kutokana na kushindwa kununua gari aina ya Fusso baada ya Maluni kumpa Sh. milioni 30.

"Kwa ushahidi wa mazingira, mahakama lazima ijiridhishe kwa asilimia 100 bila kuacha shaka yoyote kuwa ni kweli kilichotokea ndio uhalisia na mahakama imejiridhisha kuwa mshtakiwa alikuwa na nia ovu," alisema.

Hakimu Joyce pia alisema upande wa mashtaka umethibitisha kilichofukuliwa Februari 9, 2015 eneo la Sharifushamba, Ilala jijini Dar es Salaam ni mabaki ya mwili wa binadamu.

Alisema wamethibitisha kupitia Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Binadamu na Vifo vya Shaka, Innocent Mosha aliyedai kuwa, kabla ya kuuawa na kufukiwa, Maluni alifungwa kamba ya katani mikononi na kichwani alifungwa plasta.

Hakimu Minde alisema uthibitisho wa masalia ya mwili wa Maluni umedhihirika kutokana na nguo za marehemu zilizopatikana zikiwa kwenye mabaki hayo ya mwili wake ambazo zilithibitishwa na mke wa marehemu, Tatu Ally ambaye alidai ni nguo alizomwandalia mume wake asubuhi siku hiyo.

Akichambua utetezi wa mshtakiwa Ally, Hakimu Minde alisema mshtakiwa hakuwasilisha ushahidi mahakamani kama alihama kwenye nyumba aliyopanga Sharifushamba kwa sababu ya maji na umeme kuunganishwa kinyume cha sheria.

Pia alisema upande wa utetezi ulishindwa kumhoji vizuri shahidi Gumbo kutokana na utetezi wake kuwa alikuja kutoa ushahidi dhidi yake kwa sababu alimfukuza kazi katika kampuni yao.

"Upande wa utetezi ulishindwa kuhoji masuala ya msingi na pia kushindwa kuleta vitu vya msingi kuonesha au kuthibitisha alichokidai mshtakiwa kama suala la maji na umeme," Hakimu Joyce alisema.

Aliendelea kubainisha kuwa mshtakiwa katika utetezi wake alidai mateso na vipigo ndiyo vilimfanya atie saini maelezo ambayo hakuyasema, lakini mahakama ilijiuliza kama maneno ya maelezo ya onyo na aliyoyatoa mahakamani yanafanana au la.

"Mahakama iliona maneno yanafanana kwa sababu alichokuwa akiuulizwa mahakamani ndicho kilichokuwapo kwenye maelezo ya onyo ikiwamo idadi ya ndugu zake na jina la baba yake mzazi," alisema.

Wakati Hakimu anasoma hukumu hiyo kuanzia saa 4:45 asubuhi hadi saa 5:53, mshtakiwa alikuwa akimwangalia hakimu bila kupepesa macho yake na alipoelezwa kuwa amepatikana na hatia, macho yake yalianza kuwa na rangi nyekundu.

Baada ya kuelezwa hivyo, Hakimu Joyce alisimama huku mshtakiwa akitaka kutoka kwenye kizimba, lakini hakimu akamwambia asitoke na kumwambia adhabu yake ni kunyongwa hadi kufa.

Taarifa hiyo ilimfanya mshtakiwa kuonekana kama kupigwa butwa ndani ya kizimba cha mahakama huku akipepesa macho yake kwa watu ambao walikuwa wakisikiliza hukumu hiyo ndipo askari magereza aliyekuwa karibu yake akashika bega lake akamkalisha chini kwanza kumtuliza.

Baada ya hakimu kutamka adhabu hiyo, upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili Caroline Kigembe hawakusema lolote kuhusu kukata rufani dhidi ya hukumu hiyo ya kifo.

Awali, Dk. Mosha katika ushahidi wake, alidai haikuwa rahisi kujua chanzo cha kifo cha Maluni, lakini kutokana na kuwapo plasta eneo la fuvu, alihisi aliuawa kwa kuzibwa mdomo na kumsababishia akose pumzi.

Inadaiwa Juni mwaka 2014, Ally alimuua Maluni eneo la Sharif Shamba ndani ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam na kumfukia mbele ya nyumba aliyokuwa akiishi.

**NJE YA MAHAKAMA**

Mke wa marehemu Maluni, Tatu, akiwa na ndugu zake wengine, alionekana akilia na kutamka "mahakama imetenda haki kwa sababu mshtakiwa amemtenganisha na mume wake na watoto wake wawili".

"Mungu mkubwa, maumivu niliyoyapitia mimi na yeye atayapitia hayo hayo, amenitesa sana mimi na wanangu kwa kukatisha uhai wa mume wangu," alidai.

Dada wa marehemu (hakutaja jina lake) alidai hakimu ametoa adhabu inayostahili kwa sababu mshtakiwa alichukua uhai wa mdogo wake bila huruma.

Wakati wakiendelea kulia, mjomba wa marehemu aliwabembeleza kutoka eneo la mahakama na kuondoka kwa sababu tayari mke wa marehemu alikuwa na hali mbaya, hivyo waliondoka huku wakiwa wamemshikilia Tatu ambaye alionekana kukosa nguvu kutembea.


LUHUNGA INVESTMENT CO.LIMITED
P.O.BOX 73 MAFINGA-IRINGA
CONTACT: 0754 819 799/0657 990 766
E-mail: luhungainvestment@gmail.com
Auctioneers, Brokers, Debts and Collection Services
Uaminifu na Ufanisi

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA LEO TAREHE 18/10/2022**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **MUCOBA BANK PLC-MAFINGA** TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU WA MUCOBA BANK PLC- MAFINGA MNADA UTAFANYIKA KUANZIA TAREHE 16/11/2022 SIKU YA JUMATANO NA KUENDELEA KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI MPAKA SAA 12:00 JIONI MAHALI ZILIPO DHAMANA ZA WADAIWA.

**ORODHA YA WADAIWA NI KAMA WAFUATAO:-**

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
|---|---|---|---|
| 1. | STEWARD LUTEGO | NYUMBA | NYOLOLO -NJIAPANDA |
| 2. | SAID KWAY | NYUMBA | KINYANAMBO -MAFINGA |
| 3. | BLANTINA KALINGA | NYUMBA | KINYANAMBO- MAFINGA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. MNADA UTAFANYIKA SEHEMU ILIPO DHAMANA
2. MNUNUZI ATAKAYEFIKIA BEI YA JUU ATALAZIMIKA KULIPA 25% YA BEI ILIYOFIKIWA HAPO HAPO NA 75% ATALAZIMIKA KULIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) BAADA YA TAREHE YA MNADA.
3. ENDAPO MTEJA ATASHINDWA KUMALIZIA 75% NDANI YA SIKU KUMI NA NNE KIASI KILICHOTOLEWA AWALI 25% HAKITARUDISHWA NA MNADA UTARUDIWA TENA.
4. GHARAMA ZA KUBADILISHA HATI MILIKI (TRANSFER OF OWNERSHIP) PAMOJA NA GHARAMA NYINGINE NI JUU YA MNUNUZI.
5. MALI ITAUZWA KAMA ILIVYO

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA KWA NAMBA: 0754 819 799/0657 990 766

217098202




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (wa tatu kulia), akiongoza ujumbe wa Tanzania alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi anayesimamia masuala ya Masoko ya Mitaji, Maendeleo ya Nishati na Mabadiliko ya Tabia Nchi wa Taasisi ya Benki ya Dunia inayoshughulika na utoaji dhamana katika uwekezaji kwa sekta binafsi (MIGA), Sarvesh Suri (kushoto), ambapo Dk. Nchemba anaongoza ujumbe huo kwenye Mikutano ya Mwaka ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Washington D.C, Marekani. Kutoka kulia ni Balozi wa Tanzania nchini Marekani, Elsie Kanze, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango-Zanzibar, Dk. Juma Malik Akil na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba. **PICHA: BEN MWAIPAJA**




# Askofu: Ndoa jinsia moja ni hatari kuliko corona

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

ASKOFU Msaidizi wa Jimbo Katoliki la Singida, Francis Limu, amesema wanaume na wanawake kujihusisha na ndoa za jinsia moja ni ugonjwa mbaya zaidi ya Ukimwi na corona.

Katika mahubiri yake jana baada ya kuzindua Kigango cha Migugu Parokia ya Mtinko ambacho kimezaliwa kutoka Kigango cha Makuro, Askofu Limu, alisema sakramenti ya ndoa inayotambuliwa na maandiko matakatifu ni kati ya mwanamume na mwanamke.

"Mwanamume haolewi na mwanamume mwenzake wala mwanamke haolewi na mwanamke mwenzake. Ukiona hivyo, ujue hao ni vichaa ni wagonjwa," alisema.

Askofu Limu alisema ili ndoa iendelee vizuri ni lazima mwanamke abaki kuwa mwanamke na mwanamume abaki kuwa mwanamume, hivyo tabia ya ndoa za jinsi moja ni hatari kama ulivyo ugonjwa wa Ukimwi na corona.

**MIGOGORO WANANDOA**

Alisema siku hizi familia zinakuwa na shida kwa kuwa mmoja anapopata fedha, matatizo yanaanza katika ndoa, akisisitiza kuwa kitu muhimu ni sala kwa wanandoa kuombeana.

"Kinamama siku hizi wanafanya kazi wanapata fedha na akishapata fedha, anasema 'mimi ndio baba, mimi ndio mama'. Mnanyoa ndevu siku hizi kinamama? Kama wewe ndio baba, basi tuone umekuwa beberu," alisema.

Askofu Limu alisema: "Kinababa mke wako akianza kusema yeye ndio baba, ndio mama, lazima kuna mahali mwanamume hayupo sawa, nati imelegea, hujatimiza majukumu yako vizuri."

Alisema mafanikio yoyote ya kiuchumi na ya kijamii yasiiondoe jamii kwenye msingi wa sakramenti ya ndoa. Hivyo, "suala la ndoa za jinsi moja ambalo linaonekana kupendwa na vijana, halifai na liachwe kabisa."

Waumini zaidi ya 300 wa Kigango kipya cha Migugu walimshukuru Paroko wa Parokia ya Mtinko, Padri Pasiani Mwanga kwa kubariki uamuzi wa kuzinduliwa kigango hicho kwa kuwa awali waliruhusiwa wazee 12 pekee kusali mahala huko kutokana na umbali wa kwenda Makuro.



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Mohammed (katikati), akishuhudia Mkurugenzi wa Biashara wa Kampuni ya CPS, Tobias Dietzold na Mkurugenzi wa Busara Promotions, Yusuf Mahmoud, wakipeana mikono baada ya kusaini mkataba wa udhamini wa miaka mitatu wa tamasha la Sauti za Busara baina ya pande hizo mbili. Hafla hiyo ilifanyika Fumba, Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MSD kuimarisha upatikanaji dawa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BOHARI ya Dawa (MSD) imebainisha mageuzi mbalimbali yaliyofanywa yakilenga kuimarisha upatikanaji wa dawa kufikia asilimia 90 ya mahitaji ikiwamo kufanya mapitio ya mpango wa ununuzi wa bidhaa za afya.

Imesema katika bajeti 2022/23, hadi sasa imeshapokea Sh. bilioni 57 kati ya bilioni 200 zilizotengwa kwa ajili ya kununua bidhaa za afya kwa mwaka mzima.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, alisema mabadiliko ya kimuundo na kimfumo kwa taasisi nzima yako katika hatua za mwisho ili kuimarisha upatikanaji wa bidhaa.

Alisema MSD imefanya mapitio ya taratibu za ununuzi kuongeza kasi ya ununuzi kwa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria ambayo kwa sasa inashirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).

"MSD inafanya mapitio ya maboresho ya mfumo mzima wa mnyororo wa ugavi kwa kuhusisha wadau mbalimbali yanayolenga kuhakikisha uendeshaji wa taasisi unaendana na mahitaji ya vituo vya afya na wadau wengine," alisema.

Alisisitiza kipaumbele kwa sasa ni kuimarisha upatikanaji wa dawa hadi kufikia asilimia 90 ya mahitaji kwa kuingia mikataba ya muda mrefu na wazalishaji wa bidhaa.

"Vipaumbele vingine ni kufanya mapitio ya mpango wa ununuzi wa bidhaa za afya utakaomarisha mfumo mzima wa upatikanaji wa bidhaa za afya, kufanya mapitio ya usimamizi wa mali, kufanya mapitio ya makadirio ya matokeo ya bidhaa ili kupata uhalisia," alisema.

Kuhusu Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote, Mkurugenzi huyo alisema MSD haitakuwa kikwazo kuhakikisha kunakuwapo upatikanaji wa dawa na kwa gharama nafuu.

## Shaka amfagilia Samia kuleta maendeleo nchini

**Na Mwandishi Wetu,** KIBONDO

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ni mwana maendeleo thabiti aliyedhamiria kuleta maendeleo kwa nchi.

Shaka alitoa kauli hiyo jana alipokaribishwa kusalimia wananchi wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika katika Uwanja wa Taifa mjini Kibondo, Rais Samia akiwa ziarani mkoani Kigoma.

"Niwahakikishie wana Kigoma na niwahakikishie Watanzania, ajenda ya maendeleo kwa Rais Samia ipo katika mikono salama kwa kuwa maendeleo kwake ni sawa na kulwa na doto.

"Tathmini ya kazi mnayoifanya ndio hii ambayo leo sisi kama chama tumekuwa na wewe mguu kwa mguu kuona namna gani ambavyo mmetekeleza yale ambayo tumewaahidi Watanzania.

"Mwenyekiti kama ni duka sisi CCM ndio wamiliki wa duka hili. Ninayo furaha kumwambia Rais Samia biashara mnaifanya vizuri sana kuwaletea maendeleo Watanzania," alisema.

Shaka alisema CCM na wananchi ni mashuhuda wa kazi kubwa inayofanyika kila siku kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi.

"Leo hii wote tumeshuhudia wewe, timu yako na sisi CCM tumeshuhudia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2020-2025 ulivyofanyika kwa ufanisi mkubwa ndani ya Mkoa huu wa Kigoma.

"Tumeshuhudia utekelezaji wa Ibara ya 83 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, tuliahidi kuimarisha huduma za afya kwa kujenga majengo ya kisasa na kusimamia upatikanaji wa vifaa tiba, mmefanya kwa ufanisi mkubwa.

"Tumeshuhudia utekelezaji wa Ibara ya 100 inayohusu kuimarisha na kuhakikisha usambazaji na upatikanaji wa majisafi na salama ndani ya Mkoa huu wa Kigoma," alifafanua.

Shaka pia alivipongeza vyama vya upinzani na kuwashukuru viongozi walioshiriki mkutano huo, akibainisha kuwa ni jambo jema katika kumuunga mkono kiongozi huyo kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

"Tunawashukuru kwa kuja kuona mambo mazuri, karibuni tuungane pamoja tuijenge nchi yetu. Nchi ni moja na taifa ni moja, Rais Samia ameanza vizuri kutuunganisha Watanzania mbali na imani zetu na itikadi zetu, Tanzania ni moja," alisema.

Awali msafara wa Rais Samia ulipokelewa katika eneo la Runzewe wilayani Bukombe na Mkoa wa Kagera kwa ajili ya kuwasalimia wananchi, Shaka alisema Rais Samia ameonesha uimara mkubwa katika kuwabana wabadhirifu na wala rushwa na CCM inamuunga mkono katika hilo.

"Mkono wa Rais Samia ni mwepesi kama pamba katika kumwaga fedha za maendeleo kwa Watanzania. Mikono ya Rais Samia ni migumu kama chuma cha pua kwa wabadhirifu na wanaotumia vibaya fedha za maendeleo za Watanzania. Tuendelee kumuunga mkono," alisema.

TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

# TAARIFA KWA UMMA

## USAJILI WA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN) KWA WAAJIRIWA

***Dar es salaam, Oktoba 18, 2022***

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuukumbusha umma kuhusu waajiriwa kuwa na Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) ikiwa ni matakwa ya Kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019. Matumizi ya TIN sahihi ni muhimu katika kuweka kumbukumbu sahihi za waajiriwa na kuwezesha uwasilishaji wa ritani ya kodi za waajiriwa yaani Pay as You Earn (PAYE) kwa kutumia mfumo wa a uwasilishaji wa ritani kielekroniki (e-filing).

Ikumbukwe kuwa, Mamlaka iliagiza waajiri wote wahakikishe waajiriwa wao wana TIN na kuanza kuzitumia kikamilifu ifikapo tarehe 31 Desemba 2020. Pamoja na ukweli kwamba waajiri wengi wameonesha mwitikio chanya bado kuna kundi dogo la waajiri ambao wameshindwa kusimamia matakwa hayo ya kisheria na wamekuwa hawatumii TIN sahihi za waajiriwa au kutumia TIN 999 999 999 ambayo ilikua ni ya mfano katika kipindi cha mpito.

kufuatia hilo, Mamlaka inapenda kuwakumbushwa waajiri na waajiriwa wote kuhakikisha kuwa wanazingatia takwa hili la kisheria la kuhakikisha matumizi sahihi ya TIN. Ikumbukwe kuwa TIN hutolewa bure na Mamlaka na upatikanaji wake ni rahisi. Kwa waajiriwa wenye namba za usajili (NIN) inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), wanaweza kuomba TIN kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa online TIN Registration unaopatikana kwenye tovuti ya TRA (ambayo ni **www.tra.go.tz**). Waajiriwa wasio na NIN wanalazimika kutembelea Ofisi za TRA ili kufanya maombi na kupatiwa TIN.

Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo Karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:

| | |
|---|---|
| **Tovuti** | **: www.tra.go.tz** |
| **Namba za Simu bila malipo** | **: 0800 750 075 / 0800 780 078 au 0800110016** |
| **WhatsApp** | **: 0744 23 33 33** |
| **Barua pepe** | **: huduma@tra.go.tz** |

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Imetolewa na:**

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**
**TRA MAKAO MAKUU**

217098402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Telegrams" "MALIASILI"
Tel: +255 26 2321514/2321568
Barua pepe: ps@maliasili.go.tz
Tovuti: http/www.maliasili.go.tz

Mji wa Serikali
Mtumba,
Mtaa wa Waziri Mkuu,
S.L.P 1351,
40472 DODOMA.

# TAARIFA KWA UMMA

## UTARATIBU WA UTOAJI WA HUDUMA ZA UGANI NA MAFUNZO YA UFUGAJI NYUKI

*Dodoma 12 Oktoba, 2022*

Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa jukumu la kusimamia Sekta ya Maliasili, Malikale na kuendeleza Utalii. Wizara kupitia Idara ya Misitu na Nyuki ina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za Sekta ya Ufugaji Nyuki. Aidha, moja ya jukumu linalotekelezwa na Idara ni kutoa miongozo mbalimbali itakayowezesha usimamizi na uendelezaji wa ufugaji nyuki.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ufugaji Nyuki Na. 15 ya mwaka 2002 kifungu cha 53 Wizara imeelekezwa kutoa utaratibu utakaohakikisha kuwa huduma ya ugani na mafunzo ya ufugaji nyuki yanatolewa kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo. Aidha, katika kutelekeza hilo Wizara imetoa Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo ya Ufugaji Nyuki na Utoaji wa Huduma za Ugani *(National Beekeeping Training and Extension Services Guideline - NBTEG).* Lengo la mwongozo huu ni kuhakikisha kuwa huduma ya ugani na mafunzo yanayotolewa kwa wafugaji nyuki na wadau wengine yanakidhi viwango vinavyohitajika.

Hivyo, kwa tangazo hili Wizara inapenda kuwakumbusha wadau wote wanaojihusisha na utoaji wa huduma za ugani na mafunzo ya ufugaji nyuki kutekeleza yafuatayo:

i. Kuzingatia na kutekeleza maelekezo yaliyotolewa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo ya Ufugaji Nyuki na Utoaji Huduma za Ugani;
ii. Kutoa taarifa kwa Mamlaka za Mkoa/Wilaya/Halmashauri/Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu pindi unapotoa mafunzo ya ufugaji nyuki katika eneo husika; na
iii. Kuwasilisha taarifa za taasisi yako zinazoonesha usajili, aina ya huduma zinazotolewa, anuani na umiliki kwa ajili ya utambuzi na ufuatiliaji. Taarifa hizi zitumwe wizarani kupitia barua pepe: **ps@maliasili.go.tz** au **dfob@maliasili.go.tz** kabla au ifikapo tarehe **30 Disemba, 2022.**

Wizara inapenda kuwasisitiza wadau wote wa ufugaji nyuki kufuata taratibu zilizopo na kushirikiana na Mamlaka mbali mbali za Serikali wakati wa kutekeleza majukumu yao kwa wananchi.

**Imetolewa na: -**
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

217098702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wakulima changamkieni fursa ya CPB

**NI** habari njema kwa wakulima baada ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko nchini (CPB) kufungua milango kwa ajili ya kununua mazao mbalimbali ya wakulima yakiwamo ya chakula.

Habari hiyo njema ilitangazwa na bodi hiyo ikiwa na lengo la kusaidia kuondoa tatizo la ukosefu wa masoko linalowakabili wakulima wengi hapa nchini.

Tatizo la wakulima kukosa masoko ya mazao yao ni kubwa. Wanatumia nguvu nyingi kutayarisha mashamba hadi wakati wa mavuno, lakini ukija upande wa soko wanasumbuka na wengine mazao yao kuharibika au kuuzwa kwa bei ya hasara.

Bodi hiyo sasa imesema imekuja na mkakati wa kununua mazao hayo na wao kuyaongezea thamani ili yaweze kuuzika ndani na nje ya nchi.

Wakulima wengi nchi wamekosa elimu ya kuyaongezea mazao yao thamani na matokeo yake yanapokosa soko mapema huishia kuharibika.

Kwa wanaosafiri kwenda mikoa mbalimbali, barabarani wanashuhudia inapokuwa msimu wa matunda kama machungwa, maembe na mananasi, wakulima wanapata hasara wanapokosa wateja wa uhakika na kubaki kuoza na kuwa chakula cha wanyama.

Hali hiyo hutokea pia kwa mazao mengine yanayoharibika haraka kama nyanya. Wakulima wengine kwa kuona uchungu wa kupoteza mazao hayo, huwaomba wateja kuchukua hata kwa mkopo ili mradi tu aone mazao yake yamechukuliwa na mtu badala ya kutupa.

Kama kungekuwa na viwanda vya kutosha vya usindikaji, mazao hayo yangeweza kuongezewa thamani kwa kusindikwa na kufungashwa vizuri kwa kupata soko la ndani na nje kwa kipindi cha muda mrefu.

Taarifa ya Bodi hiyo kununua mazao kwa wakulima itawaletea faraja kwa kuwa imesema bei wanayonunulia mazao hayo ni ile inayotumika sokoni.

Bodi hiyo imegundua imefungua milango ya kununua mazao hayo ya wakulima baada ya kuona wengi wanalalamika kukosa soko baada ya kuvuna, na hata lile linalopatikana ni la kulanguliwa kwa bei ya hasara na wafanyabiashara wakubwa.

Katika kuwasaidia wakulima ili wapate motisha ya kuendelea kulima mazao hususani ya biashara bila kukata tamaa wameona wasaidie kununua mazao yao baada ya kushuhudia wengine wakiishia njiani.

Baadhi ya mazao wanayonunua wateja kuwa ni mpunga, mahindi, maharagwe na ya jamii ya kunde na yanayotumika kwa ajili ya chakula na lishe.

Vigezo wanavyovitumia katika kununua mazao hayo ni pamoja na kuhakikisha hayana uchafu. Mfano kama ni mchele ni lazima uwe hauna uchafu kama wa mawe.

Pia, bodi hiyo imefungua matawi ya kuuza mazao hayo katika nchi zote za Afrika Mashariki na kuwataka wakulima kuendelea kulima mazao ya biashara.

Lengo lao ni kuhakikisha mkulima ananufaika, anapatiwa fedha ambayo inalingana na bei ya sokoni. Lengo ni kuondoa tatizo la wakulima kufanyiwa udalali na wafanyabiashara wakubwa wasio waaminifu ambao hupendelea kuwaonea ili wao ndiyo wapate faida zaidi.

Fursa hii iliyotolewa kwa wakulima itumike vizuri na kama ilivyoelezwa, mazao hayo yanapopelekwa kuuzwa yawe katika ubora unaotakiwa.

Fursa isitumike kuharibiwa wengine kwa kujaza uchafu ili kuongeza kilo kwenye vipimo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mmomonyoko maadili 'tumefeli' nyumbani

Na Reubeni Lumbagala

**KAMUSI** ya Kiswahili Sanifu ya 2004, inaelezea maana ya maadili kuwa ni mwenendo mwema, onyo au mafundisho yanayotolewa kwa njia mbalimbali kwa wanajamii kuanzia watoto hadi watu wazima.

Yanaweza kuwa malezi nyumbani, shuleni, kazini na ndani ya jamii, ili kuelekeza binadamu atende namna ambayo inamjenga pamoja na jamii nzima.

Maadili yanajumuisha kanuni na imani bora zinazokubalika na jamii. Leo si jambo la kuficha kusema kuwa dunia inaishi katika jamii ambayo sehemu kubwa inaumizwa na mmomonyoko wa maadili kupindukia.

Mmomonyoko huo si tu upo kwa baadhi ya watoto na vijana, lakini pia hata baadhi ya wazazi na walezi, ambapo kimsingi ndiyo walipaswa kuwa kielelezo kizuri cha kuwalea watoto katika misingi ya maadili mema na taratibu zinazokubalika na kila mmoja.

Kutokana na mmomonyoko wa maadili uliopo kwa sasa, jitihada za makusudi zinapaswa kuchukuliwa ili kunusuru kikazi cha sasa na kijacho. Hofu ya Mungu, upendo na undugu vimepungua mno badala yake ukatili, chuki, visasi vimechukua nafasi kubwa.

Hapa kuna tatizo kubwa. Vyombo vya habari kama vile runinga, mitandao ya kijamii, magazeti na redio vimekuwa vikitoa taarifa za mauaji, ubakaji, wizi unaofanywa katika maeneo mbalimbali hapa nchini na hata nje ya mipaka ambazo zimekuwa zikisababisha vifo vya watu, ulemavu na hata kurudisha nyuma jitihada za kimaendeleo zinazofanywa na watu binafsi na serikali.

Kujenga maadili kunagusa wadau wengi, lakini msingi mkuu wa ujenzi wake maadili ni katika familia. Hapa kunanikumbusha mwimbaji wa nyimbo za Injili Daniel Thomas, alipotunga wimbo uitwao "Ibada Njema" ambao katika wimbo huo anasisitiza kuwa mambo mazuri yanajengwa na kuanzia nyumbani yaani familia kwanza.

Mwimbaji Daniel katika wimbo huo anasisitiza kujenga kwanza mambo ya nyumbani kabla ya kuanza ya sehemu nyingine. Kushindwa kujenga maadili bora katika ngazi ya familia ndipo kunapoleta ugumu kwa walimu shuleni, viongozi wa dini kwa waumini wao na viongozi wa serikali kwa watumishi na wananchi wao kuwajenga katika maadili mema wakati watu hao wakiwa wamekosa msingi bora wa maadili katika ngazi ya familia.

Hata maandiko matakatifu mfano yanapokumbusha kuhusu malezi bora yakisema: "Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee". Maandiko na maelekezo hayo yanaweka kielelezo cha kujenga tabia na maadili mema kwa watoto katika ngazi ya familia ambapo wazazi na walezi wanawajibika moja kwa moja kufanya jukumu hilo.

Wanasaikolojia wanaamini kila mtu anazaliwa akiwa na tabia njema, hivyo anahitaji mwendelezo wa kulelewa katika malezi na maadili mema ili kuendelea kuwa na tabia na maadili mazuri. Ugumu uliopo wa kujenga tabia na maadili bora unaweza kupungua au kumalizika kabisa kama wazazi na walezi watatimiza kikamilifu jukumu la kulea watoto wao katika maadili bora.

Ni wajibu wa wazazi na walezi kuwafundisha watoto tabia njema na madili mema nyumbani kukawa sehemu muhimu ya mafunzo kwa watoto.

Ukatili, ubakaji, mauaji ya kutisha, wizi na ujambazi ni matokeo ya mmomonyoko wa maadili. Kama watoto watafundishwa maadili mema katika hatua za mwanzo na za awali za ukuaji wao wakiwa nyumbani kuna uwezekano wa kujenga jamii yenye maadili na heshima.

Wanaojiita 'panyarodi' wanaofanya uhalifu na ukatili tena wakati mwingine mauaji ya watu mitaani baada ya kuvunja milango nyumbani hawatakuwepo ikiwa watoto watalelewa katika maadili hofu na kumcha Mungu huku juhudi hizo zikianzia ndani ya familia. Jukumu jema la kuwafundisha watoto na vijana maadili na tabia njema lianzie nyumbani kwanza, ndipo baadaye liendelee katika nyumba za ibada, shuleni na sehemu nyingine za kijamii.

Gharama za kujenga maadili bora kabla mambo hayajaharibika ni ndogo kuliko kazi za kujenga maadili baada ya mmomonyoko wa maadili kutokea. Jamii ibadilike ili kufundisha na kuimarisha familia, jamii na taifa lenye upendo, amani, utulivu na maendeleo badala ya uhalifu na upotevu ambao ni ulegevu na kukosa bidii kutawala maisha ya watu.

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISRTATION AND LOCAL GOVERNMENT
## KYELA DISTRICT COUNCIL

# THE FINANCIAL STATEMENTS FOR THE KYELA DISTRICT COUNCIL FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE 2021

## STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2021

| | NOTE | 2021 TZS ('000) | 2020 Restated TZS ('000) |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current Assets** | | | |
| Cash and Cash Equivalent | 22 | 1,533,804 | 1,511,956 |
| Equity Investments | 23 | 12,540 | 12,540 |
| Receivables | 24 | 65,322 | 391,234 |
| Loans Receivables | 25 | 448,642 | 736,657 |
| Prepayments | 26 | 415,455 | 94,937 |
| Inventories | 27 | 239,819 | 594,977 |
| **Non Current Assets** | | | |
| Investments in LGLB: LGAs To LGLB | 28 | 37,936 | 37,936 |
| Work in Progress | 29 | 947,171 | 311,187 |
| Property Plant and Equipment | 29 | 23,905,356 | 23,686,906 |
| **TOTAL ASSETS** | | 27,606,045 | 26,878,330 |
| **LIABILITIES** | | | |
| Payables and Accruals | 30 | 2,874,596 | 2,972,517 |
| Deposit - Others | 31 | 378,491 | 495,176 |
| Deferred Income (Recurrent) | 32 | 91,814 | 236,927 |
| Deferred Income (Development) | 33 | 727,689 | 820,806 |
| **TOTAL LIABILITIES** | | 4,072,590 | 4,525,426 |
| **Net Asset** | | 23,533,455 | 22,352,904 |
| **NET ASSETS/EQUITY** | | | |
| Taxpayer Fund | | 0 | 0 |
| Other Reserves | | 54,560 | 54,560 |
| Accumulated surpluses/(deficits) | | 23,478,895 | 22,298,344 |
| **TOTAL NET ASSETS/EQUITY** | | 23,533,455 | 22,352,904 |

The financial statements were authorised for issue by the Full Council Meeting on 29 September 2021 and were signed on its behalf by:

Hon.Katule G.Kingamkono
Council Chairperson
Date: 29/9/2021

MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA KYELA

Ezekiel H.Magehema
Council Director
Date: 29/9/2021

MKURUGENZI MTENDAJI CWD KYELA

Controller and Auditor General    AR/LG/VT.78J5/2020/21

## STATEMENT OF FINANCIAL PERFOMANCE FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | NOTE | 2021 TZS ('000) | 2020 Restated TZS ('000) |
|---|---|---|---|
| **REVENUE** | | | |
| Revenue From Exchange Transactions | 9 | 36,440 | 10,500 |
| Levies | 10 | 1,813,613 | 1,317,995 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 11 | 1,427,517 | 1,653,203 |
| Other Revenue | 12 | 959,053 | 53,849 |
| Subvention From Other Government Entities | 13 | 28,630,937 | 29,619,587 |
| **TOTAL REVENUE** | | 32,867,560 | 32,655,134 |
| **EXPENSES AND TRANSFERS** | | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 14 | 24,363,720 | 25,075,167 |
| Supplies and Consumables Used | 15 | 3,860,650 | 6,123,541 |
| Routine Repair and Maintenance Expenses | 16 | 829,581 | 592,164 |
| Social Benefits | 17 | 811,877 | 159,572 |
| Other Expenses | 18 | 100,717 | 49,046 |
| Provision for Obsolete Inventories | 19 | 0 | 30,507 |
| Subvention to Other Government Entities | 20 | 17,283 | 344,141 |
| Depreciation of Property, Plant and Equipment | 29 | 1,074,920 | 1,055,383 |
| Impairment of Receivables | 21 | 621,104 | 396,237 |
| **TOTAL EXPENSES AND TRANSFERS** | | 31,679,852 | 33,825,758 |
| Share of Surplus/ (Deficit) of Associates and Joint Ventures | | 0 | 0 |
| Surpluses/deficits for the period | | 1,187,708 | (1,170,624) |

The financial statements were authorised for issue by the Full Council Meeting on 29 September 2021 and were signed on its behalf by:

Hon.Katule G.Kingamkono
Council Chairperson
Date: 29/9/2021

MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA KYELA

Ezekiel H.Magehema
Council Director
Date: 29/9/2021

MKURUGENZI MTENDAJI CWD KYELA

## STATEMENT OF CHANGE IN NET ASSETSFOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | TZS ('000) | TZS ('000) | TZS ('000) |
|---|---|---|---|
| Opening Balance (01 July,2020) | 22,298,344 | 54,560 | 22,352,904 |
| Other Appropriations | (7,157) | 0 | (7,157) |
| Surplus/(Deficit) during the year | 1,187,708 | 0 | 1,187,708 |
| Closing Balance (30 June,2021) | 23,478,895 | 54,560 | 23,533,455 |
| | Restated | Restated | Restated |
| Opening Balance (01 July,2019) | 26,935,920 | 54,560 | 26,990,480 |
| Other Appropriations | (3,466,952) | 0 | (3,466,952) |
| Surplus/(Deficit) during the year | (1,170,624) | 0 | (1,170,624) |
| Closing Balance (30 June,2020) | 22,298,344 | 54,560 | 22,352,904 |

The financial statements were authorized for issue by the Full Council Meeting on 29 September 2021 and were signed on its behalf by:

Hon.Katule G.Kingamkono
Council Chairperson
Date: 29/9/2021

MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA KYELA

Ezekiel H.Magehema
Council Director
Date: 29/9/2021

MKURUGENZI MTENDAJI CWD KYELA

## CASH FLOW STATEMENT FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | Notes | 2021 TZS ('000) | 2020 TZS ('000) |
|---|---|---|---|
| **CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | | |
| **RECEIPTS** | | | |
| Subvention from Other Government Entities | 47 | 27,765,263 | 27,959,807 |
| Revenue from Exchange Transactions | 50 | 36,440 | 10,500 |
| Other revenue | 51 | 959,053 | 53,849 |
| Levies | 48 | 1,656,805 | 1,283,742 |
| Fees, fines, penalties and Forfeits | 49 | 1,289,133 | 1,626,446 |
| Exchequer Revenue | | 64,150 | 94,158 |
| **Total Receipts** | | 31,770,844 | 31,028,502 |
| **PAYMENTS** | | | |
| Wages,Salaries and Employee Benefits | 54 | 24,471,190 | 25,197,334 |
| Supplies and consumables paid | 55 | 3,608,128 | 2,956,232 |
| Subvention to Other Government Entities | 59 | 17,283 | 344,141 |
| Social Benefits | 57 | 811,877 | 159,572 |
| Routine repair and maintenance paid | 56 | 829,581 | 592,164 |
| Other Expenses | 58 | 110,717 | 134,772 |
| Decrease in Deposit | 52 | 116,685 | 84,754 |
| **Total Payments** | | 29,965,461 | 29,468,969 |
| **Net CashFlow from Operating Activities** | | 1,805,383 | 1,559,533 |
| **CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | | | |
| **Investing Activities** | | | |
| Receipt from Loan Issued | 53 | (208,015) | (14,279) |
| Loan issued | 53 | 420,000 | 104,648 |
| Acquisition of property, plant, and equipment | 60 | 1,507,400 | 883,634 |
| **Total Investing Activities** | | 1,719,385 | 974,003 |
| Net Increase / Decrease in Cash | | 85,998 | 585,530 |
| Effect of Foreign Currency Changes | | 0 | 0 |
| Cash to be surrendered to Holiding Account | | 0 | 0 |
| Cash to be surrendered to CF | | 64,150 | 94,158 |
| Cash and cash equivalent at beginning of period | | 1,511,956 | 1,020,584 |
| Cash at the end of period | 22 | 1,533,804 | 1,511,956 |

The financial statements were authorised for issue by the Full Council Meeting on 29 September 2021 and were signed on its behalf by:

Hon.Katule G.Kingamkono
Council Chairperson
Date: 29/9/2021

MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA KYELA

Ezekiel H.Magehema
Council Director
Date: 29/9/2021

MKURUGENZI MTENDAJI CWD KYELA

## 1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENT

**1.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL**

**Hon: Chairperson of the Council,**
**Kyela District Council,**
**P.O. Box 320,**
**MBEYA, TANZANIA.**

**1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS**

**Opinion**
I have audited the financial statements of Kyela District Council, which comprise the statement of financial position as at 30 June 2021, the statement of financial performance, statement of changes in net assets, cash flow statement and the statement of comparison of budget and actual amounts for the year then ended, as well as the notes to the financial statements, including a summary of significant accounting policies.

In my opinion, the accompanying financial statements present fairly in all material respects, the financial position of Kyela District Council as at 30 June 2021, its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) accrual basis of accounting and the manner required by the Local Government Finances Act, 1982 (R.E 2000).

**Basis for Opinion**
I conducted my audit in accordance with the International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the Auditor's Responsibilities for the audit of the financial statements section of my report. I am independent of Kyela District Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

**Key Audit Matters**
Key audit matters are those matters that, in my professional judgment, were of most significance in my audit of the financial statements of the current period. I have determined that, there are no key audit matters to communicate in my report.

Charles E. Kichere
Controller and Auditor General,
Dodoma, United Republic of Tanzania.
February 2022

217099402

## Wizara yatoa waraka unaotaka matokeo bora, maadili shuleni

**Na Beatrice Moses**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa waraka unaotaka kuwapo jitihada za kuhakikisha upatikanaji wa matokeo bora kitaaluma unakwenda sanjari na utunzaji wa maadili.

Waraka huo namba sita wa mwaka 2022 unataka kuwapo usimamizi wa maadili kwa wanafunzi wa shule za awali, msingi na sekondari.

Katika waraka huo uliotolewa Oktoba 6 ukitiwa saini na Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, inabainishwa kuwa unapaswa kuanza kutekelezwa kwenye shule zote za serikali na binafsi.

Waraka huo umeelekezwa kwa taasisi za dini, nakala zake zimetumwa kwa wakuu wa ubora wa shule wa kanda na wilaya ili kusimamia ama kuhamasisha utekelezaji wake.

Sehemu ya waraka huo inabainisha: "Imebainika kuwa kumekuwa na jitihada kubwa kutoka kwa wadau wa elimu nchini kusisitiza matokeo bora kitaaluma na kuacha au kuweka jitihada ndogo katika ujenzi wa maadili na tabia za wanafunzi."

Waraka huo unabainisha kuwa hali hiyo kwa kiasi kikubwa inaweza kutoa mwanya kwa watoto wetu kujenga tabia zisizokubalika na kusababisha mmomonyoko wa tamaduni na maadili ya nchini.

Katika waraka huo pia imeelezwa kuwa kuna vyanzo vya taarifa vinavyofanya kazi ya kufundisha na kutoa malezi katika mfumo rasmi au usio rasmi, zikitwaja video nyumbani, taasisi na vibandaumiza, kompyuta (michezo ya kompyuta, mtandao wa kijamii ya face book, twitter, Instagram na barua pepe).

Pia zimetajwa vyanzo vingine vikijumuisha simu, redio, katuni, vinyago na vikaragosi, mabango mbalimbali, vitabu, magazeti, majarida na vipeperushi, mavazi, tabia na mitindo mbalimbali ya maisha ya watu kutoka ndani na nje ya nchi, watu maarufu, wasanii na wanamichezo, makundi rika na kumbi za starehe.

Wizara imebainishwa kuwa utafiti kuhusu makuzi na maendeleo ya mtoto umeonyesha kwa kiwango kikubwa tabia na maadili aliyonayo mtu mzima ni matokeo ya malezi aliyopata wakati wa miaka minane ya awali katika maisha yake.

Waraka huo pia umeeleza kuwa vyanzo hivyo vya vinahitaji umakini na utayari wa jamii katika kuweka mazingira ambayo yatahakikisha kuwa vyanzo husika vya taarifa havisababishi athari hasi kwa tabia na maadili ya watoto na jamii kwa ujumla.

Waraka huo umetoa maazigo 11 ambayo yanapaswa kutekelezwa ili kufanikisha kulinda maadili shuleni.

Maagizo hayo ni shule zote kuanzisha au kuimarisha kamati za maadili/nidhamu shuleni kwa usimamizi wa karibu wa walimu wakuu na wakuu wa shule ili zifanye kazi zake za ujenzi wa tabia na maadili mema kwa wanafunzi kwa ufanisi.

Lingine ni kuimarishwa kwa mabaraza na madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto ili kuhakikisha suala la maadili linajadiliwa katika vikao vyote kama ajenda ya kudumu na shule zote za awali, msingi na sekondari ziweke msisitizo katika ufundishaji wa somo la dini ili kuweka msingi imara wa maadili kwa wanafunzi.

# Waziri awataka watumishi kufunguka kero dhidi yao

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewataka watumishi wa umma kutoogopa kusema kero wanazokumbana nazo maeneo yao ya kazi kwa kuhofia kujengewa chuki na wakuu wa idara zao.

Pia amesema serikali itaendelea kufanyia kazi malalamiko yote yanayowasilishwa na watumishi hao na kuwaahidi kuwalinda dhidi ya viongozi wao pale wanapotoa taarifa za kero kwenye maeneo yao ya kazi.

Ndejembi alitoa kauli hiyo kwa nyakati tofauti alipokuwa akizungumza na watumishi wa Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi na viongozi wa taasisi mbalimbali za umma.

Alisema taarifa za kero zinazotolewa na watumishi hao, zinaisaidia serikali kupata mrejesho wa kujenga utumishi wa umma wenye uadilifu na unaowajibika kwa maslahi ya watumishi wenyewe na taifa kwa ujumla.

"Sisi viongozi tunaomsaidia Rais Samia Suluhu Hassan tunapowatembelea, msiogope kuelezea vikwazo vinavyowakabili kwa kuwa lengo ni kuvitatua na tutawalinda.

"Mkiogopa kusema changamoto zenu, mnajinyima fursa wenyewe. Mnapoziwasilisha kwetu, mnaisaidia serikali kufahamu na kuzitatua," aliagiza.

Ndejembi alisema ofisi yake haitosita kumchukulia hatua ofisa utumishi au mwajiri yeyote atakayebainika kumwonea mtumishi wa umma kwa sababu ya kuwasilisha kero zinazomkabili katika eneo analofanyia kazi.

Kuhusu watumishi ambao hudai kubadilishiwa daraja baada ya kujiendeleza kielimu, Ndejembi aliwataka kuhakikisha wanazingatia mahitaji ya waajiri wao kabla ya kujiendeleza.

"Nitoe ushauri kwa watumishi wa umma nchini, pindi wanapotaka kujiendeleza kielimu kuhakikisha wanazingatia uhitaji wa mwajiri kwa wakati huo ili anapohitimu awe na tija ya kiutendaji ambayo inamshawishi mwajiri kumbadilishia kada," alisema Ndejembi.



Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mivinjeni, Charles Francis, akifafanua jambo kwa wajumbe (hawapo pichani) waliohudhuria mkutano wa wakazi wapatao 45 wanaoishi Kota, Reli, Polisi, Ufundi barabara ya Kilwa Kurasini jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Dar kujenga kituo cha watoto wanaoishi mazingira magumu

**Na Golden Kisapile, TUDARCo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema mkoa huo unatarajia kujenga kituo cha kuwahifadhi watoto wa mitaani na watu wanaoishi katika mazingira magumu eneo la Kigamboni.

Amesema lengo la ujenzi wa kituo hicho ni kuwasaidia watoto hao kujiepusha na matukio ya uhalifu.

Alibainisha kuwapo mpango huo mwisho mwa wiki mkoani hapo wakati wa warsha ya watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na kuwasilisha tathmini ya sensa kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Makalla alisema Mkoa wa Dar es Salaam umeweka mkakati wa kuwasaidia watoto wa mitaani kwa utaratibu ambao hivi karibuni utaanza kutekelezwa.

"Mikakati hiyo ni pamoja na kutengeneza kituo kikubwa cha kuwalea watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu. Kwa hiyo, kama mtoto huyo atakuwa anahitaji kusoma, atapelekwa shuleni kusoma. Kama anahitaji elimu ya ujasiriamali, atapewa elimu hiyo.

"Pia ninataka fursa mbalimbali ziwafikie na katika kituo hicho kutakuwa na fursa za taasisi ambazo zitaweza kuwasaidia watoto wa mitaani ili maisha yao yabadilike," alifafanua.

Makalla alizitaka taasisi za sekta binafsi kushirikiana na makundi maalum yakiwamo ya watu wanaoishi katika mazingira magumu na watoto wa mitaani pindi kituo hicho kitakapokamilika.

"Ninaomba mpango kazi huo utakaotekelezwa mtoe ushirikiano kila mahala, pia nitoe wito kwa taasisi mbalimbali kushirikiana na makundi maalum ikiwamo watu wanaoishi kwenye mazingira magumu na watoto wa mitaani," alisema.

Makalla alisema alishaagiza kuandaliwa eneo husika patakapojengwa kituo hicho, Kigamboni.

Alisema lengo la ujenzi wa kituo hicho ni kuwabadilisha kimaisha na kimtazamo kwa watoto wa mitaani.

"Tusiwaseme vibaya watoto wa mitaani kwa sababu siyo kila kila mtoto alipenda kuwa hivyo, bali tuwapende na tuwasaidie ili wasimame na hatimaye wajitengenezee maisha yao.

"Wazazi na walezi ninawaomba msiwatelekeze watoto, bali muwalee katika mazingira bora na katika misingi ya maadili. Jambo hilo likifanikiwa, tutakuwa tumepunguza ongezeko la watoto wa mitaani na ongezeko la matukio ya kihalifu," alisema.

Mkuu wa Mkoa huyo pia aliwataka wazazi na walezi kutimiza majukumu yao kwa kuhakikisha wanawafuatilia watoto wao kwa kila hatua.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi 2022, Anne Makinda, aliipongeza serikali kwa kuamua kuendesha sensa kwa kundi la watoto wa mitaani, pia akilisifu kundi hilo kwa kukubali kuhesabiwa.

Spika mstaafu wa Bunge la Tanzania huyo alibainisha kuwa takwimu hizo zitatumika katika kupanga mipango ya maendeleo na Dira ya Taifa ya 2026-2050.

# TEN/MET yataka ulinzi zaidi wanafunzi waliorejea shuleni

**Na Elizabeth Zaya**

MTANDAO wa Elimu Tanzania (TEN/MET) umeiomba serikali kufanyia marekebisho Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 ili kuweka kipengele kitakachoweka ulinzi zaidi kwa wanafunzi walioruhusiwa kurejea shuleni baada ya kukatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito.

Novemba 24, mwaka jana, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitangaza uamuzi wa kuwarudisha shuleni wanafunzi wanaokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito.

Mkurugenzi wa Mtandao wa Taifa, Ochola Wayoga, alisema juzi kuwa pamoja na juhudi za serikali za kuwarudisha shuleni wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali, juhudi hizo hazitoshi kama uamuzi huo hautawekwa rasmi kwenye sheria.

"Katika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, hapa kwetu tukumbuke kwamba serikali tayari imeruhusu wanafunzi wanaokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba kurudi shuleni.

"Haiwezi kusaidia huko mbeleni hasa wanapokuja viongozi wenye mtizamo tofauti. Kwa hiyo, ili kuweka ulinzi zaidi, ni vyema kipengele hicho kikawekwa kwenye sheria kabisa.

"Marekebisho haya yatasaidia kuliweka kundi hili katika usalama zaidi wa kutimiza ndoto yao katika eneo la elimu hasa baada ya kukatisha masomo yao wanapokumbana na changamoto zisizoepukika. Kwa hiyo, TEN/MET tunaiomba serikali kushughulikia suala hili kwa uzito zaidi," aliwasilisha hoja yake.

Alisema watoto wa kike wanapitia vikwazo vingi katika kufikia ndoto zao za kielimu, ikiwamo mila na desturi potofu katika jamii inayowazunguka, hivyo kuna haja ya kuendelea kukemea ili kuwasaidia kupata haki zao za msingi kama ilivyo kwa watoto wa kiume.

"Wakati Tanzania inaadhimisha miaka 10 ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike, tuhakikishe dhamira yetu ya kutokomeza mila potofu kwa watoto hawa inaungwa mkono na kila mtu kwenye jamii, ili kuhakikisha anatengenezewa mazingira mazuri ya kutimiza ndoto zake na kupata haki zake mbalimbali.

"Pia ni vyema serikali ikawekeza kwenye kuboresha zaidi katika mazingira ya kufundishia na kujifunzia, ili yapatikane matokeo mazuri kwa wanafunzi hususani katika shule ya msingi," alisema.

Alitoa wito kwa wadau wa elimu katika mataifa mbalimbali kupitia upya na kutathmini hali ya utekelezaji wa sera na sheria zao za ulinzi wa watoto wa kike, kupinga vitendo vya ubaguzi dhidi ya kundi hilo na kuhakikisha wanapata haki sawa katika maeneo yote.

Pia alisema ni vyema zikahakikisha zinawalinda watoto hao dhidi ya unyanyasaji, mimba na ndoa za utotoni.



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amos Nungu, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), katika uzinduzi wa shughuli ya wiki moja ya Sahara Sparks mjini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mratibu Mkuu wa Sahara Sparks 2022, Rose Urassa (kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sahara Ventures, Jumanne Mtambalike (wa pili kushoto), Mwakilishi wa Clouds Media Group, Shafii Dauda na Meneja wa Mradi wa Funguo wa UNDP, Joseph Manirakiza (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bodi yaanza kununua mazao ya wakulima

**Na Elizabeth Zaya**

BODI ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) imefungua milango kwa msimu huu kununua mazao mbalimbali ya wakulima hususani ya chakula.

Ofisa Biashara wa Bodi hiyo Kanda ya Ziwa, Frank Bubelwa alisema jana kuwa lengo la kufungua milango hiyo ni kusaidia kuondoa tatizo la ukosefu wa masoko linalowakabili wakulima wengi nchini.

Alisema baada ya kununua mazao hayo yataongezwa thamani ili wayauze ndani na nje ya nchi, bei ya ununuzi itazingatia iliyopo sokoni.

"Tumeamua kufungua milango ya kununua mazao hayo ya wakulima baada ya kuona wakulima wengi wanalalamika kukosa soko baada ya kuvuna, na hata lile linalopatikana ni la kulanguliwa kwa bei ya hasara na wafanyabiashara wakubwa.

"Kwa hiyo, tukaliona hilo kuwasaidia wakulima ili wapate motisha ya kuendelea kulima hayo mazao hususani ya biashara bila kukata tamaa kama ambavyo tumekuwa tukishuhudia wengine wakiishia njiani," alisema.

Alitaja baadhi ya mazao wanayonunua kuwa ni mpunga, mahindi, maharagwe, mazao yote ya jamii ya kunde na yote ambayo yanatumika kwa ajili ya chakula na lishe.

"Baadhi ya vigezo tunavyovitumia katika kununua mazao hayo ni kuhakikisha hayana uchafu. Mfano, mchele ni lazima uwe hauna ule uchafu mkubwa ikiwamo mawe makubwa na baada ya kuyaleta mazao husika, tunayapima huku mkulima akiwa anashuhudia.

"Bei tunayonunua sisi ni ile ambayo iko sokoni. Kwa mfano, kama maharagwe yanauzwa kwa Sh. 2,000 kwa kilo sokoni na sisi tutanunua kwa bei hiyo hiyo. Na zaidi sana sisi tunayaongezea thamani baada ya kununua kwa ajili ya soko la ndani na nje," alisema.

Aliongeza kuwa tayari wamefungua matawi ya kuuza mazao hayo katika nchi zote za Afrika Mashariki na kuwataka wakulima kuendelea kulima mazao ya biashara.

"Lengo letu ni kuhakikisha mkulima ananufaika, tunampatia fedha ambayo inalingana na bei ya sokoni. Lengo ni kuondoa tatizo la wakulima kufanyiwa udalali na wafanyabiashara wakubwa wasio waaminifu ambao hupendelea kuwaonea ili wao ndio wapate faida zaidi,"alifafanua.

# Bodi ya Tumbaku yapongeza uwekezaji uliotoa ajira Moro

**Na Mwandishi wetu,**
MOROGORO

BODI ya Tumbaku nchini imepongeza mwekezaji mzawa Ahmed Huwel na menejimenti ya kiwanda cha tumbaku cha Mkwawa Leaf Tobacco kwa kufanikiwa kukifufua kikichakata tumbaku kama ilivyokuwa awali.

Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku nchini, Victor Mwambalaswa, alitoa pongezi hizo wakati wa ziara ya wakurugenzi wa bodi hiyo kiwandani huko juzi.

"Lengo la ziara hii ni kutembelea kiwanda hiki na kuona kama kinafanya kazi kama ambavyo walitueleza. Tumefurahishwa sana na kile tulichokiona kiwandani hapa," alipongeza Mwambalaswa ambaye ni Mbunge mstaafu wa Lupa.

Kiongozi huyo na wengine waliteuliwa hivi karibuni kuongoza bodi hiyo.

Alisema kiwanda hicho ambacho awali kilikuwa kinamilikiwa na kampuni ya Marekani na kufungwa miaka minne iliyopita, kilinunuliwa na mwekezaji mzawa na kuanza uzalishaji hivi karibuni.

"Kwa sasa kiwanda kimefufuliwa na kinafanya kazi vizuri ambapo tumeona wenyewe kimenunua tani milioni saba zao la tumbaku na tayari kimeanza kulichakata zao hilo," alisema.

Mwambalaswa alisema uchumi wa wilaya unategemea tumbaku na alifurahishwa na ajira zinazotolewa kiwandani huko, zikisaidia kukuza uchumi wa mkoa na mtu mmoja mmoja.

Aliutaka uongozi wa kiwanda hicho kuendeleza juhudi ya uchakataji zao hilo kwa kuwa uwekezaji walio nao ni mkubwa na kuhakikisha tumbaku inaletwa kiwandani hapo inachakatwa kwa ufanisi mkubwa, bila kujali ni mali ya kiwanda hicho au ni mali ya makampuni mengine.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo, Stanley Mnozya, aliupongeza uongozi wa kiwanda hicho kwa kufikia malengo ya kununua tumbaku na kuwasaidia wakulima kwa kuwapatia soko la uhakika tofauti na awali.

Pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zilizowezesha kiwanda hicho kinaendelea kuzalisha na kutoa ajira kwa Watanzania wote.

"Kwa hiyo kuanzia sasa ni marufuku kwa mfanyabiashara yeyote wa tumbaku kusafirisha zao hilo kwenda nje ya nchi bila kuchakatwa. Tuliweka utaratibu huo hapo katikati kwa kuwa tulikuwa na tatizo la uchakataji nchini, hasa baada ya kufungwa kwa kiwanda hiki ambacho ndicho kikubwa, sasa baada ya kufufuliwa utaratibu huo sasa ukome," aliagiza.



## Viongozi wanaouza maeneo ya hifadhi watangaziwa kiama

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

KAMISHNA wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, ametangaza kiama dhidi ya viongozi wa umma, wanaoshiriki kuuza maeneo ya hifadhi ya misitu.

Alitangaza kuanza kwa operesheni ya kuwadhibiti viongozi hao jana, baada ya kwenda kukagua eneo la hifadhi hiyo iliyoko Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, ambalo limevunwa miti na kuchomwa mkaa.

"Endapo wananchi wataendelea kukubali hili na kuruhusu ardhi ichukuliwe na watu wakafanya shamba la bibi la kuvuna misitu. Wataishia kubaki bila kuimiliki ardhi yao.

"Nitoe wito kwa wananchi, wasiruhusu misitu ile itumike bila idhini yao, kama wenyeviti wa vijiji wanauza maeneo wao wawe wa kwanza kusema hapana.

"Wasikaribishe madalali wa ardhi kwenye maeneo yao kwa kuwa madalali hao wataichukua ardhi na kuinua kwa bei rahisi, watavuna misitu na baadaye wataimiliki na wananchi watakuwa hawana ardhi ya kuimiliki." Alisema.

Prof. Silayo alielezwa na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Handeni, Amiri Changogo, kwamba wenyeviti wa serikali za mitaa na vijiji, wanaoshiriki kuhujumu misitu watachukuliwa hatua kali.

"Wenyeviti wetu wa vijiji kwanza waelimishwe athari ya kuhujumu misitu, atakayerudia tutajua anafanya makusudi na hapo hatua kali zitachukuliwa dhidi yake, kwasababu sisi misitu tunategemea, mvua zimepotea sasa Handeni," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe, alielezea ni kiasi gani misitu imeharibika katika wilaya hiyo na hatua zitakazochuliwa kupitia uchunguzi uliofanywa na Kamati ya Usalama ya Wilaya kwa kushirikiana na TFS.

"Tumebaini kuna vibali hewa vya kusafisha mashamba, kuna madalali wa kuchoma na kuuza mkaa na mbao ambao wanaomba vibali TFS kwa kushirikiana na wenyeviti wa vijiji au vitongoji na watendaji," alisema.

Alisema: "Kwa hiyo nimeagiza TAKUKURU pamoja na TFS wasimamishe mara moja kazi za usafishaji wa mashamba Handeni, pia vibali vyote nilivyosaini mwezi uliopita vipitiwe upya na kujiridhisha iwapo kweli mtu ana shamba".

# Serikali yatatua mgogoro uliodumu kwa miaka 17

**Na Hamida Kamchalla,**
TANGA

SERIKALI imeupatia ufumbuzi mgogoro wa mipaka ya kiutawala kati ya Wilaya za Tanga na Mkinga, ambao ulidumu kwa kwa miaka 17.

Mwarobaini wa mgogoro huo ulipatikana juzi baada ya Mkuu wa Mkoa huo, Omar Mgumba, kueleza kuwa kiini cha mgogoro kilikuwa ni uelewa mdogo wa baadhi ya viongozi wa wananchi katika kutambua mipaka. "Ukiangalia Mkinga, imezaliwa mwaka 2005 na walipopata eneo lao la utawala la Wilaya ya Mkinga, katika kutambua mipaka yao wakaenda kuweka mipaka sehemu tofauti na mpaka halisi ulipo, hapo ndiko tatizo lilipoanzia.

"Eneo lililokuwa na mgogoro ni Mtaa wa Mleni ulioko Halmashauri ya Jiji la Tanga na Gombero iliyopo Mkinga."

Kutokana na athari za mgogoro huo, Mgumba, alisema hatua alizochukua awali kabla ya kufanya uamuzi huo ni kuunda timu iliyokuwa na viongozi wa maeneo husika pamoja na wataalamu wa ardhi, Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga, ambao walibaini mambo manane.

"Baada ya timu hii kupita, tumebaini kimsingi matangazo yote matatu ya magazeti ya serikali yalikuwa sawa kama ambavyo tumeamua leo hii kumaliza mgogoru huu.

"Na hayo ni tangazo la kwanza, namba 89 la kuanzisha Halmashauri ya Tanga la Mwaka 1983, tangazo la pili, namba 237 la mwaka 2005 la kuanzisha Jiji la Tanga na tangazo la tatu la gazeti la serikali, Namba 337 la mwaka 2005 la kuanzisha Wilaya mpya ya Mkinga.

"Matangazo yote matatu, yanashabihiana mipaka ilivyotamkwa. Kwa hiyo hatuna mgogoro kwenye matangazo ya serikali, yote yanakubaliana mpaka ndiyo hapo ulipopita,"

Hata hivyo, alibainisha kuwa tangazo lingine la kuanzisha Kata ya Mzizima nalo linashabihiana na matangazo hayo manne, kwa hiyo hauna mgogoro kwenye matangazo hayo ya serikali.

Alisema: "Tumebaini kuna nyumba 54 zilizoko kwenye eneo la mgogoro, awali zilikuwa zinatambulika kwamba zipo Wilaya ya Tanga, lakini sasa zitatambulika ziko Wilaya ya Mkinga".



Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Kiria Laizer (kulia), akizungumza baada ya viongozi wa Chama cha Walimu (CWT) kumpongeza kushika nafasi hiyo jana, kushoto ni Katibu wa CWT Simanjiro, Nazama Tarimo na Mwenyekiti, Abraham Kisimbi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Uhaba viti mwendo wazielemea shule jumuishi H'shauri Arusha

**Na Allan Isack,** ARUMERU

HALMASHAURI ya Arusha, imetangaza kuwa na uhaba wa viti mwendo katika shule jumuishi zilizotengwa kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu.

Akizungumzia hali hiyo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Seleman Msumi, alisema kutokana na uhitaji huo, wamelazimika kufungua milango kuyaita mashirika binafsi, taasisi za umma na watu wenye uwezo kiuchumi kuchangia upatikanaji wa viti hivyo.

"Tunakabidhi viti mwendo vinne kwa wanafunzi wenye ulemavu kutoka shule nne zenye vitengo vya elimu maalumu ili kuwarahisishia wanafunzi hao kuwawezesha kufuata elimu na kufanya shuguli zao binafsi.

"Tunaamini kwamba msaada huu, utasaidia kupunguza tatizo la wanafunzi hawa kushindwa kutembea, hasa wakiwa katika mazingira ya shule kutokana na kuwa na uwezo mdogo wa kutembea." alisema.

Kutokana na uhitaji huo, Msumi, amewaita wadau mbalimbali kujitokeza kusaidia wanafunzi wengine wenye uhitaji wa namna hiyo ili watoto hao waweze kutimiza ndoto zao.

"Tuna uhitaji mkubwa wa vifaa kwa ajili ya kuwahudumia wanafunzi hawa wanapokuwa shuleni, hivyo natoa wito kwa mdau yeyote atakayeguswa kutoa msaada akaribie kwenye ofisi zetu za halmashauri au mojawapo ya shule zenye watoto wenye uhitaji wa namna hii waweze kutoa msaada huo," alisema.

Hata hivyo, wazazi wa wanafunzi waliopatiwa msaada huo, waliishukuru serikali kwa kuwakumbuka wahitaji kwa kuwa sasa hivi wataendelea kupata elimu bila ya kuwa na tatizo lililokuwa linawakabili hapo awali.

"Ninamshuru Rais Samia Suluhu, kwa kunipatia hiki kiti kitanisaidia kusoma bila kuwa na tatizo lolote, kwa kuwa mama alikuwa ananibeba kunipeleka shuleni, hivyo anachoka sana na wakati mwingine hakunipeleka, naamini nitatimiza ndoto yangu ya kuwa Mhasibu," alisema Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Naurei, Catherine Paul, ambaye ana ulemavu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Naurei, Getruda Tarimo, alisema: "Tunatambua na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na serikali hasa kwa kutoa fedha ya chakula kila mwezi kwa watoto wenye ulemavu na sasa imeona umuhimu wa kuwaletea viti mwendo, licha ya kuwa uhitaji bado ni mkubwa lakini tumepata sehemu ya kuanzia."

Halmashauri ya Arusha inakabiliwa na uhaba wa viti mwendo zaidi ya 20 katika shule zake nane zenye vitengo vya elimu maalum pamoja na vifaa vingine kwa ajili ya kuwahudumia hao watoto.





# Wasichana 200 Simanjiro wakeketwa kwa siri

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WASICHANA 200 katika Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, wanadaiwa kukeketwa kwa siri licha ya serikali na wanaharakati wanaopiga vita ukatili wa kijinsia, kuweka mitego kila kona ili kukabiliana na vitendo hivyo.

Kwa mujibu wa Ofisa Rasilimali Watu wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Christina Marwa, wasichana hao waligunduliwa baada ya kupata ujauzito na kwenda kwenye vituo vya afya, kwa ajili ya kujifungua.

Marwa alitoa taarifa hiyo juzi wakati akizindua mradi wa kupambana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto unaosimamiwa na Shirika la Pastoralist Economic and Social Advancement (PESA).

Mradi huo unafadhiliwa na Shirika la The Foundation for Civil Society.

"Hawa wasichana wote wana umri chini ya miaka 20 na waligunduliwa miezi miwili iliyopita. Hii wilaya inatishiwa na ukatili wa kijinsia ukiwamo ndoa za utotoni na ukeketaji.

"Ukeketaji na ndoa za utotoni, bado ni tatizo kubwa kwa jamii ya kifugaji, hasa ya Kimasai. Hali inayosababisha baadhi ya wasichana kuzikimbia familia zao na kwenda kutafuta mahali salama pa kuishi," alisema.

Alisema ukatili dhidi ya wasichana na watoto katika wilaya hiyo, unatakiwa kuwekeza nguvu ya mapambano na ushirikiano kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, jamii na taasisi mbalimbali ili kukomesha suala hilo.

Mmoja wa waathirika wa ukatili huo, (jina limehifadhiwa), Mkazi wa Kijiji cha Ndepesi, Kata ya Lobosoito, alisema baada ya kufanya mtihani wa darasa la saba mwaka jana, wazazi wake walimuandaa kumuozesha na wakati akijiandaa kujinusuru kwa tukio hilo, walifanikiwa kumkeketa.

Mwathirika mwingine, alisema alibahatika kusoma hadi kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Oljoro na baada ya kufanya mtihani wa kuhitimu masomo yake, wazazi wake walianza taratibu za kutaka kumuozesha.

Hata hivyo, alisema wakati hatua hizo zikiendelea, matokeo yalitoka amefaulu daraja la tatu, hivyo alitakiwa kwenda kujiunga na Chuo Morogoro, lakini wazazi wake waliendelea na mchakato wa kujipanga kumuozesha.

Mkuu wa Dawati la Jinsia wa Jeshi la Polisi, Wilaya ya Simanjiro, Tusajigwe Deus, alisema tatizo la ukatili kwa watoto wa kike wilayani humo ni kubwa na linahitaji nguvu ya pamoja kunusuru wasichana kuendelea kukeketwa na kuozwa wakiwa na umri chini ya miaka 18.

# Samia awapa neema wasichana wanaoishi mazingira magumu

**Na Oscar Assenga,** TANGA

RAIS Samia Suluhu Hassan amepeleka 'neema' kwa wasichana wanaoishi mazingira magumu katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, baada ya kutenga Sh.250, 000 kwa kila mmoja wao kuanzisha mradi wa kiuchumi utakaomuepusha asiingie kwenye tamaa na kurubuniwa kimapenzi.

Akizungumzia mpango huo, Mkurugenzi wa Jiji hilo, Spora Liana, alisema fedha hizo ni zile zinalolenga kuwezesha mtoto wa kike kutimiza malengo.

"Mpango huu unaonyesha ni namna gani Rais (Samia), anavyowajali watoto wa kike na kuwathamani. Kama ndivyo mtoto wa kike usikubali kurubuniwa kimapenzi.

"Badala yake wekezeni nguvu kubwa kwenye kusoma kwa ajili ya mafanikio yenu ya baadaye, kwa sababu elimu ndiyo njia pekee inayoweza kuwakomboa kiuchumi wao na jamii yao." Alisema.

Akizungumza wakati wa maadhimisho hayo ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, Naibu Meya wa Jiji hilo, Mwanaidi Kombo, alisema bado watoto wa kike wana jukumu la kufanya ili kuondokana na adha ya kukosa maendeleo.

Katika maadhimisho hayo, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Shirika la BRAC Maendeleo Tanzania, Isihaka Mirambo, alisema wao wamejikita kuwasaidia watoto wa kike kukabiliana na matatizo mbalimbali na kuwawezesha kuchangamkia fursa za kiuchumi.

Alisema wanufaika 1,376 wamepatiwa mafunzo mbalimbali yahusuyo elimu ya afya ya uzazi, athari zitokanazo na matumizi ya dawa za kulevya na ujasiriamali.

Alisema: "Lakini watoto takribani 2100 tumewapatia elimu ya awali katika vituo vyetu vya malezi na makuzi vilivyopo katika shule za serikali za msingi mkoani Tanga.

"Huku watoto wengine 772 wakiendelea kunufaika na elimu hiyo nchini ya Ufadhili wa NORAD (Shirika la Maendeleo la Norway) na BRAC Maendeleo, ikiwa ni utekelezaji wa mradi huu."



Kaimu Meneja wa Benki ya NMB Muheza, mkoani Tanga, Hobokela Wilson, akimkabidhi zawadi ya fedha Sh. 20,000 mwanafunzi wa darasa la pili, Monika Amani anayesoma Shule ya Msingi Muheza Estate baada ya kuwa wa kwanza katika mashindano ya kusoma vitabu, kuandika na kuhesabu yaliyowashirikisha wanafunzi 15. (Wa pili kushoto) ni Kaimu Ofisa Elimu Msingi Wilaya, Beatus Mtumbuka. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Somo kuzuia biashara wanyamapori, ujangili kufundishwa shule za polisi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKURUGENZI wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai nchini (DCI), Ramadhan Kingai, amesema mchakato wa kuingiza mtaala mpya wa elimu katika shule za polisi, kwa ajili ya kuongeza nguvu ya kukabiliana na ujangili na usafirishaji wa mazao ya wanyamapori kwenda nje ya nchi, umeiva.

Kwa mujibu wa DCI, Kingai, mtaala huo utatekelezwa katika shule zote za polisi nchini, ambazo zitakuwa zikifundisha askari wapya pamoja na maofisa mbalimbali wa jeshi hilo wanaopanda vyeo.

Mpango huo unatekelezwa kwa ubia, kati ya Jeshi la Polisi nchini na Taasisi ya Kimataifa ya Afrika Mashariki ya Kuzuia Biashara Haramu za Wanyamapori na Ujangili.

"Tunakuja na mbinu bora zaidi duniani za kukabiliana na uhalifu huo wa biashara haramu za wanyamapori na ujangili.

"Tunaamini kwamba elimu hiyo tutakayoanza kuitoa, itasaidia kukabiliana na matukio hayo, ambayo yamekuwa yakihatarisha uhai na usalama wa viumbe hao katika hifadhi mbalimbali za taifa hapa nchini,"alisema.

Maeneo yatakakofundishwa mbinu hizo ni Shule ya Polisi Moshi (TPS), Chuo cha Polisi Dar es Salaam, Chuo cha Polisi Kidatu na Chuo cha Polisi Zanzibar.

Aidha, akifafanua zaidi kuhusu mpango huo, Meneja Mradi wa Kuongeza Nguvu za Kupambana na Biashara Haramu za Wanyamapori na Ujangili Afrika ya Mashariki, William Mallya, alisema mafunzo hayo yatatolewa hadi kwa askari waliopo katika maeneo ya mipaka ya nchi na viwanja vya ndege.

Mtaalamu mbobezi wa wanyamapori nchini, Dk. Andimile Martin, alisema elimu hiyo itakayotolewa pamoja na mambo mengine itawasaidia askari wa Tanzania, kuimarisha ulinzi wa wanyamapori kwa kukusanya taarifa za kiintelijensia zitakazosaidia kukamatwa majangili.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 18, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




## Mtaala Uraia umetuangusha




Waliokatishwa masomo 70 wanavyonufaika ni shule tena




## Ni kilio binti akijuta baba alivyomkwamisha kielimu

ELIMU

NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA

# Boda mkaa kitisho kipya barabarani

• Licha ya kusababisha ajali za mara kwa mara misitu inateketea, mazingira yakibaki taabani



Mfanyabiashara akiwa na viroba vilivyosheheni kwenye bodaboda. **PICHA: SABATO KASIKA**

WASOMAJI tunapoisoma TESA tumshukuru Mwenyezi Mungu kila mahali na kila saa kwa kuwa ndiye aliyetuumba na ni yeye peke yake mwenye 'hatimiliki' ya uhai wetu. Anatupatia riziki za kila siku pamoja na kuturehemu, jina lake lihimidiwe.

Baada ya utangulizi huo, sasa nirejee kwenye hoja kwa msingi kwamba "aulizaye ataka kujua, je, kisheria pikipiki zinaruhusiwa kubeba mkaa na kuusambaza kwa wateja? Limefanyiwa kazi kikamilifu kabla ya kuliruhusu jambo hili?

Nauliza kwa sababu limekuwa suala la kawaida na la muda mrefu kwa bodaboda kujikita katika usafirishaji wa mkaa na kuupeleka kwa watumiaji, pamoja na kufanya hivyo huenda wanajipa jukumu hilo kwa kulazimisha.

Jijini Dar-es-Salaam, matumizi ya pikipiki kubeba mkaa kutoka kwenye misitu ya asili, ni makubwa, karibu barabara zote kuu Mandela, Ali Hassan Mwinyi na Morogoro zinazotoka mikoani kuingia jijini humo hukosi kuona bodaboda kadhaa zikiwa na shehena ya magunia ya mkaa.

Yanabebwa matatu au manne makubwa kupindukia na hata namna magunia yanavyobebwa kwenye pikipiki ni hatari kwa mwendeshaji na watumiaji wengine wa barabara. Unakuta magunia yaliyojaa mkaa kupitiliza rumbesa, mawili yanaunganishwa pamoja kuwa kama gunia moja. Wakati mwingine mwendesha pikipiki haonekani maana nyuma yake ni magunia na pembeni pia, kulia na kushoto kadhalika ni magunia ya mkaa.

HUENDA HAWADHIBITIKI

Inavyoelekea ni vigumu kuwadhibiti waendesha pikipiki katika ujumla wao, hata ambao wanabeba binadamu taratibu za kisheria zinawakataza kubeba abiria watatu kwenye pikipiki moja, lakini wanafanya hivyo. Isitoshe hata kwenye makutano ya taa za barabarani wanapita bila kujali zuio la taa zikiwa nyekundi.

Hawajali wakati rangi ya kijani ndiyo ya kuruhusu wapite lakini hawana subira. Kuna msemo wa 'subira yavuta heri' kwao msemo huu hawauthamini bali ni haraka haraka mradi wamepita na kunusurika bila kujali usalama wao na abiria, matokeo yake ni ajali nyingi.

Katika matukio hayo wapo wengine wanaopoteza maisha au viungo na kuwa walemavu, lakini vyombo vya usafiri huharibika na miundombinu nayo kubomoka.

Hapo busara iko wapi maana unahitaji pikipiki uitumie upate riziki ya kila siku lakini ukaishia kupoteza maisha au kuwa mlemavu.

Mwaka 2012 zilifanyika juhudi za kuwakamata waliokuwa wakibeba mkaa kutoka sehemu za Dumila na kwingineko, kuuleta mjini Morogoro lakini hazikufanikiwa. Askari wawili wa usalama barabarani (trafiki) waliweka kizuizi karibu na eneo la mzani wa kupima magari makubwa (ya mizigo na abiria) barabara ya Morogoro kwenda Dodoma.

Hata mimi nilikuwapo pia nikisaidiana nao, cha kushangaza ofisa usalama barabarani alipokuwa akiona pikipiki iliyobeba mkaa alisimama katikati ya barabara na kunyoosha mkono kumtaka mwendesha pikipiki asimame; lakini ilikuwa kama anawachochea kuongeza mwendokasi mkubwa hivyo, kumlazimisha polisi akwepe ili asigongwe.

Baada ya kuona zoezi hilo hali-

INAENDELEA UK.18

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Waliokatishwa masomo 70 wanavyonufaika ni shule tena

• DC awamulika wazazi, walezi wasiojali malezi

KITUO cha mafunzo ya ujuzi wa fani mbalimbali kwa mabinti waliokatisha masomo kwa sababu za mimba na ndoa za utotoni cha 'Reach the Goal', kimepiga hodi katika Kijiji cha Mwanambaya wilayani Mkuranga mkoa wa Pwani, wasichana wakifundishwa kushona mavazi ya kila aina, kutengeneza mishumaa, pedi, urembo na mapambo ili kuwasaidia kujikimu pamoja na watoto wao.

Reach the Goal inayosimamiwa na Himiza Development Organization (HDO) na Lutogo Development Initiative, ilizinduliwa na Mkuu wa Wilaya, Khadija Ali, hivi karibuni kuanza kufunza mabinti hao mara moja.

Mkurugenzi wa Himiza, Prisca Ngweshemi, anasema kituo kimeshapokea mabinti 70, watakaoanza mafunzo hivi karibuni akiamini yatakuwa na mchango katika kuinua maisha ya walengwa hasa kuwaongezea kipato, mbinu za utafutaji na ubunifu.

"Tulipanga kuanza na mabinti 70 kulingana na uwezo wetu, lakini inaonekana wanaohitaji ni wengi zaidi, itabidi tuwafundishe kwa zamu," anasema Prisca na kuongeza kuwa kukatisha masomo kwa sababu na mimba au ndoa za utotoni limekuwa kama jambo la kawaida kwenye baadhi ya jamii, na kwamba wanataka mabinti watimize ndoto za kupitia ujuzi watakaopata kituoni hapo.

Mkurugenzi huyo anasema wapo baadhi ya wazazi na walezi wanaodai kuwa wana hali duni ya maisha inayowafanya wawakatishe masomo mabinti zao ili waolewe, wapate mahari na fedha na kwamba hiyo ni hatari kwa ustawi wa watoto wa kike.

"Kwa ujumla huku vijijini changamoto ni nyingi, kwani katika karne hii, wapo watu wasiojua umuhimu wa elimu, kwani katika kundi ambalo tumelikusanya, wamo ambao hawakubahatika hata kusoma shule ya msingi," anaeleza.

Mwanzilishi wa Lutogo Development Initiative, Lulu Mwalubandu, anasema umoja ni nguvu, na kwamba shirika lake limeamua kuungana na Himiza kwa hali na mali, ili kuwakomboa watoto wa kike katika kijiji hicho wakiamini kuwa wakipata uwezo watapanua shughuli zao wilaya nzima, kwani inaonekana tatizo ni kubwa.

Anasema Siku ya Mtoto wa Kike Afrika inayofanyika kila Oktoba 11, walikuwa katika Shule ya Sekondari ya Kiparang'anda tukiwasaidia wanafunzi pedi, tukagundua kuwa mabinti wanahitaji kuelimishwa ili kukwepa vikwazo," anasema Lulu.



Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Ali (katikati), alipozindua kituo cha Reach the Goal. Kulia ni Mkurugenzi wa Himiza Development Organization, Prisca Ngweshemi, Mwanzilishi wa Lutogo Development Initiative, Lulu Mwalubandu, Diwani wa Kata ya Mipeko, Adili Kinyenga, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya hiyo, Timothy Kudra. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**



Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Ali (mwenye kitambaa shingoni) na viongozi wa mashirika hayo, Diwani wa Kata ya Mipeko, Adili Kinyenga (kushoto), wakiwa na baadhi ya mabinti watakaofaidika na kituo hicho.

> Mmeniomba kuwa mlezi wa Reach the Goal, nimekubali, lakini sharti langu ni kwamba mashirika yenu yasiwe ya mfukoni, bali yafanye kazi kuhakikisha jamii inabadilika kwa kuachana na mila potofu.

Mwenyekiti Kijiji cha Mwanambaya, Leila Chabruma anasema kina wakazi 10,000 na kwamba suala la mabinti kukatisha masomo limekuwa kama jambo la kawaida hasa kutokana na mila na desturi za huko.

"Hawa wenzetu walioleta kituo wamechukua mabinti 70, lakini ukweli ni kwamba wapo wengi tu ambao wanahitaji kusaidiwa, lakini pia kuelimisha wazazi na walezi kutambua umuhimu wa elimu," anasema Leila akifafanua kuwa tatizo liko katika vitongoji vyote saba vinaavyounda kijiji hicho vya Madodo, Kiloweka, Mizugu, Kibeneke, Mamangwa, Mabatini na Mivule.

### ONYO LA DC

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Ali, anawaonya wazazi na walezi wasiosimamia malezi bora kwa watoto wao akisema serikali itawachukulia hatua za kesheria bila huruma, kwa kuwa baadhi yao wanawaacha watoto wajilee wenyewe.

"Ninawatangazia wazazi na walezi ambao hamtimizi wajibu wenu wa malezi hatua kama kuwakamata na kuwafikisha mahakamani zitachukuliwa dhidi yenu kama hamtasimamia malezi," anasema Khadija.

Anasema katika wilaya hiyo kumekuwa na matukio mengi ya aina mbalimbali yakiwamo ya ndoa za utotoni, mabinti kupewa mimba huku wazazi na walezi wakimalizana kimya kimya na watuhumiwa ambao wakati mwingine ni ndugu zao na kusababisha unyanyasaji huo kuota mizizi na kukomaa.

"Kumbukeni mzazi au mlezi kumuozesha mtoto ni kumkatili na pia kumkatisha masomo na kumfanya asitimize ndoto zake, hivyo niwaombe wanawake muwe mstari wa mbele kukemea na kutoa taarifa ya matendo yote maovu dhidi ya watoto wote wakiwamo wa kiume," anasema.

Anasema hataki kuona hayo yakiendelea wilayani mwake, na kwamba kila mzazi na mlezi atimize wajibu wake wa malezi, na kuwa tayari kutoa taarifa kwa vyombo vya dola anapoona kuna viashiria vya ukatili kwa watoto.

DC Khadija anasema baadhi ya wazazi wamekuwa wakiilaumu serikali, pale watoto wao wanapofanya maovu katika jamii, wakidai imeshindwa kudhibiti vitendo viovu bila kutambua kuwa chanzo ni malezi duni.

Aidha, mkuu huyo wa wilaya, ameyataka mashirika ya Himiza na Lutogo kufanya kazi ya kusaidia kukomboa watoto wa kike katika kijiji hicho na kuisaidia jamii kubadilika na sio kuwa mashirika ya mfukoni.

"Mmeniomba kuwa mlezi wa Reach the Goal, nimekubali, lakini sharti langu ni kwamba mashirika yenu yasiwe ya mfukoni, bali yafanye kazi kuhakikisha jamii inabadilika kwa kuachana na mila potofu," anasema.

### OMBI KIJIJI/ KATA

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Mkuranga na mratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali wilayani humo, Timothy Kudra, anaomba uongozi wa kijiji na kata ya Mipeko kushirikiana na taasisi hizo ili jamii ielimishwe na kuachana na mila potofu.

"Serikali haiwezi kutekeleza kila jambo, ndiyo maana kuna mashirika yasiyo ya kiserikali, hivyo niuombe uongozi wa Kijiji cha Mwanambaya na Kata ya Mipeko kwa ujumla, mshirikiane na aidha, anafafanua kuwa Wilaya ya Mkuranga kwa sasa ina mashirika yasiyo ya kiserikali zaidi ya 40, na kwamba yanashirikiana na serikali vizuri, huku ikiyawekea mazingira mazuri ili yatimize majukumu yaliyonayo.

"Katika kuonyesha kwamba mashirika yasiyo ya kierikali yana mchango mkubwa, kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike, Himiza na Lutogo zilifanikisha siku hiyo kwa kutoa pedi kwa wanafunzi wa Sekondari ya Mwanambaya," anasema.

ELIMU

**NA ANKRAS LUOGA**

# Kuzomea vikojozi, wazembe kunavyoumba mbumbumbu

• Wazazi, walimu acheni kuhamasisha, mnabomoa hamjengi

NI kawaida kusikia mzazi au mlezi akisema mzomeeni huyu kikojozi au ameshindwa hiki au kile. Mwalimu naye yumo analiambia darasa mzomeeni amekosea kusoma au ametenda mambo haya.

Wote wawili huungana na watoto au wanafunzi katika kumcheka aliyekosea bila kujali ametenda kwa kudhamiria au kwa kutokujua na kibaya ni athari zake katika maisha ya mtoto au mwanafunzi anayezomewa maana pamoja na kuumia kisaikolojia anadhoofishwa kifikra pia.

Japo wazazi, walezi na walimu hao hufanya hivyo kwa nia njema wakiamini ni kumfanya mtoto au mwanafunzi abadilike na kufanya mambo mazuri, matokeo yake kimalezi ni mabaya, husababisha mtoto akose kujiamini na kukata tamaa katika kuweka juhudi za kufanya vizuri zaidi au kushindwa kuachana na tabia inayosababisha azomewe. Matokeo yake ni kuwa na jamii isiyosaidiana ila yenye kuchekana na kuzomeana wenzao wanapopitia changamoto za kimaisha.



Watoto wanapokusanyika wafurahiane si kuzomeana wala kuchekana. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### ATHARI KUZOMEA/ KUCHEKA

Kuwacheka na kuwazomea waliokosea kunaleta athari nyingi na mojawapo ni watoto na wanafunzi kuanza kuathirika kisaikolojia hasa kwa kukosa kujiamini na kutokuwa wabunifu katika yale wanayoyafanya au wanayotakiwa kuyafanya. Hii hutokea kwa sababu ya kushindwa kufanya kitu au vitu kwa kuogopa kuzomewa na kuchekwa na wenzao, pia watoto hawa hukosa upendo kwa wengine, wazazi walezi na hata walimu wao kwa kuona kuwa hawapo pamoja kipindi wanapopitia magumu na wala hawawasaidii katika kuyakabili.

Wahusika na jamii wakumbuke matokeo haya siyo mazuri kwa maisha ya watoto ya sasa na ya baadaye kwa maana yataendelea kwa maisha yao yote. Hilo hupelekea kutokea kwa kizazi kisichosaidiana katika kutatua changamoto zao na kisicho kuwa na upendo.

> Tukumbuke swali kubwa na la msingi kwetu na tujiulize na kujijibu kila mara 'ni nini jukumu, mchango na nafasi yetu katika kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya watoto na wanafunzi wetu?

### NAMNA YA KUSAIDIA

Wazazi, walezi na walimu waanze kujitathmini na kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mtoto au mwanafunzi wanaoweza kuwa waathirika wa kuzomewa mfano, mzazi mwenye mtoto anayekojoa aanze kumfuatilia kwa ukaribu na kusaidia ili apunguze kunywa vitu vyenye maji hasa muda wa jioni na usiku kabla ya kwenda kulala.

Aidha, ampeleke hospitali au kwa wataalamu wa masuala ya mfumo wa mkojo, saikolojia na pia hata kumsaidia kwa kumuamsha usiku hata zaidi ya mara moja ilia ache kukojoa kitandani. Kwa wanaoshindwa darasani, wazazi au walimu wamsaidie mtoto ili kuacha vituko darasani au kitu kisichofaa anachofanya na kama ni masomo hafanyi vizuri mwalimu anaweza kumpa mazoezi ya ziada pia nyumbani wamsimamie na kumfuatilia.




Wote wafahamu kuwa wanaopitia changamoto hizo hawazifanyi kwa makusudi ili wakosee kusoma au wakojoe vitandani au wawe na tatizo lolote inatokea na pia ikumbukwe kuwa kuna tabia na vitendo vingi vinavyotokana na matatizo ya kiafya ambayo wanatakiwa kuyafanyia ufuatiliaji kwa wataalamu wa afya ili kuyatatua.

Mfano, mtoto anayeshindwa kufanya vizuri darasani, inawezekana inatokana na vitendo vya ukatili nyumbani au maeneo mengine katika jamii. Tatizo kama hili ni lazima litatuliwe kwa njia ya kitaalamu na sio kumzomea au kumcheka wakati anapitia shida hiyo.

Zaidi ya wazazi na walimu tujiulize vizuri juu ya "je, tumetumia muda wa kutosha kutafuta maarifa ya kutosha ili kuelewa vizuri kile tunachokiona au kinachotokea kwa watoto wetu au wanafunzi wetu? Je, tumetumia njia sahihi katika kutatua tatizo hilo linalomkuta mtoto au mwanafunzi wetu?"

Badala ya kuzomea na kucheka watoto familia na walimu shuleni wafuatilie kwa ukaribu ili kugundua vyanzo halisi vya tabia au matatizo ya watoto au wanafunzi wao, ili kuchukua hatua sahihi za kumsaidia mtoto kuliko kumcheka au kumzomea.

Kuwasaidia kutawajengea watoto na wanafunzi kujiamini, kuwa wabunifu na wenye uthubutu katika mambo wanayoyafanya katika maisha yao ya sasa na ya baadaye bila kuwa na woga wa kuchekwa au kuzomewa na wengine. Watoto na wanafunzi wataweza kutoa maoni na mawazo yao bila kuogopa kuchekwa au kuzomewa na wenzao wala wazazi, walezi na walimu wao.

Pia watoto na wanafunzi hawa watajenga dhana ya kupendana wao kwa wao na kuona kuwa jamii iko pamoja nao katika changamoto zao na wanawasaidia katika kuondokana na matatizo hivyo kuwa na upendo na utayari kutoa nguvu zao katika kujenga maisha yao na ya wengine yote yatafanikisha kufikia kizazi na taifa lenye kujiamini, ubunifu, uthubutu, amani na upendo.

### WITO KWA WALIMU

Wazazi na walimu tuache tabia ya kuhamasisha watoto au wanafunzi wetu kuwazomea au kuwacheka wenzao ambao hawafanyi vizuri kitabia au kielimu bali tuwasaidie kuondokana na changamoto. Tusipofanya hivyo watoto na wanafunzi wanakata tamaa na kukosa kujiamini na ubunifu katika kila kitu wanachokifanya wakiishi na wasiwasi.

Walimu na wazazi waanze kujitafakari kama njia na hatua mojawapo ya kujitathmini na kujifanyia ufuatiliaji wa karibu katika kuwasaidia watoto na wanafunzi kufikia malengo yao katika maisha.

Wazazi, walezi na walimu waache kuwa chanzo cha kujengeka kwa woga na ukosefu wa ubunifu kwa watoto na wanafunzi kwa kuhamasisha wengine kuzomeana na kuchekana pale mmoja wao anapokosea au kwenda tofauti na utaratibu uliozoeleka.

Tukumbuke swali kubwa na la msingi kwetu na tujiulize na kujijibu kila mara 'ni nini jukumu, mchango na nafasi yetu katika kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya watoto na wanafunzi wetu?

***Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi katika fani ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya Miradi ya Afya - Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili -MUHAS***

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Ni kilio binti akijuta baba mzazi alivyomkwamisha kielimu

"BABA alimtelekeza mama mwaka 2005 nilipoanza shule ya msingi na kuanzia hapo maisha yangu kielimu yakawa magumu. Umbali mrefu kufika shuleni bila fedha mfukoni wala chakula tumboni ilisababisha kuonewa huruma na kijana aliyejitolea kunisaidia nauli na hatimaye kutumia udhaifu huo kunipa mimba."

Anasema Mwanaisha Kapinda (25), anayeishi Kijiji cha Mtandango wilayani Kilwa Masoko mkoa wa Lindi, anapoelezea jinsi ndoto yake ya kusoma ilivyokatishwa, kutokana na ukatili wa kijinsia, wakati wa mazungumzo na Nipashe Siku ya Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike, wilayani hapo, yanayofanyika kila mwaka Oktoba 11.

Mwanaisha anakumbusha kuwa baba alipowatelekeza aliacha mzigo mkubwa kwa mama wa kulea familia bila masaada jambo lililochangia kuwakwamisha kimaisha na hata kielimu.

"Nilitamani sana kuwa mwalimu tangu nikiwa mdogo nikiamini ningefikia hatima hiyo baada ya masomo yangu, lakini ndoto yangu ilizimwa baada ya matatizo mengi yaliyotokana na baba kuitelekeza familia yetu," anasema.

Ingawa kuna siku baba alikuwa anatuma hela ya chakula na sabuni kwa mwezi shilingi 30,000 lakini bado zilikuwa hazitoshi kwa matumizi ya nyumbani kuanzia chakula, tiba na mavazi.

"Nilikuwa natoka kijiji Mtandango kwenda Sekondari ya Kikanda kwa miguu nikitumia saa sita kwenda na kurudi ni kwa sababu hakuna usafiri wa wanafunzi wala wa mabasi ila kwa familia zenye uwezo wanafunzi walipelekwa na bodaboda au gari, " anasema Mwanaisha na kuongeza kuwa matatizo ya njaa, kutembea umbali mrefu na umaskini yalisababisha kurubuniwa na kupata mimba.

"Nilipata ujauzito nikiwa kidato cha tatu na kuanzia hapo maisha yalibadilika kuzidi kuwa magumu nikihangaika mitaani hadi nilifungua Juni 2014 hali ikazidi kuwa ngumu nikiishi na mama." Anaeleza.

Anasema mambo yalizidi kuwa magumu na mtoto wake kupata shida, mwaka 2018 niliolewa na mwanaume mwingine na kupata mtoto wa pili lakini Machi 2020, mume wake wa pili alifariki dunia, na kabla ya kifo chake mzazi mwenzake aliaga dunia na kuachwa na watoto wawili.

Mwanaida anakabiliana na ugumu wa maisha kwa kurudi nyumbani kwa baba yake na kuanza kilimo cha mpunga, kuokota korosho katika shamba la mzazi huyo, kusuka wateja mbalimbali na kuuza keki, lakini bado maisha yalikuwa magumu na alitamani kuendelea na masomo lakini hakujua pa kuanzia.



Mwanaisha Kapinda. **PICHA: BEATRICE PHILLEMON**

> Nilitamani sana kuwa mwalimu tangu nikiwa mdogo nikiamini ningefikia hatima hiyo baada ya masomo yangu, lakini ndoto yangu ilizimwa baada ya matatizo mengi yaliyotokana na baba kuitelekeza familia yetu.

### KURUDIA MASOMO

"Ingawa nimepita katika changamoto hii, nashukuru Shirika la Actionaid- Kilwa, Jukwaa la Wanawake Tumaini Jipya kwa Wanawake Kilwa (TUJIWAKI) na Tanganyika Christian Refugee Services (TCRS) kutoa elimu kuhusu haki za wasichana, ukatili wa kijinsia na masuala mengi ambayo yamenifumbua macho hadi nimefika hapa leo," anasema Mwanaisha.

Kupitia elimu na ushauri alioupata, amejiunga na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Kilwa-Masoko, akisoma kozi ya ushonaji kwa muda wa miaka miwili aliyoianza Februari mwaka huu.

"Safari yangu ya elimu ilianza tena 2019 katika kijiji cha Mtandango, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike, TUJIWAKI, TCRS na dawati la jinsia la polisi walikuwa wakitoa mafunzo mbalimbali walinichukua kuwaelimisha wasichana wenzangu wasiopendi kusoma wakitaka kuolewa."

Aidha, Mwanaisha anasema kupitia matamasha mbalimbali na vipindi vya radio amejifunza mambo mengi, anajua wapi anaweza kupata haki yake, madhara ya ukatili wa kijinsia, mimba za utotoni na hivi majukwaa ya wanawake wilayani Kilwa wanamtumia kama balozi wa mfano ili kuhamasisha wasichana wapende kusoma badala ya kuolewa.

Aidha, anamshukuru mwalimu Shakila Natangu, wakati akienda kusuka walimu shuleni, alimhimiza asikate tamaa kwa sababu elimu haina mwisho na kuongeza:

"Nakumbuka siku moja mwalimu Shakila, aliniita akanishauri kuhusu kuchangamkia nafasi katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Masoko na kunieleza kuwa watoto waliopata matatizo ya kukatishwa masomo kama mimi wanasomeshwa na serikali na kwamba kukosa ada kulimkwamisha kuendelea na masomo."

Mwanaisha, aliupokea ushauri lakini hata hivyo alipata changamoto nyingine, ambayo ni sehemu ya kuwaacha watoto wake ili aweze kwenda shuleni, alipata ufumbuzi kwa kusaidiwa na dada yake anayewatunza.

"Namshukuru ndugu yangu kwa kulelea watoto, ActionAid -Kilwa, TUJIWAKI kwa kutoa mafunzo mbalimbali na serikali kwa kugharamia mafunzo ambayo yamemsaidia kurudi tena shuleni, matroni Theresa Nalinga kwenye chuo ninachosoma akinishauri kila siku, nisiache kusoma, niendelee na masomo, changamoto zipo za kila siku nipambane miaka miwili siyo mingi nitahitimu." Anasema na kuomba serikali kuongeza kozi ya kudarizi na mapishi pia chuoni hapo.

### TUJIWAKI YANENA

Katibu wa Jukwaa la Wanawake, Tumaini Jipya kwa Wanawake Kilwa (TUJIWAKI), Pili Kuliwa, anasema, Mwanaisha ni miongoni wa wasichana walionufaika na mafunzo yanayotolewa na asasi hiyo kuhusu kukabili ukatili wa kijinsia, haki za wasichana kwa njia ya radio na matamasha ya aina mbalimbali.

"Mwaka 2019, TUJIWAKI tulifanya mkutano wa kuelimisha jamii katika kijiji cha Mtandango wananchi walifundishwa masuala mbalimbali, akiwa kwenye kusanyiko hilo alipata nafasi ya kuuliza anawezaje kufika kwenye chuo cha maendeleo ili kusoma nasi tukampa maelekezo," anasema.

Pili alipiga simu kwa mkuu wa chuo hicho kujua kama kuna nafasi ili Mwanaisha ajiunge na kufahamishwa kuwa ipo na akaanza kufuatilia na ndugu zake na wadau wengine wakiwapo walimu waliokuwa wakimshauri mambo mbalimbali ili kumjengea ujasiri walifanikisha lengo lake.

Mbali na hilo, Shirika la Action-Aid- Kilwa kwa kushirikiana na TUJIWAKI wameendelea kufundisha kinamama kutambua na kuripoti matukio ya ukatili, usawa wa kijinsia, haki za binadamu, matunzo ya watoto, mafunzo ya ujasiriamali kwa nadharia ili watu wajiimarishe kiuchumi na kupambana na umasikini.

Aidha kutambua athari za mabadiliko ya tabia nchi na jinsi ya kukabiliana nazo ni mambo wanayofunzwa pia huku kinamama wakifundishwa kushiriki katika masuala ya kijamii kama vile kuchangamkia nafasi za uongozi na kugombea, utunzaji na umiliki wa ardhi ili wawe na nguvu za kiuchumi.

TEKNOLOJIA

NA GAUDENSIA MNGUMI

# CRISPR-Cas9, utaalamu kitabibu unaopindua nasaba, jeni, viungo

• Kusuka upya mifumo asilia kukabili udhaifu unaorithiwa



Jeni au nasaba zinazosababisha kuzaliwa na ualbino zinaweza kuhaririwa kwa kuboreshwa zaidi kupunguza na kuondoa maumbile hayo. **PICHA: MTANDAO**

KUZUKA kwa maradhi yanayotishia maisha na mengi yakiambatanishwa na nasaba -DNA na mifumo ya jeni (genes) kunaongeza kasi ya kutumia teknolojia na ugunduzi kwenye muundo wa seli na tishu za viumbe hai wakiwamo binadamu, ili kukabili milango au maeneo yenye hitilafu zinazoleta udhaifu na kuruhusu hitilafu mwilini.

Ujio wa teknolojia ya 'gene editing' au 'kuhariri jeni' ni utaalamu unaohusisha kuondoa, kuongeza, kubadilisha na kuweka sawa zaidi jeni au nasaba za binadamu ili awe bora utimilifu kiviungo na afya zaidi kwa kupunguza magonjwa.

Jeni au genes ni mambo yanayopatikana kwenye DNA au vinasaba ambayo vimekusanya habari na taarifa zote zinazohusu kiumbe. Hutoka kizazi kimoja hadi kingine nasaba zinabeba mkusanyiko wa habari za aina ya kiumbe kama ni mnyama au mmea. Zina maelekezo yanayotengenezwa kiumbe hicho kama ni mwanadamu awe mwanaume anakuwa na miguu miwili, mikono miwili na vidole, rangi ya ngozi, nywele, kucha awe na jinsia ya kiume, mrefu wa futi sita, akili yake na mambo yote yanayomkamilisha.

Aidha, hali hiyo pia iko kwa wanawake ndani ya seli zao kuna jeni zenye habari zinazodhibiti tabia za kike ndani yake mfano kuwa na matiti, habari za hedhi kila mwezi, maumbile, rangi ya ngozi na vitu vyote ambavyo wanadamu anakuwa navyo awe Mwafrika, Mzungu au Mchina vyote vikirithishwa kutoka vizazi baada ya vizazi. Kadhalika hali hiyo iko kwa wanyama wengine kuanzia virusi, vimelea, fungasi na kwa mimea ya aina yote.

Mara nyingi kazi za kuhariri zinahusishwa na kuboresha au kuziandika vizuri taarifa ziwe za habari, magazeti, ripoti za vitu mbalimbali, tafiti, vitabu na majarida, lakini leo, teknolojia imefanikisha kuhariri jeni na nasaba kuzipa sura mpya kwa kuondoa mbovu au iliyokuwa duni.

Teknolojia ya uhariri wa chapisho la asili la jeni (natural genes) unaitwa CRISPR-Cas9 ambayo ni teknolojia ya kisasa zaidi kwenye matibabu inayowapa wanasayansi na mabingwa wa utafiti wa tiba uwezo wa kubadilisha DNA ya kiumbe. Mchakato huo unaruhusu nyenzo za kijeni kuongezwa, kuondolewa, au kubadilishwa katika maeneo mahusussi ndani ya mwili wa binadamu.

Mbinu kadhaa za uhariri wa jeni zimegunduliwa na kutengenezwa, na inayojulikana zaidi ni CRISPR-Cas9, huu mfumo wa haraka, nafuu, sahihi zaidi na wenye ufanisi kuliko mbinu nyingine za uhariri wa jeni.

> Safu za CRISPR zinapofanyakazi huziruhusu bakteria "kukumbuka" virusi au vimelea vinavyohusiana au kufanana kwa karibu na kirusi kilichomvamia binadamu au kiumbe.

CRISPR-Cas9 iliibuliwa kutoka kwenye mfumo wa uhariri wa jene, unaofanyika mwilini kwa utaratibu wa maumbile ambako bakteria wa kutengeneza kinga huutumia kama ulinzi dhidi ya maradhi. Wanadamu au viumbe wapoambukizwa virusi, bakteria huyo hukamata vipande vidogo vya DNA au nasaba za virusi vivamizi na kuviingiza kwenye DNA yao wenyewe katika muundo fulani ili kuunda sehemu zinazojulikana kama safu za CRISPR.

Safu za CRISPR zinapofanyakazi huziruhusu bakteria "kukumbuka" virusi au vimelea vinavyohusiana au kufanana kwa karibu na kirusi kilichomvamia binadamu au kiumbe.

Ikiwa virusi vitashambulia tena, bakteria huzalisha sehemu za RNA (Ribonucleic Acid) au Asidi ya Ribonucleic kutoka kwa safu za CRISPR zinazotambua na kushikamana na maeneo maalum ya DNA ya virusi. Bakteria hutumia Cas9 au kimeng'enya kinachofanana na Cas9 li kukatakata DNA ya kirusi na kukiangamiza na huko ndiko kuukinga mwili na magonjwa.

Uhariri wa genome au jeni una manufaa makubwa na maslahi muhimu kwa binadamu katika kuzuia na matibabu ya magonjwa. Hivi sasa, uhariri wa jeni hutumiwa katika seli na mifano ya wanyama kwenye maabara za utafiti ili kuelewa na kufuatilia magonjwa chimbuko na jinsi yanavyoweza kudhibitiwa.

Wanasayansi za tiba wanafanya juhudi kubaini kama mbinu hii ni salama na inafaa kutumika kwa watu wakati utafiti unaendelea wanachunguza kwa kufanya majaribio ya kimatibabu kuangalia aina mbalimbali za magonjwa, ikiwa ni pamoja na matatizo ya jeni moja kama vile 'cystic fibrosis', 'hemophilia' tatizo la mwili kukosa uwezo wa damu kuganda na kusababisha kuvuja muda wote' 'hemophilia' na seli mundu.

Pia inaongeza mwangaza kwenye kuzuia na kutibu magonjwa ya saratani, moyo, maradhi ya akili na mishipa ya fahamu na maambukizi ya virusi kama vya ukimwi (VVU) na mengine ambayo yanaambatana na taarifa zilizohifadhiwa kwenye vinasaba na jeni.

Wasiwasi wa kimaadili unajitokeza wakati wa uhariri wa jeni, kwa kutumia teknolojia kama vile CRISPR-Cas9, inatumiwa kubadilisha jeni za binadamu. Mabadiliko mengi yanayoletwa na uhariri ni madogo kwa seli za 'somatic' hizi ndizo zinazounda mwili. Ni zaidi ya seli za asili kama 'yai' kwa upande wa wanawake na seli za manii kwa wanaume.

Mabadiliko au uhariri unaofanywa hutengwa kwa tishu fulani siyo mwili mzima na mabadiliko au uhariri unapofanyika haurithishwa kizazi kimoja na kingine au jeni zilizoboreshwa hazipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine au kutokwa mzazi kwenda kwa watoto, wajukuu na vitukuu.

Hata hivyo, mabadiliko yanayofanywa kwenye chembe za urithi katika yai au mbegu za kiume au chembe za urithi za kiumbe kichanga kilicho tumboni zinaweza kupitishwa kwa vizazi vijavyo.

Hata hivyo, uhariri wa seli za viumbe vichanga kwenye kizazi havifanyiki kwa sababu huleta changamoto kadhaa za kimaadili, ikiwa ni pamoja na iwapo itaruhusiwa kutumia teknolojia hiyo ili kuboresha sifa za kawaida za binadamu (kama vile urefu, ufupi au akili) huenda ikiwa ni kutumia vibaya fursa hiyo.

Wasiwasi kuhusu maadili na usalama, uhariri wa seli ya viini ni kinyume cha sheria kwa sasa hata nchini Marekani na nchi nyingine nyingi mambo hayo hayafanyiki.

**MEDILINE PLUS**

# Boda mkaa kitisho kipya barabarani



Mkaa unaosubiri wateja wakiwamo bodaboda ili kuufikisha kwa wateja mijini hasa Dar- Es- Salaam. **PICHA: TFS**

**INATOKA UK.13**

fanikiwi kama ilivyokuwa imekusudiwa ikabidi waondoke, vilevile, hata kuwazuia wasipite taa za barabarani zikiwa nyekundu, changamoto ni hiyo ya mwendesha pikipiki yupo radhi amkanyage polisi ilimradi asonge mbele.

Wakati mwingine ajali zinatokea katika barabara ya mwendokasi kisa, kulazimisha kutumia njia hizo wakati hawaruhusiwi. Hii ni dhana potofu ya kutafuta fedha kwa kulazimisha na kuvunja sheria na taratibu za barabarani, matokeo yake ni majuto na kuathiri hali za maisha kwa abiria na wao wenyewe na familia zao. Ndiko kuangamizwa kwa kukosa maarifa kutokana na kufanya maamuzi yasiyo sahihi.

**KUHARIBU MAZINGIRA**

Kibaya zaidi pikipiki hizo zinachochea ukataji miti ovyo ili kutengeneza mkaa. Kwa sababu

> Vilevile, Wakala wa Huduna za Misitu usitoe vibali vya kusafirisha mkaa au mazao mengine ya misitu kwa kutumia pikipiki.

misitu mingi ya asili katika ardhi za vijiji hata katika baadhi ya misitu ya serikali kuu na halmashauri za wilaya, hakuna usimamizi na ulinzi wa kutosha. Hivyo ni kama 'shamba la bibi' watu wanaingia na kufanya wanavyotaka na kusababisha uharibifu mkubwa katika maeneo yenye misitu.

Hali ya mazingira nchini ni mbaya tena sana wakati hakuna pengine pa kukimbilia. Mwenyezi Mungu ametupa Tanzania ili kuishi kwa amani na furaha, lakini sasa hali ya maisha inageuka kuwa kilio na majonzi je, nani alaumiwe?

Tujilaumu wenyewe tumeshindwa kuimiliki sayari kwa misingi endelevu, tunatumia rasilimali zilizopo husasani misitu ya asili, kwa njia zisizoendelevu, hali inayopelekea nchi kugeuka jangwa. Vilevile, upepo mkali na kutopata mvua kwa wakati uliotarajiwa lakini pia inayonyesha ni kidogo isiyowezesha mazao kustawi katika sehemu nyingi nchini.

Wachoma mkaa bila utaratibu unaokubalika kisheria, ukiwauliza kwa nini wanafanya hivyo husema wanahangaika 'kuganga njaa'. Vivyohivyo, wavua samaki kwa kutumia 'baruti' au 'sumu' au 'nyavu zisizostahili'; pia wanadai 'kuganga njaa' au kusaka riziki.

Hivi kweli matendo ya namna hiyo ndiyo njia sahihi ya kujitafutia chakula? Au ni kuikaribisha njaa? Kimsingi badala ya 'kuganga njaa' wanaofanya hivyo wanaichochea iongezeke badala ya kuikomesha. Tunapoharibu mazingira ya nchi kwa kukata miti ovyo kutokana na shughuli mbalimbali zisizozingatia kanuni za matumizi bora ya ardhi na rasilimali zilizopo kwa vyovyote tunaifukuza hali ya kuwa na neema, badala yake kuikaribisha balaa kubwa na 'njaa kali'.

Kupotea kwa kasi kubwa uoto wa asili ikiwamo misitu, ni janga kubwa kwa Watanzania kuelekea kukosa mvua za kutosha, ardhioevu ikiwamo mito, maziwa na mabwawa kujaa udongo na taka nyingine kutokana na mvua kusababisha mmomonyoko wa udongo kirahisi na kusombwa hadi mabondeni na kwenye hizo ardhioevu.

**TUFANYE HAYA**

Jambo la kupongeza ni pale serikali inapodhamiria kuifanya Tanzania ya 'kijani' (green economy), kwa kuwezesha wakulima na wafugaji kutumia eneo dogo kuzalisha chakula kingi na mazao ya mifugo ya kutosha bila kuathiri mazingira. Hili ni suala la kuwekewa mkazo sana. Vilevile, tukiongeza nguvu kwenye matumizi ya nishati mbadala kama gesi (kwa kuiwekea ruzuku ili bei iwe rafiki kwa watumiaji hasa wenye kipato kidogo na wafanyyabiashara wakiwamo mamalishe. Tutapunguza matumizi ya mkaa kwa kiasi kikubwa. papohapo, matumizi ya pikipiki kusomba mkaa kutoka porini yapigwe marufuku kisheria watakaolazimisha, pikipiki zitaifishwe.

Nimalizie kwa kuiomba serikali na wadau kuanzia Wakala wa Huduna za Misitu (TFS), Wizara ya Mali Asili, NEMC, Mamlaka ya Usafirishaji Ardhini (LATRA) na Kikosi cha Usalama suala la pikipiki kubeba magunia ya mkaa kinyume na matumizi yaliyokusudiwa, litazamwe kwa macho mapana. Waendesha pikipiki warejee kwenye matumizi halali, kubeba abiria au mizigo yao lakini siyo magunia ya mkaa.

Vilevile, Wakala wa Huduna za Misitu usitoe vibali vya kusafirisha mkaa au mazao mengine ya misitu kwa kutumia pikipiki.

Tusikubali kushindwa kuwadhibiti bodaboda, iwe ni marufuku kwa waendesha pikipiki kusafirisha mkaa. Hakuna lisilowezekana chini ya jua ni watunga sera na wafanya maamuzi kuwa na dhamira thabiti na utayari wa kutekeleza maagizo ipasavyo kwa faida ya wote.

## WANENAVYO MALENGA

### HIYO NDIYO AFYA YAKO

USIKIWEKE chochote, kwenye huo moyo wako,
Kuhusu mtu yeyote, katika maisha yako,
Ishi na raha upate, akupazo Mungu wako,
Moyo ukiwa mweupe, hiyo ndiyo afya yako.

Mungu alivyokuumba, wewe uko peke yako,
Mwingine amemuumba, naye peke yake yuko,
Kumbeba ni kasumba, ya shetani siyo yako,
Moyo ukiwa mweupe, hiyo ndiyo afya yako.

Shetani kwake Ayubu, tunasoma maandiko,
Alilionyesha gubu, kwa kile chake kicheko,
Akatafuta sababu, kwake kuleta vituko,
Moyo ukiwa mweupe, hiyo ndiyo afya yako.

Aliyofanya twajua, kuyarudia ni mwiko,
Kweli alimsumbua, yake wala siyo yako,
Nawe usijeibua, kwako mambo ya mwenzako,
Moyo ukiwa mweupe, hiyo ndiyo afya yako.

Mwenzako akikosea, kuumiza moyo wako,
Jua nawe wakosea, mbele ya Mwokozi wako,
Na ameshaelezea, ufanye sehemu yako,
Moyo ukiwa mweupe, hiyo ndiyo afya yako.

Sala kuu ni fundisho, kwangu hata pia kwako,
Fanya leo siyo kesho, kwa usalama wako,
Ni kweli si vichekesho, ndiyo uponyaji wako,
Moyo ukiwa mweupe, hiyo ndiyo afya yako.

Mungu ni msamehevu, kwa yale madhambi yako,
Lakini pia mwerevu, maagizo yako kwako,
Kama wewe ni mvivu, kusamehe doa kwako,
Moyo ukiwa mweupe, hiyo ndiyo afya yako.

Kama wewe wasamehe, pata msamaha wako,
Si Mchungaji na Shehe, aagiza Mungu wako,
Samehe kwake sherehe, pata uponyaji wako,
Moyo ukiwa mweupe, hiyo ndiyo afya yako.

Kama mtu kakuudhi, abaki moyoni mwako,
Mwingine ulimuudhi, kakupa uhuru wako,

Yako yafike kwa kadhi, unayo adhabu yako,
Moyo ukiwa mweupe, hiyo ndiyo afya yako.

Maudhi hayanabudi, kuja kila siku kwako,
Mengine kwa makusudi, yapime imani yako,
Nawe siwe mkaidi, asojua maandiko,
Moyo ukiwa mweupe, hiyo ndiyo afya yako.
(Mathayo 6:12)

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

ELIMU

NA ELIZABETH ZAYA

# Mtaala Uraia umetuangusha

## • Chanzo ushiriki duni vijana michakato kisiasa
## • Kuzorotesha maandalizi kuwa viongozi kesho



Somo la uraia-'civics' ndilo linaloanzisha vuguvugu la vijana na uongozi katika hatua za mwanzo ambao baadaye huunda umoja wa vijana wa vyama mbalimbali ndani kama ilivyo UVICCM. **PICHA: MTANDAO**

KUPUUZA somo la uraia kwa fikra kuwa halina umuhimu, huku mitaala yake ikiwa na kasoro nyingi, uhaba na uduni wa walimu wake na jinsi linavyofundishwa shule za sekondari kumesababisha vijana wengi kukosa mwamko wa masuala ya kisiasa.

Aidha, namna linavyofundishwa katika sekondari kumeathiri pia mwenendo wa vijana kujihusisha na kushiriki michakato ya kidemokrasia na kuwa na ari ya kushiriki uongozi ni kwa mujibu wa utafiti unaofanywa na Taasisi ya HakiElimu ya Dar-Es- Salaam.

Utafiti unaoangazia mchango wa elimu ya uraia shule za sekondari kumwandaa kijana kujifunza na kushiriki vema katika michakato ya kidemokrasia nchini, unabaini kuwapo kwa changamoto kubwa ya mtaala wa somo hilo.

Unaonya kuwa matokeo yake pamoja na kukosekana mazingira mazuri ya kumwandaa kijana kushiriki kwenye nyanja za demokrasia kama kiongozi wa baadaye kumezidi kushusha ari ya vijana kwenye eneo la siasa.

Aidha, imebainika kuwa uraia ni somo lisilokuwa na walimu wa kutosha na wabobezi kama ilivyo kwa mengine. Ukifanyika katika wilaya za Mkuranga, Tabora, Ukerewe, Kilwa, Sumbawanga na Arusha, utafiti unabaini ushiriki hafifu wa masuala ya kidemokrasia ndani na nje ya shule unaosababishwa na upungufu katika mtaala huo wa elimu.

"Kwa mfano, kama hakuna mwalimu mahsusi wa kufundisha somo hilo yeyote anapewa jukumu la kufundisha hata kama hajasomea uraia," anasema Mtafiti wa ripoti hiyo kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, Perpetua Kalimasi.

"Tumebaini kwamba mitaala yetu ya elimu katika somo hilo, ina changamoto, haijatilia mkazo maudhui na mbinu za ufundishaji za kuwaandaa wanafunzi kwenye mawanda mapana ya ufahamu wa somo hilo."

Aidha, wamebaini kwamba elimu ya uraia itolewayo shuleni ina mchango kidogo katika kumsaidia kijana kujifunza na kushiriki mambo ya siasa na demokrasia.

"Mfano mtaala kwenye somo hilo, kwa kiwango kikubwa haumpi mafunzo stahiki mwanafunzi yatakayomsaidia aelewe vyema na kushiriki shughuli za kidemokrasia katika ngazi mbalimbali katika nafasi yake na hata walimu wengi wanaofundisha somo hilo hawana maarifa stahiki yanayowawezesha kufundisha na kuwaandaa vijana," anasema Perpetua.

Anaongeza kuwa wanafundisha somo hilo la uraia hawana maarifa stahiki yanayowezesha kuwafundisha na kuwaandaa vijana kuelewa maana ya siasa safi na umuhimu wa ushiriki wao katika mifumo ya kidemokrasia kuanzia shuleni, nyumbani na ndani ya jamii.

"Pamoja na utafiti kuonyesha kuwa vijana wengi hutarajia kuwa shule ndiyo chanzo kikubwa cha kujifunza na kujengewa uwezo na uzoefu katika eneo la uraia na michakato yote ya kidemokrasia ukilinganisha na kutumia vyombo vya habari, lakini matarajio yao hayo yanakwama kutokana na mapungufu katika utoaji wa mafunzo ya elimu hiyo," anaeleza Perprtua.

Wanafunzi wengi wa sekondari hawana uelewa mpana wa demokrasia na umuhimu wa ushiriki wao katika kukuza ustawi na maendeleo ya taifa, anasema.

Katika ngazi ya shule utafiti unaonyesha asilimia 44.4 ya wanafunzi hawaelewi maana ya demokrasia, wakati nyingine asilimia 85.5 hawajawahi kushiriki au kushirikishwa katika vikao rasmi vya shule vinavyofanya uamuzi kuhusu mapato na mgawanyo wa rasilimali za shule.

"Asilimia 68.9 hawajawahi kugombea au kuonyesha nia ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi shuleni wakati, asilimia 44 hawashiriki katika chaguzi za uongozi wa wanafunzi na asilimia 26 hawajashiriki mdahalo na mijadala ya hoja kama sehemu ya kuwajengea uwezo wa ushawishi na demokrasia."

Anasema utafiti huo pia unaonyesha asilimia 47 ya viongozi wa shule za sekondari hawapatikani kwa njia ya chaguzi za kidemokrasia bali kwa kuteuliwa na shule, asilimia 11 kwa hujitolea wakati asilimia 42 pekee ndiyo ambayo



Kaimu Mkurugenzi wa HakiElimu, Godfrey Boniventura. **PICHA: HAKIELIMU**

hupatikana kwa kufanyika uchaguzi ambao wanafunzi wenzao hupata fursa ya kupiga kura na kwamba hali hiyo inachangia kwa kiasi kikubwa kudumaza ushiriki wa vijana katika kidemokrasia pamoja na kushindwa kuona umuhimu wake kama viongozi wajao.

Utafiti unabainisha kwamba katika ngazi ya jamii, zaidi ya asilimia 80 ya vijana walioko shuleni, hawajawahi na hawahamasishwi kushiriki mikutano ya kampeni na siasa, asilimia 67.8 hawajawahi kuhudhuria mikutano ya kijiji au mtaa na asilimia 67.5 hawajawahi na hawaoni umuhimu wa wao kushiriki shughuli za kijamii hususani zinazohusu maendeleo ya vijiji au mtaa kwa kujitolea jambo ambalo siyo jema.

"Sehemu kubwa ya jamii inashindwa kuoanisha elimu ya uraia na maandalizi ya viongozi wa baadaye na uwepo wa siasa safi, hali hii imechangia jamii kutoa hamasa kidogo kwa vijana kushiriki shughuli za siasa na demokrasia wakiwa bado shuleni. Kama jamii inapaswa kuwaandaa vijana hawa wakiwa bado wadogo ili kutengeneza viongozi wema wa baadaye katika nchi yao," anasema Kalimasi.

> "Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kutoridhika kwa vijana na namna mfumo wa elimu na jamii unavyowaandaa kuelewa na kushiriki katika mambo ya siasa na demokrasia.

"Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kutoridhika kwa vijana na namna mfumo wa elimu na jamii unavyowaandaa kuelewa na kushiriki katika mambo ya siasa na demokrasia." Anasema.

Anashauri kuwapo kwa sheria kama za uchaguzi zinazoandaa vijana kuanza kushiriki katika masuala ya siasa demokrasia ili kuleta ustawi na maendeleo ya taifa katika kasi inayotarajiwa.

Kaimu Mkurugenzi wa HakiElimu, Godfrey Boniventura, anasema taasisi hiyo inapendekeza kufanyike mapitio ya mtaala wa elimu ya uraia ili kutilia mkazo maudhui na mbinu za ufundishaji kwa ajili ya kuwaandaa wanafunzi na vijana kwenye mambo ya uraia na umuhimu wa ushiriki katika demokrasia na kupata maarifa ya uongozi mapema.

Boniventura anapendekeza kuboresha ufundishaji wa somo hilo darasani ikiwamo kusisitiza mawasiliano ya karibu zaidi kati ya walimu na wanafunzi.

HakiElimu inataja changamoto katika mtaala huo wa somo la uraia shule za sekondari, kwa kiwango kikubwa haumpi mafunzo stahiki mwanafunzi kuelewe vyema na kushiriki shughuli za siasa katika ngazi mbalimbali kwa nafasi yake.

# HABARI PICHANI



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng`wilabuzu Ludigija (wa tatu kulia), Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, SACP Wilbroad Mutafungwa (katikati), wakiongoza uzinduzi wa alama maalum za waendesha pikipiki ujulikanao kama Bafaron uliodhaminiwa na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) kwenye barabara ya Bibi Titi jijini Dar es Salaam juzi, kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Jose Moran. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mwenyekiti wa Wazee wa Chama cha TLP Taifa, Consolata Momba (kulia), akizungumza na viongozi wa chama hicho Dar es Salaam juzi, ikiwa ni sehemu ya kupanga mikakati ya kurejesha uhai wa chama hicho. **PICHA: SABATO KASIKA**



Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Calvary Assemblies of God, lililoko Ubungo Dar es Salaam, Imelda Maboya, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), wakati wa kuhitimisha wiki mbili za kuombea nchi amani juzi, pia aliiomba serikali iingilie kati mgogoro wa ardhi ulioko kati ya kanisa hilo na mwekezaji. Wengine pichani ni wazee wa kanisa hilo, Barton Mwasamengo (kulia) na Lucas John. **PICHA: SABATO KASIKA**

## CHEMSHABONGO NA -00 13 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. mwanamwali
5. eneo ambalo halioti nyasi na miti
6. korongo la maji yanayotiririka
8. Mji mkuu wa Swaziland
11.mji mkuu wa Ufilipino
13.fuata mtu
15.mbuga
16.paku, bato
17.hutengenezwa na nyuki
18.hali ya kulingana

Chini:
1. hutumika kwa kupikia, kuogea
2. neno la maumivu Afrika kusini
3. msitu mkubwa duniani
4. nchi ambayo Wahabeshi ni wenyeji
6. ugonjwa wa kichwani
7. anjaza
8. mlozi
9. elezwa
10.fahamu jambo
12.maisha ya starehe
14.minyoo ya kuvulia samaki



## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

DAKAR
UMBUA
MTOTO
UGUA
FARU
VAMIA
UMBO
TANUA
ABIRIA
JUANA
FAULU
KIBANDA
RIAKA
TAMBAA
GANDALO
FUNGA
UUZAJI

TAJA
JUA
ANU
MBU
ZOBA
UFA
AUA
OA
NUBIA
FARU
MVUA
OMBI
TIARA
URU
AUANA
INI
BA

U G U A

Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| W | A | T | A | N | G | A | Z | A | J | I |
| | S | | | | O |  | | | | B |
| | M | B | U | Z | I | | | | | I |
| | A | | M | | G | | | | | L |
| | R | | B | | O | | | | | I |
| M | A | D | I | R | I | S | H | A | | S |
| A | | | K | | | U | A | S | H | I |
| F | | L | A | L | A | M | I | K | A | |
| U | Z | I | | | M | A | B | A | B | U |
| V | | M | | F | U | K | A | R | A | |
| U | Z | A | O | | | U | | I | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | O | N | G | O | | S | | | T |
| U | N | A | A | | M | H | A | Y | A |
| N | E | N | D | A | N | A | | | B |
| G | A | D | I | | A | B | U | D | U |
| E | | I | M | A | R | I | K | A | |
| | U | | U | D | A | K | U | | K |
| M | J | A | | H | | I | B | U | A |
| K | I | C | H | A | A | | W | | T |
| O | | H | | B | U | R | A | H | A |
| A | D | A | B | U | | | | | A |



## Wapigwa marufuku kuwapangia walimu vituo kusimamia mitihani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAOFISA wilayani Mbeya, wamepigwa marufuku kuwapangia walimu vituo vya kusimamia mitihani ya ngazi mbalimbali bila kuwalipa posho za kujikimu kwa maelezo kuwa jambo hilo linasababisha mrundikano wa madeni.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alipiga marufuku hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Walimu (CWT), Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Dk. Chuachua alisema walimu wanapopangiwa vituo vya kusimamia mitihani ni lazima walipe malipo yao mapema kabla hawajaanza kazi kwa kuwa inawavunja moyo walimu hao.

Alisema madeni mengi ya watumishi hasa walimu huwa yanatengenezwa na watendaji wa ngazi za chini na kusisitiza kuwa ili kuyadhibiti ni lazima kuzuia utaratibu huo.

"Kuanzia leo sihitaji kusikia walimu wanadai posho za kusimamia mitihani, walimu ni kundi muhimu sana kwenye sekta ya elimu ambalo tusipolisimamia vizuri tunaweza tukajikuta tunaiharibu sekta hii muhimu," alisema Dk. Chuachua.

Katibu wa CWT wa halmashauri hiyo, Mwalimu Judith Mangi, alisema walimu wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mengi kwa muda mrefu ikiwamo kutopandishwa madaraja kwa muda.

Pia, wamekuwa wakilimbikiziwa madeni mengi yakiwamo yanayotokana na kuchelewa kulipwa fedha za likizo, uhamisho pamoja na malipo mengine.

Aliiomba serikali kuwalipa kwa wakati malipo yao ili kuwaongezea morali ya kufanya kazi na kuwapunguzia madeni kwenye jamii.

# Bima ya Afya kwa Wote kupunguza umaskini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MPANGO wa Bima ya Afya kwa Wote unatarajiwa kupunguza umaskini kwa Watanzania wengi wanaouza mali zao kwa lengo la kugharamia matibabu wanapougua au kuuguliwa na ndugu zao wa karibu.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, aliyasema hayo jana wakati akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa familia nyingi za kitanzania zinatumbukia kwenye dimbwi la umaskini mwanafamilia mmojawapo anapougua magonjwa yanayohitaji matibabu ya gharama kubwa kutokana na kuuza mali zao ili kumudu gharama hizo.

Alisema mpango wa serikali wa kuhakikisha kila Mtanzania anaingia kwenye mfumo wa bima ya afya utapunguza ama kumaliza tatizo la gharama za matibabu na kuzinusuru familia nyingi za kitanzania kuzama kwenye umaskini kwa kugharimia matibabu.

"Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, unalenga kuleta usawa kwenye upatikanaji wa matibabu kwa Watanzania wote, kila mtu mwenye bima ya afya atatibiwa bila kulazimika kuwa na fedha za kugharimia matibabu, hivyo hakuna yeyote atakayelazimika kuuza mali yake ili aweze kupata huduma," alisema Dk. Mbwanji.

Serikali imeshakamilisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ambao umeshafikishwa bungeni na kusomwa kwa mara ya kwanza.

Kwa upande wake Mkuu wa Divisheni ya Tiba katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Dk. Uwesu Mchepange, alisema mpango huo unakusudiwa kuongeza idadi ya Watanzania walio kwenye mfumo wa Bima ya Afya na kuwapatia uhakika wa kupata matibabu wanapougua.

Alisema kwa sasa ni asilimia 15 pekee ya Watanzania walioijiunga na mifuko ya bima ya afya huku asilimia 84 ya Watanzania wote wakilazimika kugharimia huduma za matibabu kwa kutoa fedha taslimu.

"Mpaka sasa ni asilimia 15 pekee ya Watanzania wamejiunga na bima ya afya, kati yao asilimia nane wamejiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), asilimia sita wamejiunga na Mfuko CHF na asilimia moja imejiunga na mifuko ya bima ya afya binafsi," alisema Dk. Mchepange.

Alisema yapo mataifa mengi duniani yamefanikiwa vizuri kuwaingiza wananchi wao kwenye mifuko ya Bima ya Afya ambazo ni pamoja na Rwanda iliyofikia asilimia zaidi ya 90 na Ghana iliyofikia asilimia zaidi ya 40.

Wakitoa maoni yao kwenye mpango wa bima ya afya kwa wote, baadhi ya waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya walipendekeza utaratibu huo uzingatie hali halisi ya maisha ya Watanzania maskini kwa kupanga gharama zinazoweza kulipika.

Wanahabari hao walitaka watu wasiojiweza hususan wazee wapangiwe utaratibu maalum wa kupata matibabu bila usumbufu hata kama watashindwa kulipia bima hiyo.



Mkurugenzi wa Shule ya Paradise Mission Pre and Primary School iliyoko Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, Ndele Mwaselela (kushoto), akiongozana na Mchungaji Amani Mwasote (kulia) na watumishi wa shule hiyo, katika mahafari ya kwanza ya darasa la saba shuleni hapo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# W'biashara maeneo yasiyo rasmi kuchukuliwa hatua

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

HALMASHAURI ya Busokelo wilayani Rungwe, itaanza kuwachukulia hatua za kisheria wananchi wote wanaofanya biashara kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi wakiwamo wa kwenye hifadhi za barabara.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Loema Peter, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Kamati ya Ushauri ya Programu ya Uboreshaji wa Mnyororo wa Thamani wa Kahawa, Chai na mazao ya Bustani (AGRI-CONNECT), inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU).

Aliyasema hayo wakati kamati hiyo ilipotembelea soko la mboga na matunda lililopo katika Mji wa Rwangwa lililojengwa na Shirika la HELVETAS ambalo ni miongoni mwa watekelezaji wa programu hiyo ya AGRI-CONNECT.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo wanatabia ya kuuza mboga na matunda kwenye maeneo yasiyo rasmi licha ya kujengewa soko hilo la kisasa ambalo lina miundombinu yote muhimu kwa ajili ya shughuli za biashara.

Alisema soko hilo limekuwa likijaa siku mbili za gulio kwa wiki Jumatano na Jumamosi, lakini siku zingine zote linakuwa tupu huku wajasiriamali wanaotakiwa kuuzia bidhaa zao hapo wakiendelea na shughuli barabarani.

Loema alisema ili kukomesha hali hiyo wameamua kuweka utaratibu wa kuzuia watu kufanya biashara nje ya soko hilo na wanaokutwa watatozwa faini kubwa ili kuwalazimisha kuingia kwenye soko hilo.

"Magari ya matangazo yameshapita katika maeneo yote kuhamasisha watu kuja hapa na kuwazuia kuuzia bidhaa zao barabarani, hili soko limejengwa vizuri sana la kisasa, itakuwa aibu watu wametusaidia halafu hatulitumii tunapanga bidhaa chini," alisema Loema.

Aliwataka watumishi wote wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanapohitaji mahitaji kwenda kwenye soko hilo badala ya kununua mitaani ili kuwafanya wauzaji wa mitaani kuondoka kwenye maeneo hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, alisema ameziagiza halmashauri zote mbili za wilaya hiyo kuweka utaratibu utakaowalazimisha wafanyabiashara wote wa mboga na matunda kuingia kwenye masoko.

Pia alisema soko la Tandale lililoko katika Halmashauri ya Rungwe lililojengwa na shirika hilo wananchi wanalikimbia na kuuzia bidhaa zao barabarani.

"Sio lazima mkatumia nguvu kuwaondoa, mnaweza mkaanzisha utaratibu wa kutoza ushuru mkubwa kwa wanaofanya biashara nje ya masoko haya ili iwe chaguo la mtu kuuza humu ndani ama auze nje na alipe ushuru mkubwa," alisema Dk. Anney.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuitunza miundombinu ya masoko hayo ili iwasaidie kwa muda mrefu.

Aliwataka kuhakikisha wanayafanyia usafi wa mara kwa mara ili wanunuzi wengi wavutiwe kwenda kupata huduma kwenye masoko hayo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Mpango wa Kilimo Bora kwa wanawake na vijana (KIBOWAVI-HELVETAS), Daniel Kalimbya alisema masoko hayo ni sehemu ya uboreshaji wa masoko ya bidhaa za wananchi jambo ambalo ni miongoni mwa malengo ya AGRI-CONNECT.

Alisema wamejenga masoko hayo kwa kushirikiana na halmashauri husika kwa maelezo kuwa wahandisi wa halmashauri ndiyo walioandaa michoro na kusimamia ujenzi.



# Mahudhurio ya wajawazito kliniki Bahi yaongezeka

**Na Renatha Msungu,** BAHI

MAHUDHURIO ya kliniki kwa wajawazito wa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, yameongezeka kutoka asilimia 30 hadi 90 baada ya kupata elimu ya afya ya mama na mtoto.

Elimu hiyo ilitolewa na wahudumu ngazi ya afya katika vijiji mbalimbali wilayani humo chini ya usimamizi wa serikali na Shirika la World Vision Tanzania.

Mganga Mkuu wilayani Bahi, Dk. Maira Biseko, aliyasema hayo alipokuwa akitoa takwimu za mahudhurio ya wajawazito wanaojitokeza kuanza kuhudhuria kliniki kwa ajili ya vipimo mbalimbali.

Dk. Biseko alisema kabla ya mradi huo kutekelezwa, wajawazito wengi wamekuwa wagumu kuhudhuria kliniki kutokana na kukosa elimu ya umuhimu wa kuhudhuria mapema.

"Mahudhurio ya kliniki kwa wajawazito hivi sasa yamekuwa makubwa na hii inatokana na elimu wanayopata kutoka kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii chini ya usimamizi wa World Vision na serikali," alisema Dk. Biseko.

Dk. Biseko aliwashukuru wafadhili kutoka Ireland ambao wameleta mradi huo huku wakiahidi kuendelea kuusimamia ili kuhakikisha wajawazito wanahudhuria kliniki mapema kupata elimu ya kujikinga na maradhi mbalimbali.

Alisema vijiji 13 wilayani humo vilivyofikiwa na mradi huo vimekuwa na mwamko mkubwa wa kuhudhuria kliniki kipindi wanapokuwa wajawazito na baada ya kujifungua jambo lililochangia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Naye Meneja Mradi huo, Daud Gambo, aliishukuru serikali kutokana na ushirikiano walioonesha wakati wa utekelezaji wa mradi huo katika Wilaya ya Chemba na Bahi.

Gambo alisema elimu iliyotolewa katika vituo vya afya na wahudumu wa afya ngazi ya jamii ikiwamo kuitisha mikutano ya hadhara, imesaidia wakazi wa wilaya hiyo kutambua umuhimu wa elimu kuhusu afya ya mama na mtoto.

Aliwataka wakazi wa Bahi pamoja na mradi huo kufikia ukingoni, wasiache kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili kuwasaidia kuhudhuria kliniki kipindi wanapokuwa wajawazito na baada ya kujifungua.

Mhudumu wa afya ya jamii, kutoka Kijiji cha Chilungulu, Rosa chimagae, alisema awali ilikuwa kazi ngumu kuzunguka maeneo mbalimbali vijijini kwa ajili ya kuwapa elimu wananchi umuhimu wa afya ya mama na mtoto, lakini kwa sasa jamii imeelewa umuhimu wa kuhudhuria kliniki.

"Tunaishukuru serikali kutujengea zahanati na vituo vya afya ambavyo tunavitumia kutoa elimu kwa jamii inayokuja kuhudhuria kliniki," alisema Chimagae.

Salumu Omary, mhudumu ngazi ya afya ya jamii kutoka Kijiji cha Kongogo, alisema elimu iliyotolewa kwa wananchi inasaidia kutoa mwamko kwa wanaume kuwahimiza wake zao kuhudhuria kliniki kipindi wanapokuwa wajawazito.

Alisema vijijini suala la kliniki ni tatizo, wanashukuru shirika hilo na serikali kwa kuamua kutekeleza mradi huo katika wilaya za Chemba na Bahi kwa sababu umesaidia kuleta mwamko mkubwa kwa wananchi wa umuhimu wa wajawazito kuhudhuria kliniki.




Mkurugenzi Mkuu Bohari ya Dawa (MSD), Mavere Tukai, akizungumza na waandishi wa habari ukumbi wa Idara ya Habari Maelezo jijini Dodoma jana, kuhusu masuala ya mnyororo wa ugavi wa bidhaa za afya nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vyakula vyaongeza mfumuko wa bei

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) imesema mfumuko wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2022 umeongezeka hadi asilimia 4.8 kutoka 4.6 kwa mwezi Agosti 2022.

Ongezeko la mfumuko huo limechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na zisizo za chakula ikiwamo samaki maji baridi, unga wa mahindi, mchele, maharagwe makavu, gesi ya kupikia na nguo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali, ongezeko hilo linamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2022 imeongezeka ikilinganishwa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti, 2022.

Ilifafanua baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi hizo ni pamoja na mchele kwa asilimia 0.3, mahindi kwa asilimia 4.5, unga wa ngano kwa asilimia 0.2, unga wa mahindi kwa asilimia 3.2, samaki wa maji baridi kwa asilimia 1.2, dagaa wakavu kwa asilimia 2.0, nazi kwa asilimia 3.0.

Pia karanga mbichi kwa asilimia 1.3, maharagwe makavu ya kawaida kwa asilimia 4.2 na jamii ya kombati kwa asilimia 4.9.

Kwa upande wa bidhaa zisizo za chakula zilizochangia kuongezeka ni vitambaa vya nguo kwa asilimia 0.6, nguo za wanaume kwa asilimia 0.5, viatu vya wanaume kwa asilimia 0.2, bidhaa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba kwa asilimia 1.4 na gesi ya kupikia kwa asilimia 0.4.

# Wazee waona tatizo unywaji pombe uliokithiri

**Na Mwandishi Wetu,** CHEMBA

WAZEE waishio maeneo ya vijijini wamesema unywaji wa pombe uliokirithi husababisha kutozingatia lishe na kushauri elimu itolewe ili kupunguza tatizo hilo.

Katibu wa Baraza la Wazee wa Kijiji cha Chambalo, Seleman Lumambo, aliyasema hayo wilayani hapa hivi karibuni kwenye maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Dorcas Aid International Tanzania yaliyofanyika kijijini hapo.

Lumambo alisema wazee kutokupata chakula cha kila siku kunasababisha wengi wao kuishia kunywa pombe.

Alisema kuna wazee wanalazimika kuunga mkono ukeketaji, ndoa za utotoni ili kujipatia fedha.

Kuhusu upatikanaji wa huduma za afya, Katibu huyo alisema wazee bado wanalalamika kukosa huduma za afya za uhakika kutokana na kutokuwa na uwezo wa kumudu gharama za matibabu. "Tumewasilisha kwa Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Chacha na amesema serikali inafanya kila jitihada kuhakikisha wazee wanapata matibabu na kuwaandalia dirisha maalumu kwenye vituo vya afya mbalimbali," alisema.

Mratibu wa Mradi wa Community Safety net Project kutoka Shirika la Dorcas Aid International Tanzania, Godluck Kivuyo, alisema wameamua kuwasaidia wazee kwa kuwapatia bima za afya ili kuamsha ari kwa wadau wengine kuwasaidia wazee hasa maeneo ya vijijini.

Pia alisema shirika hilo linatekeleza mradi wa wazee waliopo katika mazingira magumu kuwasaidia kupata huduma muhimu.

"Lengo la mradi huo ni kuwasaidia wazee wanaoishi katika hali duni, kuwapa tumaini wazee waliokata tamaa kwa kuwaunganisha na jamii zao pamoja na huduma mbalimbali ikiwamo huduma za afya," alisema.





## Serikali: Watakaopisha ujenzi barabara kulipwa fidia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Khadija Khamis Rajab, amewataka wananchi ambao maeneo yao yatapitiwa na mradi wa ujenzi wa barabara za mjini kutoa ushirikiano kwa wajenzi pamoja na serikali ili kufikia lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Aliyasema hayo jana baada ya kukamilika kwa kikao maalum baina ya wizara na makandarasi wa ujenzi wa barabara za mjini kutoka Kampuni ya CCECC, kilichofanyika mjini hapa.

Alisema suala la ujenzi wa barabara linahitaji usimamizi wa pamoja na kukamilika kwake kutasaidia kushajihisha harakati za maendeleo ya nchi na kuinua uchumi wa wananchi kwa ujumla.

Alisema utaratibu utakaotumika katika ujenzi wa barabara hizo ni kuandaa michoro pamoja na ujenzi, mambo yote yatakwenda sambamba huku akihimiza wananchi watakaoguswa kulipwa fidia zao kwa mujibu wa taratibu.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo Mhandisi, Shomar Omar Shomar, alisema ndani ya kipindi cha mwezi mmoja, wananchi watashuhudia harakati za ujenzi wa barabara za mjini kuanza kuonekana.

Alisema katika ujenzi huo kunaweza kusababisha usumbufu kutokana na baadhi ya barabara kufungwa, aliwataka wananchi kuwa wastahamilivu ili kuruhusu kazi ziendelee.

Kwa upande Mkurugenzi wa mradi kutoka kampuni ya CCECC, Daniel Kamau, alisema baada ya kikao hicho cha kwanza kukamilika kampuni itakwenda kutekeleza majukumu yake kwa kasi kuhakikisha kazi inakamilika kwa wakati.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, inasimamia ujenzi huo kwa karibu kufuatia kukamilika kwa zoezi la uwekaji wa saini lililofanyika Agosti 6, mwaka huu.

# Wakulima kilimo cha mwani kuongezewa thamani zao lao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imewataka wakulima wa kilimo cha mwani kuongeza uzalishaji kutokana na kuendelea kwa ujenzi wa kiwanda kitakachoongeza thamani na kusarifu zao hilo, Chamanangwe - Pemba.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, wakati akikabidhi vifaa vya mwani kwa vikundi mbalimbali vya ushirika, kisiwani humo.

Alisema serikali imejipanga kuongeza uzalishaji wa zao la mwani ambalo kwa asilimia 80 linalimwa na idadi kubwa ya wanawake vijijini.

Aidha, serikali imechukua juhudi za ujenzi wa kiwanda cha mwani ambacho kitaongeza thamani ya zao hilo na kulisarifu kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya ziada na kuongeza kipato.

"Tunajenga kiwanda kipya cha kwanza cha kusarifu na kuongeza thamani ya zao la mwani kwa wakulima wetu ambapo tunaamini kitaongeza ari ya wakulima kulima mwani kibiashara zaidi," alisema.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maji na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, alisema kituo cha utafiti wa mazao kimeanza kufanya utafiti wa zao hilo kwa ajili ya mahitaji ya matumizi ya ziada.

Alisema kwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali kituo hicho kimeanza kufanya utafiti kwa ajili ya matumizi ya ziada ya zao la mwani ili kuwaongezea wakulima kipato kikubwa.

"Kupitia taasisi ya utafiti Zanzibar tumeanza kufanya kazi za utafiti kujua mahitaji ya ziada ya zao la mwani kwa ajili ya kuongeza kipato kikubwa kwa wakulima wetu," alisema.

Ofisa Mdhamini Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba, Hakim Vuai Shein, alisema wameanza kuwahamasisha wakulima wa kilimo cha mwani kuongeza uzalishaji wa zao hilo kufuatilia ujio wa kiwanda kipya ambacho kitahitaji uzalishaji mkubwa wa mwani.

"Zoezi la ugawaji wa vifaa vya kuzalisha mwani matarajio yetu makubwa litaongeza ari kwa wakulima wetu kufikia malengo ya kimataifa," alisema.

Vifaa vilivyogaiwa kwa wakulima wa mwani ni pamoja na tari, taitai ambazo hutumika kwa ajili ya kuufunga mwani na vijiti vidogo ili kuzuia kukatika kutokana na kasi ya maji na wakati mwingine mawimbi yanayotokana na kuchafuka kwa bahari.



Adam Filipo mfanyabiashara wa madafu akimwandalia mteja wake wakati akiyauza eneo la Mlandege Mjini Unguja jana.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wahitimu vyuo watakiwa kutumia fursa kujiajiri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi wa Chuo cha Ufundi cha Glorious GPC, kutumia fursa zilizoko za mafunzo ili kujiajiri na kuondoa dhana ya kusubiri ajira serikalini.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya uzinduzi wa chuo hicho, Mpendae, Wilaya ya Mjini Unguja.

Waziri Pembe alisema chuo hicho kitakuwa mkombozi kwa vijana na jamii katika kuongeza chachu ya kuwapo kwa ajira na uchumi nchini.

Aliutaka uongozi wa chuo hicho kuongeza juhudi na mipango ili kutimiza ndoto za Wazanzibari nchini.

Pia aliwapongeza viongozi wa chuo hicho kwa kuisaidia serikali kutekeleza sera na ilani za Chama Cha Mapinduzi.

Aliwataka wanafunzi kupiga vita masuala ya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto kutokana na hivyo kuitia dosari kubwa nchi.

Alisema ni vyema wanafunzi kuwa makini kuhusu suala la udhalilishaji kutokana na kuwapo baadhi ya walimu kutumia mianya ya kutaka kuwafelisha kwa makusudi wanafunzi ili lengo lao la kuwadhalilisha litimie.

Aliwataka kuhakikisha wanawaripoti walimu wenye tabia hiyo ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao na kukomesha vitendo hivyo.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mkuu wa chuo hicho, Omar Hassan Omar, aliishukuru Serikali ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Tanzania na wadau mbalimbali wa elimu kwa ushirikiano wa kufanikisha kusimama kwa chuo hicho.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi wa chuo, Dk. Mohamed Saleh Jidawi, alisisitiza ushirikiano baina ya wanafunzi na walimu kufanya utafiti utakaosaidia jamii ili kuleta maendeleo nchini.

Mkuu wa chuo hicho, Mhandisi Dk. Idrissa Muslim Hija, alisema kuwa Chuo cha GPC kinatoa mafunzo ya sayansi ya afya, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) pamoja na mafunzo ya amali.

Alisema kuwa lengo la chuo hicho ni kuanzisha na kuleta maendeleo na mafunzo ya utafiti ili kujaza pengo lilipo nchini.





# 'Zebaki kuathiri mfumo wa fahamu wachimbaji'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MATUMIZI mabaya ya kemikali zinazotumiwa na wachimbaji wadogo kukamatia madini ya dhahabu, imetajwa kuathiri mfumo wa fahamu kwa wachimbaji hao na kusababisha mikoa ya Kanda ya Ziwa kuongoza kuwa na wagonjwa wengi wa saratani katika Hospitali ya Ocean Road, jijini Dar es Salaam.

Mkemia Mkuu daraja la kwanza kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu Kanda ya Ziwa, Bondventure Masamba, alisema hayo wakati akifunga mafunzo ya matumizi salama ya kemikali kwa wadau wa uchenjuaji wa mialo (Vat Leaching) na viwanda vya uchenjuaji wa madini iliyofanyika wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Alisema, wakati wa zoezi la ukamatishaji wa madini kwa kutumia kemikali (zebaki), wachimbaji wengi hawachukui tahadhari na baadhi yao wanalazimika kushika kwa mikono huku sumu hiyo ikiingia taratibu na kuwaletea madhara baadaye.

Pia, alisema wakati wa kuchoma dhahabu hawavai vifaa kinga na husababisha mvuke unaotokana na uchomaji wa madini na kwenda kuathiri mfumo wa fahamu na kupata saratani.

Masamba alisema, Wilaya ya Kahama ina jumla ya mialo ya madini 150, viwanda vidogo vya kuchenjua madini 13 na matumizi ya kemikali ni makubwa na kuwataka wamiliki kuwa na mifumo mizuri ya utunza maji wanayotumia ili yasifike kwenye makazi na kuharibu mazingira.

Naye mteknolojia wa maabara ya Mkemia Mkuu Kanda ya Ziwa, Zacharia Deus, aliwataka wamiliki hao kuhakikisha wanasajili shughuli zao ili kuondokana na adhabu zinazojitokeza wakati wa ukaguzi na kubainika wanaendesha shughuli bila usajili na kuleta madhara katika jamii.

Aliwataka kuacha tabia ya kuteketeza kemikali zilizokwisha muda wake kwa kuwa zinaweza kuleta madhara makubwa kwenye jamii na badala yake wahakikishe wanatoa taarifa katika Ofisi za Mkemia Mkuu wa serikali kwa kuwa kuna mtu mahusisi kwa ajili hiyo.

"Mtu binafsi akibainika kuteketeza kemikali bila kufuata utaratibu atatozwa faini isiyopungua Sh. 50,000 na isiyozidi milioni tano, kampuni ni Shilingi milioni tano na isiyozidi milioni 50 na utatakiwa kuilipa ndani ya siku 14," alisema Deus.

Awali akifunga mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya alisema, mazingira yamekuwa yakiharibiwa na wamiliki wa mialo na viwanda vidogo vya kuchenjua madini kwa kutiririsha maji wenye kemikali hadi kwenye makazi ya wananchi wakati wa shughuli zao na kupata madhara.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimia viongozi mbalimbali wa serikali alipowasili katika Daraja la Magufuli la Kigongo-Busisi kwa ajili ya kukagua ujenzi wake jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge amnusuru mwananchi kupata upofu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Manispaa ya Shinyanga, Happines William, amesimulia jinsi alivyotaka kupofuka kwa kukosa fedha za matibabu na kumshukuru Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Lucy Mayenga kwa kuleta madaktari bingwa wa macho.

Alisimulia hayo juzi wakati Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Sophia Mjema, alipokuwa akifunga kambi ya utoaji wa matibabu ya macho bure kwa wananchi wa mkoa huo kutoka kwa madaktari bingwa wa macho, iliyoanza Oktoba 14 na kuhitimishwa juzi kwa kuratibiwa na mbunge huyo.

Alisema mwaka 2013 alipokwenda kupata matibabu ya macho, aligunduliwa kuwa ana mtoto wa jicho, lakini kutokana na ukosefu wa pesa za upasuaji alikuwa akitumia dawa za macho, huku akiendelea kuathirika zaidi na kufikia hatua ya kuanza kutoona vizuri.

"Nashukuru Mbunge Lucy Mayenga kwa kuwaleta madaktari hawa bingwa wa macho, nilitaka kupofuka macho yangu yote, lakini nimefanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho bure kabisa na sasa macho ni mazima ninaona vizuri kabisa Mungu atakulipa," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, alimpongeza mbunge huyo kwa kazi kubwa ya kuratibu madaktari hao bingwa wa macho na kuahidi serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ambao wanaisaidia jamii kutatua matatizo yanayowakabili.

Aliwaomba madaktari hao kutoka Taasisi ya Bilal Muslim Mission of Tanzania Free Eye Camp, warudi tena Januari mwakani ili kutoa tiba hiyo kwa wananchi wa mkoa huo ambao wana uhitaji mkubwa.

Kwa upande wake Mayenga, alisema baada ya kuona mkoa huo una uhaba wa madaktari bingwa wa macho, aliona ni vyema aratibu suala hilo.

Mratibu wa Taasisi ya Bilal Muslim Mission of Tanzania Free eye Camp, ambaye ni kiongozi wa jopo la madaktari hao bingwa, Ain Sharif, alisema katika mkoa huo una jumla ya watu 167 waliowafanyia upasuaji wa mtoto wa jicho, huku zaidi ya watu 4,000 wakiwapatiwa matibabu ya kawaida.

# Majaliwa aagiza ulinzi mkali miradi ya kimkakati

**Na Waandishi Wetu,** MWANZA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameliagiza Jeshi la Polisi Mkoa wa Mwanza na Wilaya ya Misungwi kudhibiti wizi wa vifaa katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), kipande cha tano kutoka Mwanza-Isaka.

Alitoa agizo hilo wakati alipokwenda kukagua maendeleo ya ujenzi mradi wa huo ambayo umefikia asilimia 14 ya utekelezaji.

Alisema upotevu wa mali haukubaliki na wahakikishe kampuni hiyo inayotekeleza mradi huo haipotezi mali zao wanapojenga reli.

Alisema kwa yeyote atakayeingia kwenye wimbi la wizi wa vifaa vya ujenzi hatua kali za kisheria zichukuliwe.

Alisema Jeshi la Polisi linatakiwa kuhakikisha mkandarasi wa mradi huo hawakwamishwi kukamilisha mradi kwa sababu ya wizi wa vifaa kwa kuwa serikali imeridhia kutoa pesa nyingi leo tunataka kutengeneza hasara jambo ambalo halikubaliki na kuwataka wananchi wa Misungwi kila mmoja awe mlinzi wa ujenzi wa reli hiyo.

Aliwataka mafundi wote ambao wameshiriki katika mradi wa ujenzi huo utakapo kamilika wawe mahiri katika ufundi kulingana na kitengo alichokuwa anafanya kazi huku akitoa mfano kama ni fundi wa kuvunja nondo awe mahiri katika kipengele hicho.

Alimuhimiza mkandarasi wa mradi huo kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huo kwa kufanya kazi kwa saa 24 na kuongeza nguvu kazi ili mradi huo ambao unapaswa kukamilika Mei 24, mwaka 2024 ukamilike mapema zaidi.

Pia, Waziri Mkuu aliwataka wananchi wa Misungwi kutumia fursa ya eneo la kituo cha reli cha Fela ambacho kitakuwa bandari ya nchi kavu baada ya kukamilika kwa ujenzi wa reli hiyo kufanya uwekezaji kwa kujenga hoteli na nyumba za kulala wageni ili kujiinua kiuchumi.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, alisema reli yote imejengwa kwa kiwango cha kimataifa na ikikamilika kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza itakuwa na urefu wa kilomita 1,219 na itatumia saa nane.

Alisema kipande hicho cha tano kutoka Mwanza-Isaka, kitatumia Sh. trilioni 3.12 mpaka kukamilika huku utekelezaji ukifikia asilimia 14.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Amina Lumuli, alisema katika kipande hicho wanategemea watalaza reli takribani 500,000, hadi kukamilisha ujenzi mradi huo ambacho kitakuwa na vituo (station) 10 ikiwamo ya Fela ambacho kitakuwa bandari ya nchi kavu.

***Imeandikwa na Emmanuel, Vitus Audax na Rose Jacob**

## Waziri Bashe kuzindua ugawaji miche kahawa

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa ugawaji wa miche 3,000,000 ya kahawa aina ya Robusta.

Miche hiyo itagawiwa bila malipo kwa wakulima wa wilaya zote sita za Mkoa wa Kagera na ugawaji utazinduliwa katika Kijiji cha Karenge, Tarafa ya Kaisho wilayani Kyerwa kesho.

Mkurugenzi wa Bodi ya Kahawa (TCB), Priscus Kimaryo, alithibitisha jana kwamba tayari maandalizi yote yamekamilika na wamemwalika Waziri Bashe kuzindua ugawaji wa miche hiyo.

Miche hiyo imezalishwa na Kampuni ya JJAD Kagera Farmers kwa kushirikiana na TCB na ni awamu ya tatu ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa uzalishaji na ugawaji wa miche aina ya Robusta bure kwa wananchi ulioanza mwaka 2020.

Mkurugenzi wa Kampuni ya JADD Kagera Farmers, Dk. Albert Katagira, alithibitisha kuwapo kwa uzinduzi huo na kuwa tayari wakulima wengi wameshaanza kujisajili kwa ajili ya kupata miche hiyo ya kahawa ambayo serikali inawagawia bila malipo.

Alisema huo ni mwendelezo wa utekelezaji wa malengo ya serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye sekta ya kilimo ili kuongeza uzalishaji mazao ya kimkakati ikiwamo kahawa.

Dk. Katagira alipongeza serikali kwa kupanua wigo wa sekta binafsi wa kushiriki katika mpango mkakati wa kuongeza tija ya uzalishaji wa zao la kahawa nchini.

Mkulima wa Kahawa wilayani Kyerwa, Estavia Henry aliishukuru kampuni ya JADD Kagera Farmers na Bodi ya Kahawa kwa kutoa miche hiyo kwa kuwa itawapa wakulima motisha.

# NMB yawapeleka Uturuki wafanyabiashara kimkakati

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA 15 wanachama wa Klabu za Biashara za Benki ya NMB (NMB Business Club) waliagwa jijini Dar es Salaam jana asubuhi na kuondoka jioni kwenda Istanbul, Uturuki kwa ziara ya siku tisa kutembelea Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa (Trade Fairs 2022).

Hafla ya kuwaaga wafanyabiashara hao ilifanyika Makao Makuu ya NMB ambako Ofisa Mkuu wa Mikopo wa Benki ya NMB, Daniel Mbotto, aliwakabidhi tiketi za safari hiyo, akishuhudiwa na Ofisa Mkuu wa Huduma Shirikishi NMB, Nenyuata Menjooli na Mkuu wa Idara ya Biashara wa benki hiyo, Alex Mgeni.

Hii ni mara ya pili kwa NMB kuratibu ziara za aina hiyo, mara ya kwanza ilikuwa mwaka 2019 ambapo wafanyabiashara 10 walitembelea na kushiriki Maonyesho ya 125 ya Canton Fair 2019 yaliyofanyika mjini Guangzhou, China kabla ya janga la corona kukwamisha safari hizo miaka miwili iliyopita, yaani 2020 na 2021.

Akizungumza kabla ya kuwakabidhi tiketi za safari zao za kwenda na kurudi za ziara hiyo iliyogharamiwa kila kitu na NMB, Mbotto alisema lengo la kusafarisha wafanyabiashara hao ni kuwapa fursa ya kujifunza masuala mbalimbali muhimu kwa ustawi wa biashara zao.

Mbotto alibainisha kuwa wafanyabiashara hao watawasili Uturuki leo majira ya saa 12 kisha kesho wataanza ziara ya kutembelea maonyesho hayo ili kuwapa mwanga kibiashara na watakuwa huko kwa siku tisa wakijifunza mengi kutoka kwa wafanyabiashara wa taifa hilo kubwa linaloendelea kwa kasi kibiashara.

"Miongoni mwa maeneo watakayotembelea ni viwanda vinavyozalisha bidhaa zenye soko kubwa nchini, ambazo wana uhusiano nazo, wakitarajiwa kuona uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo vifaa tiba, vifaa vya ujenzi, nguo na vipodozi," alisema Mbotto.

Alivitaja vigezo vilivyotumika kupata wafanyabiashara hao kuwa ni pamoja na historia yao nzuri ya ukopaji na urejeshaji mikopo, kupitisha biashara zao kwa asilimia 95 katika Benki ya NMB, kusaidia kwao kuunganisha wafanyabiashara kujiunga NMB na uwezo wa kuchangia asilimia kidogo za safari.

Mbotto aliwataka wafanyabiashara hao kuhakikisha ziara hiyo inaleta mabadiliko yao kibiashara, kutumia vyema kila fursa watakayoiona na kurejea nyumbani wakiwa na ujuzi mkubwa na kutanua mtandao wa kibiashara ili kukuza biashara zao na uchumi wa taifa.

Mwakilishi wa wafanyabiashara 15 walio katika msafara huo, Paulo Lema aliishukuru NMB kwa fursa mbalimbali inazotoa kwa wateja wao wa kada mbalimbali katika kuwaongezea nguvu ya kukua kiuchumi na kusisitiza kuwa kadri wanavyoshikwa mkono, wanarahisishiwa ukuaji wao kibiashara.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara waliopata fursa kama hiyo mwaka 2019, Award Mpandila, Mwenyekiti wa NMB Business Club Mkoa wa Dar es Salaam, alikiri kuwa ziara yao katika Maonyesho ya Canton Fair imewasaidia kubadilika kimfumo, kiuendeshaji na ufanyaji biashara.

"Ni ziara ambayo ilitupa faida mbalimbali ambazo zimekuwa chachu za ukuaji wetu kibiashara kitaifa na kimataifa na kwa sasa tumefikia hatua ya kutia saini mikataba mbalimbali na wenzetu kutoka mataifa yaliyoendelea na hivyo kuisaidia Tanzania ya Viwanda inayochakatwa na serikali.

"Uwezeshaji tunaoendelea kuupata kutoka NMB ni mkubwa na wenye tija kwa biashara zetu, kampuni zetu, taasisi na mashirika yetu. Wito wangu kwenu mliopata fursa hii mwaka huu, tambueni mnawawakilisha maelfu ya wafanyabiashara na hivyo mkawe mabalozi wema wa benki huko Uturuki," alisema.

MWANGA HAKIKA BANK

DEFINING TOMORROW TODAY

## NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**MAJEMBA COMPANY LIMITED, MOPEH COMPANY LIMITED** na **STEAM GENERATION RECOVERIES LTD** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED**, tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | UMABAMABA | UMABAMABA | BAJAJI MC 320 CVU | MABWEPANDE, DAR ES SALAAM | 05-11-2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MAJEMBA COMPANY LIMITED |
| 2 | UMABAMABA | UMABAMABA | BAJAJI MC 374 CVU | MABWEPANDE, DAR ES SALAAM | 05-11-2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MAJEMBA COMPANY LIMITED |
| 3 | UMABAMABA | UMABAMABA | BAJAJI MC 661 DBV | MABWEPANDE, DAR ES SALAAM | 05-11-2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MAJEMBA COMPANY LIMITED |
| 4 | UMABAMABA | UMABAMABA | BAJAJI MC 727 CVU | MABWEPANDE, DAR ES SALAAM | 05-11-2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MAJEMBA COMPANY LIMITED |
| 5 | UMABAMABA | UMABAMABA | BAJAJI MC 610 CWG | MABWEPANDE, DAR ES SALAAM | 05-11-2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MAJEMBA COMPANY LIMITED |
| 6 | KIHINDA ALLY BALEWA | KIHINDA ALLY BALEWA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA; TMK034811 | KIZINGA, MBAGALA WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 01-11-2022 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA | MOPEH COMPANY LIMITED |
| 7 | MWEMA KHAMIS MWAVURA | MWEMA KHAMIS MWAVURA | GARI NO. T696 CFP - TOYOTA NOAH. | MBEZI BEACH, WILAYA YA KINONDONI | 04-11-2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |
| 8 | PRIMUS M TARIMO | LILIAN MWAKILASA ATHANASI | NYUMBA YENYE HATI NA. C.T.NO. 42315, L.O.NO.313307, KIWANJA NA. 61. | SOKONI 1, ARUSHA | 05-11-2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**MAJEMBA COMPANY LIMITED**
P.O Box 10031
Arusha
Tel: 0785934209/ 0754929299
Email: majembacompany2o@gmail.com

**MOPEH COMPANY LIMITED**
P. O. Box 32372
Dar es Salaam
Tel: 0785335544, 0673335528, 0755731072
Email: mopehltd20@gmail.com

**STEAM GENERATION RECOVERIES LTD**
P. O. Box 80607
Dar es Salaam
Tel: : +255 715 91 74 51
Email: steam@steamtz.com

**MANAGING DIRECTOR**
MWANGA HAKIKA BANK LIMITED
P.O.BOX 11735
Dar es Salaam
Tel: 0747666511

217099202

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDULRAZAK ABDALLAH** KIMARO anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya MITSUBISH CANTER yenye usajili namba **T328 CSV,** CHASSIS NAMBA **FE538B520398,** ENGINE NAMBA: **4D3326514.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/406187/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI**
**Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na.1946/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU KASSIM ALLY ABDALLAH**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SIWEMA RASHID MBIMILE**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo )**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 25 mwezi 10 mwaka 2022 saa 4 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Imetolewa leo tarehe 11 mwezi 10 mwaka 2022

HAKIMU
HON- RACHUA

---

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ABIGAEL BENSON MWAMKOMBA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S0867-0705 (ACSOS6057)** iliyotolewa na PANDAMBILI SEKONDARI mwaka 2022. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MBE/KYE/RB/401771/2022.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI NAMBA 23/2022**
**GEOFREY FUNGO...........................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**PRISCA LUGOME.....................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi unataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako. Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 31/10/2022 saa 2:00 asubuhi. Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa Barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04/10/2022

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**SONGEA**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**JABIRI MOHAMED SHABANI**

Anatangaza kupotolewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC. 823 BPP.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi. **KAH/TR/RB/671/2022.**

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**ESTHER BENY MASUNGA** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma : cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4556-0015 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST CLARA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2015** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0263-0515** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **VISITATION GIRLS' SECONDARY SCHOOL** mwaka **2018.** Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/KIJ/RB/403570/2022**

---

**MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Amri ya Mahakama ya Mwanzo Chamwino Mjini nitauza **NYUMBA Plot no. 34 Block K Chidachi west, na Gari RV4 Old Model T 680 DEK Chumo la ndoa ya SARAH MKUMBO na NOTKA BANTEZE** kutokana na shauri la Madai ya ndoa namba 36 ya mwaka 2018 Muda wa mnada ni saa 4:00 Asubuhi. Mnada wa nyumba utafanyika mahali Nyumba ilipo, mnada wa gari utafanyika uwanja wa makole shule ya msingi.

**MASHARTI YA MNADA**

- Mnunuzi atalipa 25% siku mnada na 75% atailipa ndani yay a siku 14
- Mnada utafanyika mahali nyumba ilipo/kiwanja kilipo
- Gharama za kubadili ya umiliki ni juu ya mnunuzi

**Unaruhusiwa kuona mali ya kabla ya siku ya mnada, piga 0715 170 553**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TEMEKE**

**WILAYA YA TEMEKE**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 288 YA 2022**

**NANDALA YAKONGO NA WENZAKE......WADAI/MDAI**

**DHIDI YA**

**HASSAN RAJABU KHATIBU......MDAIWA/WADAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

**HASSAN RAJABU KHATIB..... POPOTE MLIPO/ULIPO**

**NANDALA YAKONGO NA WENZAKE** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Temeke (Usalama). Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 20/10/2022 saa 3:00 asubuhi/m-chana. Unatakiwa ufike/mfike wewe/nyinyi au wakili wako/wenu mwakilishi wako/wenu pasipo kukosa.

**AMRI** hii imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 17 mwezi wa 10 mwaka 2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA TEMEKE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - MWANZA**

**SHAURI NAMBA 379 LA 2022**

**ELIABU BWIRE PALAPALA.....................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SERIKALI YA KIJIJI CHA MISASI........MJIBU MAOMBI**

**KWA:SERIKALI YA KIJIJI CHA MISASI**

UNAFAHAMISHWA KWAMBA MLETA MAOMBI HAPO JUU AMEFUNGUA SHAURI/OMBI DHIDI YAKO KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MKOA WA MWANZA. OMBI HILI LIMEPANGWA KUTAJWA TAREHE 19/10/2022 KATIKA CHUMBA CHA BARAZA, BARABARA YA MAKONGORO JENGO LIKO MKABALA NA MAHAKAMA YA MWANZO MWANZA MJINI NA MAHAKAMA YA WILAYA NYAMAGANA, TANZANIA. UNATAKIWA KUWEPO, AU KUWAKILISHWA KISHERIA PAMOJA NA KULETA UTETEZI WAKO DHIDI YA SHAURI LAKO. KAA-UKIJUA KWAMBA KUSHINDWA KUFIKA, BARAZA LITASIKILIZA OMBI HILO NA KUTOA UAMUZI BILA WEWE KUWEPO. HATI HII IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA CHAPA YA BARAZA LEO TAREHE 17/10/2022

MAYEYE S. M.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
MWANZA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KOROGWE**
**YAH: MAOMBI MADOGO NA.10 YA MWAKA 2022**
**(Asili ya shauri la madai na. 76/2011 kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba Korogwe)**
**MALIKI ABEDI KAMOTE.........MSHINDA TUZO**

**DHIDI YA**
**SILAS RAPHAEL LUKOMBESO ....MSHINDWA TUZO**

**WITO**

SILAS RAPHAEL LUKOMBESO, popote ulipo, unafahamishwa kuwa MALIKI ABEDI KAMOTE amefungua shauri (Kazio la hukumu) mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Korogwe dhidi yako lenye na.10/2022. Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 31/10/2022 saa 2:30 asubuhi. Hivyo basi unatakiwa kufika siku hiyo. Vielelezo vya kesi vinapatikana katika masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Korogwe. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na maamuzi kutolewa dhidi yako.
Ofisi za Baraza zipo wazi karibu na jingo la Waalimu (CWT).
AMRI hii imetolewa na kutiwa saini na mhuri/lakiri ya Baraza hili

**MHINA E.R**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**KOROGWE**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.....13.....OF 2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE YASSIN BAKARI GEMBE**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATION**

**BY NEEMA JONAS MAEDA**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be field on or before the 03 day of November 2022
Dated at Korogwe this 13 day of October 2022

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
KOROGWE

---


# Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Harmonize amjaza 'misifa' Burna Boy

**Na Mwandishi Wetu**

MKALI wa Bongo Fleva, Harmonize, amesema kwa sasa Burna Boy ndiye msanii mkubwa duniani na kusema kuwa wapambanaji pekee ndio wanaweza kumuelewa huku akijitaja kuwa yeye anafuata nafasi ya pili.

Kupitia instastory yake Harmonize ameweka ujumbe akisema kuwa kwa sasa Burna Boy ndiye msanii mkubwa huku akitaja baadhi ya matukio aliyojifunza kutoka kwa nyota huyo kipindi yupo jijini Lagos, Nigeria.

"Sijawahi kumsikia Burna Boy akijisifia juu ya mafanikio yake na tuzo alizonazo, yeye ndiye bora duniani kwa sasa.

"Halafu baada ya Burna Boy mimi ndiye nashika nafasi ya pili kwa ubora," aliandika Harmonize.

Mbali na hilo, Harmonize amesema kuwa hawezi kuficha kusema ukweli kwamba kwa sasa Burna Boy ndio msanii namba moja, huku akisisitiza kila mtu anaweza kutaja jina la staa anayeona yeye ndiye namba moja, lakini wasisahau kuwa yeye anafuata.





# MOBETO: MIMI NI CHOMBO

**Na Mwandishi Wetu**

MWANADADA mjasiriamali na msanii wa Bongo Fleva, Hamisa Mobeto, amesema kwamba, mume wake amepata chombo kikali.

Mobeto ambaye kwa sasa yupo kwenye maandalizi ya kufunga ndoa, amesema yeye ni msichana mrembo sana na hivyo mume wake atafaidi mno.

Miezi kadhaa iliyopita, Hamisa alidai kupewa zawadi ya gari la kifahari aina ya Range Rover Evoque na mpenzi wake ambaye hajamuweka wazi hadi sasa.

Hamisa ambaye ni staa wa muziki, filamu na mitindo anasema anajiandaa na ndoa, lakini kikubwa anachojua ni kwamba mwanaume anayemuoa atakuwa amepata chombo safi.

"Mimi ninachojua mwanaume wangu anayenioa amepata chombo," amesema Mobeto ambaye ni mama wa watoto wawili wa baba wawili tofauti, Diamond Platinum na mfanyabiashara Majizo.

# *Shilole atoa sababu kuzidi kunenepa*

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa kike wa Bongo Fleva na Bongo Muvi, Zuwena Mohammed maarufu Shilole, amefunguka sababu ya kunenepa sana.

Shilole ambaye anafanya biashara ya chakula, amebainisha kwamba tabia yake ya kula mara kwa mara ndio inamfanya anenepe sana.

Shilole ambaye ni mjasiriamali, alisema alikuwa na kilo 108, lakini sasa amepunguza kilo sita na kubaki na 102 huku akiweka wazi kuwa akiamka anakunywa supu asubuhi na baadaye usiku anakula wali nazi.

"Hata ungekuwa wewe jamani naamka na vyakula vizuri kwenye mgahawa wangu asubuhi supu ya kuku, ulimi, bado usiku namaliza na wali nazi sina mkopo sina 'stress', napata mapenzi mazuri kwa mwenza wangu kwa nini nisinenepe," alisema Shilole.

"Natamani kupungua, lakini kila nikianza mazoezi nafikiria chakula ninachokula kwa sababu siwezi kuacha, napenda kula kwa sababu mimi muda wote nashinda na vyakula."

Alisema kutokana na mwili wake, anashindwa kufanya mambo aliyokuwa akiyafanya miaka ya nyuma kwenye majukwaa kwa kufanya matamasha makubwa ambayo alikuwa anatumia mwili wake mdogo kucheza vizuri.



HABARI MICHEZO

# SABABU KIPIGO TIMU YA WATOTO WA MITAANI KOMBE LA DUNIA

Na Enock Charles

BAADA ya mwaka huu kushindwa kufurukuta kwenye michuano ya Kombe la Dunia kwa Watoto wa Mitaani, Kocha wa Timu ya Tanzania ya Watoto wa Mitaani, Fulgence Novatus, amesema changamoto ya tofauti ya hali ya hewa waliyokutana nayo nchini Qatar ni moja ya sababu iliyowafanya kutolewa katika hatua ya robo fainali.

**Akizungumza na waandishi wa habari juzi wakati timu hiyo ikirejea kutoka nchini Qatar ilipoenda kushiriki mashindano hayo, Novatus alisema kutokana na joto kali wachezaji wake walishindwa kupambana ipasavyo mbele ya wapinzani wao.**

"Miaka yote ya nyuma tumekuwa tukitolewa katika hatua ya fainali, lakini sasa tumetolewa katika hatua ya robo fainali kwa kweli ni hatua ndogo ikilinganishwa na miaka ya nyuma, lakini moja ya changamoto ni hali ya hewa kwetu sisi msimu huu haikuwa rafiki.

"Kingine ni kwamba nchi zimekuwa zikijipanga vizuri kila unapofika wakati wa mashindano kwa sababu na sisi tuliamini kwamba kila mwaka lazima tucheze hatua ya fainali kumbe na nchi nyingine zinajipanga, unaona nchi kama Pakistan hii ni awamu yake ya pili anacheza fainali ingawa hajafanikiwa kuwa bingwa," alisema.

Kocha huyo aliwaomba wadau wengi zaidi kujitokeza kuifadhili timu hiyo ya Watoto wa Mitaani ili kufikia ufanisi unaotakiwa kwa kuwa kwa sasa ina mfadhili mmoja, Altaf Mansoor kutoka Kampuni ya Moil.

Timu ya Tanzania katika mashindano hayo ilitolewa katika hatua ya robo fainali na Pakistan kwa kufungwa mabao 2-1, hivyo kushindwa kuendelea katika hatua inayofuata huku timu ya Misri ikiibuka mabingwa katika mashindano hayo baada ya kuifunga Pakistan kwenye mechi ya fainali.

Ofisa Michezo kutoka Baraza la Michezo nchini (BMT), Charles Maguzu, alipongeza timu hiyo kwa niaba ya serikali na kuitaka kujipanga vema kwa msimu ujao wa mashindano hayo mwaka 2026 na kualika wadau zaidi kuishika mkono kwa vifaa na rasilimali fedha ili iweze kufanya vizuri zaidi msimu ujao.

Pia Maguzu aliwapongeza Watanzania waliopo nchini Qatar kwa kujitokeza kuishangilia timu hiyo na kuwaomba wengine kufanya hivyo mwaka 2026 kwa watakao kuwa katika nchi yatakapofanyika mashindano hayo.

Michuano ya Kombe la Dunia kwa Watoto wa Mitaani, hufanyika kabla ya Kombe la Dunia na kwenye nchi ambayo michuano hiyo ya dunia hufanyika.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Moil ambaye ni mfadhili wa Timu ya Tanzania ya Watoto wa Mitaani, Altaf Mansoor (wa tatu kulia), akiwa na Kocha wa timu hiyo, Fulgence Novatus, pamoja na wachezaji wa kikosi hicho juzi waliporejea kutoka nchini Qatar kwenye michuano ya Kombe la Dunia. **PICHA: ENOCK CHARLES**

# *Mbuni yachinjiwa Tanga Championship*

Na Adam Fungamwango

BAADA ya ushindi wa mechi nne mfululizo bila kuruhusu bao lolote, hatimaye timu ya Mbuni FC imepoteza mchezo wa kwanza kwenye Ligi ya Championship, kutokana na kuchapwa mabao 2-0 juzi dhidi ya African Sports, katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Ulikuwa ni ushindi wa kwanza wa African Sports kwenye ligi hiyo, baada ya kucheza mechi nne ikipoteza moja na kutoka sare tatu, kabla ya kushinda juzi.

Hata hivyo, pamoja na kufungwa mechi hiyo, Mbuni bado inaendelea kuongoza ligi ikiwa na pointi 12, kwani timu ambayo ilikuwa inafukuzia uongozi wa ligi hiyo, Fountain Gate nayo ilipotea mechi ya kwanza kwenye ligi hiyo, ilipofungwa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam.

Fountaine Gate nayo pia imebaki na pointi 12, lakini imezidiwa mabao ya kufunga na Mbuni FC.

Kwenye mechi zingine, timu ya Pamba imepata ushindi wa mabao 2-1 ugenini dhidi ya Gwambina FC, Biashara United ililazimishwa sare kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Karume, Musoma mkoani Mara ya bao 1-1 dhidi ya Copco, Greeen Warriors ikatoka suluhu dhidi ya Ndanda, Mashujaa pia ikiwa nyumbani Uwanja wa Lake Tanganyika Kigoma, ilitoka suluhu dhidi ya Kitayosce.

Wakati Mbuni na Fountain Gate zikiwa na pointi 12 kila moja, timu za Kitayosce na Mashujaa zina pointi 11 kila moja, lakini Kitayosce ikiwa juu kwa idadi ya mabao ya kufunga, JKT Tanzania na Pamba zote zina pointi tisa, ila maafande wanakaa juu kutokana na tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

JKT Tanzania ipo kwenye nafasi ya tano kutokana na kuwa na mabao manne ikifunga moja, Pamba ina mabao saba, lakini imefungwa idadi hiyo ya mabao, hivyo imetupwa kwenye nafasi ya sita.

# Tamasha la Busara lapata mdhamini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAMASHA la muziki la kimataifa la Afrika Mashariki la Sauti za Busara limepata mdhamini ambaye atalidhamini ili kuendelea kufanyika visiwani Zanzibar kwa muda wa miaka mitatu mfululizo.

Kampuni ya CPS inayojenga Mji Mpya wa Maendeleo wa Fumba Town, ndiyo ilijitokeza kudhamini tamasha hilo ambalo linakuza vipaji vya wasanii na tayari utiaji saini wa mkataba wa udhamini huo umefanyika na kushuhudiwa na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Muhammed Said.

Akizungumza baada ya hafla hiyo ya utiaji saini iliyofanyika jana Fumba nje ya Mji wa Zanzibar, Waziri Simai alisema tangu Tamasha la Sauti ya Busara lilipoanzishwa zaidi ya miaka 20 sasa, limekuwa na mchango mkubwa katika kutangaza sekta ya utalii pamoja na utamaduni wa muziki na ngoma za asili nchini.

"Niwaombe wasanii wa Zanzibar kulitumia tamasha hili ili kutambulika na kuonekana duniani kwa kuwasilisha kazi zenu na kutoa burudani katika tamasha hilo," alisema.

Aidha, alisema ni vema mkataba huo iwe ni fursa kwa matamasha mengine madogo kutafuta wadhamini ili matamasha hayo yaendelee kuleta tija.

"Serikali inakusudia kuanzisha mfuko wa kuendeleza utamaduni nchini ambao sehemu ya majukumu yake ni kusaidia kuimarika kwa matamasha ambayo moja kwa moja lengo lake ni kutangaza sekta ya utalii duniani kote," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tamasha la Sauti ya Busara Zanzibar, Mahmoud Yussuf, alisema malengo ya tamasha hilo ni pamoja na kutangaza utalii wa Zanzibar, lakini ni kukuza vipaji vya wasanii na utamaduni wa mambo ya kale nchini.

Alisema matarajio yao makubwa ni kuona tamasha hilo linaimarika zaidi kwa kuibua vipaji vya wasanii wadogo pamoja na utalii wa Zanzibar ikiwamo mambo ya kale.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini huo, Ofisa Mkuu wa Masoko wa Kampuni hiyo, Tobias Dietzold, alisema wameamuwa kudhamini Tamasha la Busara kwa kutambua mchango wake mkubwa katika kukuza sekta ya utalii.

Tobias alibainisha kuwa wamejitolea kufanya tamasha hilo ili kuwa imara na lenye nguvu kwa miaka ijayo wanapofurahia urithi wa kiutamaduni wa aina mbalimbali kupitia muziki wa moja kwa moja (mubashara).

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO AKATALIWA

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe amekataa kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na Ureno, Cristiano Ronaldo kwa sababu ya umri wa mchezaji huyo mwenye miaka 37. Ronaldo alisaini mkataba wa mwaka mmoja wa kuichezea klabu hiyo. ***(90min)***

### MBAPPE NA KUTUA CITY

MANCHESTER City haitakumbana na vikwazo vya kifedha katika kumsajili fowadi wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, ambaye anataka kuondoka Paris St-Germain licha ya kusaini mkataba mpya msimu wa majira ya joto. ***(Marca)***

### SOUTHGATE BONASI KUBWA

KOCHA wa England, Gareth Southgate anaweza kukusanya bonasi ya pauni milioni nne ikiwa atawaongoza 'Simba Watatu' hao kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia nchini Qatar. ***(Sun)***

### LOFTUS-CHEEK ATAKIWA MILAN

AC Milan wanaweza kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea na England, Ruben Loftus-Cheek mwenye umri wa miaka 26, wakati wa dirisha la Januari. ***(Calciomercato)***

### BONUCCI ATAJWA SPURS

MLINZI wa kati wa Juventus na Italia, Leonardo Bonucci mwenye umri wa miaka 35, amehusishwa na uhamisho wa kujiunga na Tottenham Hotspur baada ya kuomba kuuzwa katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Football Italia)***

### CHELSEA NA NYOTA WAKE

CHELSEA walikuwa wakipanga kumpa beki wa kulia wa England, Reece James mwenye umri wa miaka 22, na kiungo wa kati, Mason Mount mwenye miaka 23, mikataba mipya ya muda mrefu na klabu hiyo, hata kabla ya kuuzwa kwa timu hiyo kwa kundi la makampuni ya mwekezaji Mmarekani, Todd Boehly mwezi Mei. ***(CBS Sports)***

### MANE SI SABABU LIVER

MLINZI wa Liverpool na Uholanzi, Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 31, amesema kuondoka kwa fowadi wa Senegal, Sadio Mane, 30, kwenda Bayern Munich si sababu ya wao kuanza vibaya msimu huu wa Ligi Kuu ya England. ***(Sky Sports, via Mail)***

### STRUIJK MKATABA MPYA

BEKI wa Uholanzi, Pascal Struijk, 23, amesema anataka kusaini mkataba mpya na Leeds United. ***(Voetbalzone)***

### CHELSEA, EDWARDS BADO

CHELSEA imepata pigo katika jaribio lao la kumsajili mkuu wa zamani wa uhamisho wa Liverpool, Michael Edwards mwenye umri wa miaka baada ya yeye kutaka muda wa kufikiria chaguo lake. ***(Sun)***

### PJANIC AFUNGUKA YA BARCA

KIUNGO wa kati wa Bosnia na Herzegovina, Miralem Pjanic amesema kocha wa Barcelona, Xavi alitaka abaki katika klabu hiyo na kwamba ulikuwa uamuzi wake mwenyewe kuondoka hapo Nou Camp na kujiunga na klabu ya Emirati Sharjah katika dirisha la usajili la majira ya joto. ***(beIN, via 90min)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE: MIMI SIJAWAHI KUOMBA KUONDOKA PSG

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amesema ripoti kwamba yeye anataka kuondoka Paris Saint-Germain Januari si "za kweli kabisa."

**Mbappe, ambaye alifunga bao pekee kwenye ushindi wa 1-0 wa PSG wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, dhidi ya Marseille, Jumapili, aliripotiwa kuwa anahisi kusalitiwa na uongozi wa klabu hiyo.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, aliyeshinda taji la Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, alitia saini mkataba mpya Mei mwaka huu, baada ya miezi kadhaa ya mashaka, lakini aliripotiwa kutokuwa na utulivu kwa mara nyingine baada ya kushindwa kutimiziwa matakwa yake yaliyopo kwenye mkataba wake mpya.

Mkurugenzi wa Soka wa PSG, Luis Campos, alikanusha kwa msisitizo taarifa hizo kwa kudai Mbappe hajaifahamisha klabu hiyo kuhusu nia hiyo, huku Kocha Mkuu, Galtier pia akishangaa uvumi huo.

> ●●● Taarifa zilitoka siku ya mechi, sikuelewa, sijahusika hata kidogo na habari hii...

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa sasa ametoa la moyoni kuhusu ripoti hiyo, ambayo iliibuka muda mfupi kabla ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ya PSG dhidi ya Benfica Jumanne, na amesisitiza kuwa si za kweli.

"Nina furaha sana, sikuwahi kuomba kuondoka Januari," alisema, akizungumza na vyombo vya habari vya Ufaransa.

"Taarifa zilitoka siku ya mechi, sikuelewa, sijahusika hata kidogo na habari hii, nilishituka kama kila mtu.

"Watu wanaweza kudhani nahusika, lakini sihusiki kabisa, nilikuwa nalala usingizi. Wapambe wangu na watu wote wanaonihudumia tulishangaa sana.

"Baadaye, tulilazimika kukabiliana nayo, kulikuwa na mchezo wa kucheza. Kusema tu ni makosa kabisa, na nina furaha sana."

Mbappe alikuwa akilengwa na Real Madrid kabla ya kukubali kuongeza muda wa kukaa Paris.

Alisema: "Mimi ni mchezaji wa mpira wa miguu, jambo la muhimu kwangu ni kucheza na kujituma kwa uwezo wangu wote uwanjani.

"Unapocheza PSG, unajua unachoingia nacho, kitahusisha nini katika mazuri na mabaya. Unapaswa kuwa tayari.

"Wale wanaokuja hapa wanajua, tunawaonya. Tuko sawa kwa sasa, lakini tunalenga kushinda michezo na mataji."

Mbappe ameanza msimu huu akiwa na kiwango kizuri mbele ya lango, akifunga mabao 12 katika michezo 14 katika michuano yote akiwa na mabingwa hao wa Ufaransa.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 374,

MECHI KALI
CRYSTAL PALACE
VERSUS
WOLVERHAMPTON
1 | 2.16
X | 3.22
2 | 3.27

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# KLOPP: NILISTAHILI KADI NYEKUNDU

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amekiri kwamba, alistahili kupewa kadi nyekundu dhidi ya Manchester City, lakini kocha huyo wa Liverpool akasikitishwa na aina ya maamuzi kwenye mchezo huo wa ushindi wa bao 1-0 wa timu yake kwenye Uwanja wa Anfield.

Mohamed Salah alifunga bao pekee katika mchezo huo wa Jumapili, akiunganisha pasi ndefu kutoka kwa Alisson zikiwa zimesalia dakika 14 na kumfunga Ederson.

Kilikuwa ni kipigo cha kwanza kwa City katika Ligi Kuu ya England msimu huu, lakini wageni hao walishangazwa baada ya bao la Phil Foden kipindi cha pili kukataliwa na mwamuzi, Anthony Taylor.

Katika mapitio ya VAR ilionyesha Erling Haaland akimvuta Fabinho wakati Foden akipata mpira na kufunga bao.

Kocha wa City, Pep Guardiola na Klopp wote walionyesha kuchanganyikiwa na maamuzi ya Taylor kwenye mchezo huo.

Na Klopp alionyeshwa kadi nyekundu baada ya kupaza sauti kudai Salah alifanyiwa faulo zikiwa zimesalia dakika tano.

"Ndio, ni juu ya hisia bila shaka... kuhusu kadi nyekundu, kweli ni kosa langu," alisema Klopp katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi hiyo.

"Maamuzi ya mwamuzi hayakuwa sawa, uliona wote wawili mimi na (Pep) tulionyesha kuchanganyikiwa na mechi ilikuwa ngumu.



# Ancelotti awapigia salut wachezaji Real Madrid

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti aliwamwagia sifa Real Madrid kwa kufanya "mechi kamili" wakati 'Los Blancos' walipowafunga Barcelona mabao 3-1 kwenye mchezo wa Clasico Jumapili.

Kikosi cha Ancelotti sasa kimeshinda mechi sita kati ya saba zilizopita dhidi ya Barca katika michuano yote, baada ya mabao ya Karim Benzema, Federico Valverde na Rodrygo pale kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu.

Na sasa Los Blancos wapo kileleni mwa msimamo wa ligi kwa tofauti ya pointi tatu.

Na Muitaliano huyo alifurahishwa na ujasiri na udhibiti ulioonyeshwa na wachezaji wake.

Alipoulizwa nini kilikuwa chanzo cha ushindi wa timu yake, aliiambia DAZN: "Kila kitu. Ilibidi tufanye m chi kamili, na tulifany hivyo.

"Ni kweli mwan ulikuwa mzuri, tulita gulia mapema na tuli hibiti vema kipindi ch pili. Tulijiamini sana.

"Ilikuwa wazi kwar ba (Eder) Militao a lazimika kumdhib vilivyo Robert Lewa dowski. Tulidhib wachezaji vema kati y safu na Toni Kroos r Aurelien Tchouam ni."

,935,160

# JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/10/22 | 20:00 | Cadiz CF vs Betis | 2.85 | 3.25 | 2.43 |
| 02. 19/10/22 | 20:00 | Valladolid vs Celta Vigo | 2.47 | 3.19 | 2.85 |
| 03. 19/10/22 | 20:00 | AIK Football vs BK Hacken | 2.39 | 3.40 | 2.58 |
| 04. 19/10/22 | 21:30 | Bournemouth vs Southampton | 2.72 | 3.27 | 2.46 |
| 05. 19/10/22 | 21:30 | FC Luzern vs St. Gallen | 2.50 | 3.55 | 2.55 |
| 06. 19/10/22 | 21:45 | Wigan vs Middlesbrough | 2.54 | 3.19 | 2.69 |
| 07. 19/10/22 | 21:45 | Mechelen vs Standard Liege | 2.54 | 3.39 | 2.59 |
| 08. 19/10/22 | 22:00 | Millwall vs Watford | 2.71 | 3.20 | 2.51 |
| 09. 19/10/22 | 22:15 | Manchester Utd vs Tottenham | 2.23 | 3.42 | 2.94 |
| 10. 20/10/22 | 20:00 | Almeria vs Girona | 2.35 | 3.20 | 3.00 |
| 11. 20/10/22 | 20:00 | Degerfors vs IFK Goteborg | 2.73 | 3.32 | 2.31 |
| 12. 20/10/22 | 21:00 | Osasuna vs Espanyol | 2.22 | 3.20 | 3.25 |
| 13. 20/10/22 | 21:30 | Fulham vs Aston Villa | 2.77 | 3.22 | 2.45 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 18/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1575 | FK Lviv vs Veres Rivne | 2.74 | 3.13 | 2.41 |
| 15:00 | 4549 | Oleksandria vs FC Kryvbas Kriviy Rih | 1.66 | 3.60 | 4.58 |
| 15:30 | 2136 | Juve Stabia vs Foggia | 2.08 | 3.20 | 3.60 |
| 15:30 | 3503 | FCM Alexandria vs Farul Constanta | 7.01 | 4.58 | 1.35 |
| 18:00 | 2971 | Lokomotiv Moscow vs FK Khimki | 1.45 | 4.28 | 5.65 |
| 19:00 | 2716 | Genoa vs Spal | 1.59 | 3.97 | 5.16 |
| 19:00 | 3781 | VfB Lubeck vs Mainz | 8.86 | 5.84 | 1.29 |
| 19:00 | 3835 | RB Leipzig vs Hamburger SV | 1.31 | 5.45 | 8.69 |
| 19:00 | 3938 | Waldhof Mannheim vs Nurnberg | 3.02 | 3.47 | 2.27 |
| 19:00 | 4750 | Stuttgarter Kickers vs Eintracht Frankfurt | 30.22 | 11.08 | 1.07 |
| 19:00 | 5964 | WSG Wattens vs Rapid Vienna | 3.16 | 3.55 | 1.99 |
| 19:30 | 2759 | Charleroi vs Kortrijk | 1.74 | 3.74 | 4.28 |
| 19:30 | 2978 | Eupen vs OH Leuven | 2.69 | 3.43 | 2.43 |
| 20:00 | 1127 | Sevilla FC vs Valencia | 2.23 | 3.34 | 3.09 |
| 20:00 | 1942 | Dornbirn vs Austria Klagenfurt | 6.03 | 4.87 | 1.37 |
| 20:00 | 4103 | Al Masry Club vs Ceramica Cleopatra | 2.01 | 3.08 | 3.97 |
| 20:15 | 2466 | Gornik Leczna vs Korona Kielce | 3.31 | 3.11 | 2.10 |
| 20:30 | 2491 | Dinamo Moscow vs Rostov | 1.66 | 3.70 | 4.38 |
| 20:30 | 2656 | SV Horn vs Josko Ried | 2.97 | 3.41 | 2.13 |
| 21:00 | 4038 | Getafe vs Athletic Bilbao | 3.89 | 3.29 | 1.96 |
| 21:00 | 4339 | Koninklijke Hfc vs Telstar | 3.26 | 3.45 | 1.99 |
| 21:00 | 4433 | Hoek vs Heerenveen | 15.60 | 7.80 | 1.10 |
| 21:00 | 4522 | Almere City vs FC Oss | 1.52 | 4.27 | 4.76 |
| 21:15 | 3225 | FC Wil vs Lausanne-Sport | 3.11 | 3.59 | 2.00 |
| 21:15 | 5558 | Floridsdorfer AC vs LASK Linz | 5.05 | 4.28 | 1.50 |
| 21:30 | 1997 | Wisla Plock vs Legia Warszawa | 2.58 | 3.16 | 2.53 |
| 21:30 | 2671 | FC Winterthur vs FC Sion | 3.03 | 3.58 | 2.15 |
| 21:30 | 5561 | Brighton vs Nottingham | 1.37 | 4.65 | 7.52 |
| 21:45 | 1233 | Falkirk FC vs Alloa Athletic | 1.79 | 3.65 | 3.94 |
| 21:45 | 1323 | Inverness vs Hamilton | 1.84 | 3.46 | 3.96 |
| 21:45 | 1699 | Norwich City vs Luton Town | 1.81 | 3.42 | 4.27 |
| 21:45 | 1722 | Racing Genk vs KVC Westerlo | 1.56 | 4.29 | 4.99 |
| 21:45 | 2295 | Hoffenheim vs Schalke 04 | 1.51 | 4.53 | 5.64 |
| 21:45 | 2869 | Eintracht Braunschweig vs VfL Wolfsburg | 4.54 | 3.99 | 1.70 |
| 21:45 | 3817 | RFC Seraing vs Cercle Brugge | 3.29 | 3.39 | 2.10 |
| 21:45 | 4718 | Kilmarnock vs Dundee Utd | 2.11 | 3.06 | 3.35 |
| 21:45 | 5158 | SV Darmstadt vs Monchengladbach | 3.28 | 3.78 | 2.04 |
| 21:45 | 5191 | Clyde vs Dunfermline | 4.14 | 3.60 | 1.77 |
| 21:45 | 5200 | Linfield Belfast vs Glenavon | 1.46 | 4.37 | 5.43 |
| 21:45 | 5386 | Huddersfield vs Preston | 2.82 | 3.12 | 2.47 |
| 21:45 | 5471 | Swansea vs Reading | 1.97 | 3.36 | 3.66 |
| 21:45 | 5676 | SV Elversberg vs VfL Bochum | 3.58 | 3.68 | 1.97 |
| 22:00 | 1307 | Stoke City vs Rotherham | 1.91 | 3.47 | 3.72 |
| 22:00 | 1628 | Torino vs Cittadella | 1.43 | 4.45 | 6.53 |
| 22:00 | 5212 | Blackburn vs Sunderland | 2.18 | 3.17 | 3.27 |
| 22:00 | 5445 | West Bromwich vs Bristol City | 1.69 | 3.71 | 4.55 |
| 22:00 | 5472 | Atletico Madrid vs Rayo Vallecano | 1.54 | 3.85 | 6.20 |
| 22:00 | 5546 | Roda Kerkrade vs Heracles Almelo | 2.52 | 3.25 | 2.52 |
| 22:15 | 2349 | Crystal Palace vs Wolverhampton | 2.16 | 3.22 | 3.27 |
| 22:30 | 2180 | CD Feirense vs Moreirense | 3.30 | 3.30 | 2.09 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SERENGETI GIRLS, CANADA VITANI LEO KOMBE LA DUNIA

**Na Adam Fungamwango**

IWAPO itapata ushindi wowote ile dhidi ya Canada, timu ya soka ya Wanawake ya Tanzania chini ya miaka 17, Serengeti Girls itafanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Dunia zinazoendelea kutimua vumbi nchini India.

Timu hiyo leo itajitupa kwenye Uwanja wa DY Patil, Mumbai saa 11:30 jioni kwa saa za Afrika Mashariki, kucheza mechi ya mwisho ya Kundi D ambayo itaamua hatima yao, baada ya Jumamosi iliyopita kuichapa Ufaransa mabao 2-1 na kuzua gumzo kubwa duniani.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, amesema kikosi chake kiliendelea na mazoezi kama kawaida na kiko tayari kwa mechi hiyo ambayo inaweza kuamua mustakabali au hatima yao kwenye michuano hiyo.

**“Tutawakosa wachezaji wetu wawili ambao walipata kadi nyekundu, lakini tumejiandaa kupambana ili kuelekea hatua nyingine,” alisema.**

Neema Paul alionyeshwa kadi nyekundu kwenye mechi ya kwanza dhidi ya Japan wakati Tanzania ikifungwa mabao 4-0 na Joyce Lema akazawadiwa kadi nyekundu kwenye mechi ya pili dhidi ya Ufaransa ambayo Serengeti Girls ilipata ushindi wa mabao 2-1.

Serengeti Girls yenye pointi tatu kama itafanikiwa kupata ushindi itakuwa imejikatia tiketi ya kwenda robo fainali kwani itafikisha pointi sita ambazo haziwezi kufikiwa na Ufaransa hata kama itawafunga mabingwa watetezi, Japan.

Ikumbukwe kuwa Ufaransa ina pointi moja tu, hivyo kama ikishinda mechi hiyo itakuwa imefikisha pointi nne tu.

**ACHIA NJIA...**



Winga wa Yanga, Bernard Morrison, akipiga hesabu za kumtoka mchezaji wa Al Hilal kwenye mechi ya mkondo wa pili ya Raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Sudan juzi na Yanga kukubali kipigo cha bao 1-0, hivyo kutupwa nje kwa jumla ya mabao 2-1 kutokana na sare ya 1-1 kwenye mechi ya mkondo wa kwanza Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Wapinzani wa Yanga

INATOKA UKURASA 32

nachama na mashabiki wa klabu hiyo kuyafanyia kazi mapungufu yote yaliyojitokeza ili watakaporejea tena wawe imara zaidi, lakini kujiandaa kikamilifu na Kombe la Shirikisho Afrika walikoangukia.

“Tumemaliza mchezo salama, hakuna madhara makubwa ya kiafya, kwa bahati mbaya matokeo si yale tuliyoyatarajia, mmeona wachezaji walivyojitoa na kupambana, tunarudi nyumbani, tunaenda kujiandaa na mashindano ya ndani, lakini mashindano ya nje, Kombe la Shirikisho, ambayo bado ni mashindano ya kimataifa,” alisema Hersi.

Alisema wao kama viongozi wanakwenda kurekebisha mapungufu yaliyoonekana kwa ajili kukiimaisha kikosi.

## *Mgunda aeleza changamoto*

INATOKA UKURASA 32

sawa.

“Nashukuru sana Bodi ya Wakurugenzi, viongozi, benchi la ufundi, wachezaji na mashabiki wengi waliojitokeza kwenye mechi hii na haya yaliyotokea ni mipangilio, ni ramani ya muda mrefu na mfupi, kwa miaka mitano sasa hii ni mara ya nne kufika makundi, sasa tuna uzoefu mkubwa. Sasa inabidi tujipange kwa jili ya hatua ya makundi, sawa wote tuna furaha, lakini tujue furaha ya Simba ni ya Watanzania.

“Mgunda ameshirikiana vizuri na wachezaji, namheshimu, Mungu akinijalia nataka nikutane naye, nimsikilize, tutashirikiana naye, anaweza kabisa kuwa kocha mkuu kwa sababu amefanya mambo makubwa,” alisema.

Wakati huo huo Mwenyekiti wa zamani wa klabu ya Simba, Hassan Dalali, amewataka wachezaji, benchi la ufundi na uongozi kusahau furaha ya kuingia makundi na kupanga mikakati ya kumfunga mtani wao, Yanga kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Dalali alisema baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wanatakiwa kuwaza mechi ijayo ya watani wao kuhakikisha wanapata pointi tatu msimu huu.

# Michezo

Jumanne Oktoba 18, 2022

Nipashe




'Sijawahi kuomba kuondoka PSG' UKURASA 29

# Mgunda aeleza changamoto kuinoa Simba

●●● Rais Samia awapa kongole kutinga makundi Afrika, waonywa mechi Yanga...

Saada Akida na Adam Fungamwango

HUKU akiwapongeza wachezaji wake, benchi lake ufundi, viongozi na mashabiki kwa ushirikiano wa pamoja hadi kufanikiwa kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, ameeleza changamoto kubwa aliyokutana nayo baada ya kukabidhiwa mikoba ya kukinoa kikosi hicho.

**Aidha, baada ya juzi kuitoa Primeiro de Agosto ya Angola kwa jumla ya mabao 4-1 kutokana na ushindi wa bao 1-0 iliyoupata Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na ule wa 3-1 ugenini, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ameipongeza klabu hiyo kufanikiwa kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Rais ametoa pongezi hizo juzi kwenye mtandao wake wa kijamii baada ya Simba kuifunga Primeiro de Agosto bao 1-0, shukrani kwa Moses Phiri aliyeifungia bao hilo pekee.

"Kongole Simba ya Tanzania kwa ushindi wa 1-0 (ushindi wa jumla 4-1) mlioupata dhidi ya timu ya Primeiro de Agosto ya Angola na hivyo kufanikiwa kuingia hatua ya makundi ya Klabu Bingwa barani Afrika. Nawatakia kila kheri katika michuano inayofuata," aliandika Rais Samia.

Hata hivyo, Kocha Mgunda, akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo, alisema alipata changamoto kubwa sana hasa alipokabidhiwa jukumu la kuinoa Simba kwa sababu ya ukubwa wa timu na mashindano wanayoshiriki.

"Changamoto kwangu ilikuwa kwa sababu ya ukubwa wa Simba na presha ya mashabiki katika ushiriki wa timu hii kwenye michuano ya kimataifa, lakini nashukuru viongozi na kwa upande wa wachezaji kufanya kile ambacho ninachowapa hasa wale wakongwe katika timu," alisema Mgunda.

Alisema wanaenda katika hatua ngumu na kuwataka Wanasimba wote kuendelea kujenga nguvu moja ili kufikia hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Mgunda alisema Wanasimba jukumu lao kubwa ni kuendelea na mshikamano wanaouonyesha kwa timu yao ili iendelea kufanya vizuri katika michuano hiyo kwa kusonga mbele.

"Mafanikio haya si yangu pekee bali benchi langu, wachezaji, viongozi na mashabiki kila mmoja kwa nafasi yake ametimiza majukumu yake.

"Nawapongeza wachezaji wangu kwa kufuata maelekezo tuliyokuwa tunawapa kwa vitendo, wamefanya kazi yangu kuwa rahisi," alisema Mgunda.

Alisema baada ya kufikia malengo ya kwanza ya kuingia hatua ya makundi, maandalizi kuelekea hatua inayofuata yanaanza mara moja kwa kuwa michuano hiyo inazidi kuwa migumu.

"Tukiendelea kushikamana na kuwa nguvu moja kwa Wanasimba wote, ninaimani tunaenda kufanya vizuri katika hatua nyingine ya michuano hii," alisema Mgunda.

Kocha wa De Agosto, Filipe Nzanza, alisema mechi ilikuwa ya ushindani, amepokea matokeo hayo na anakwenda kujipanga kwa ajili ya michezo iliyoko mbele yao katika Kombe la Shirikisho Afrika.

Alisema anawapongeza Simba kwa kufanikiwa kutinga hatua ya makundi, walipambana na kutumia vema makosa yaliyofanywa na wachezaji wake na kujihakikisha kusonga mbele.

"Timu yangu bado mpya kwa sababu ndio naandaa kikosi, ninaimani baada ya muda nitakuwa na timu bora zaidi ya hii ya sasa.

"Nawatakia kila kheri Simba katika hatua nyingine na niwapongeze wachezaji wangu kupambana katika huu mchezo na sasa tunarudi uwanjani kwa ajili ya Kombe la Shirikisho," alisema Nzanza.

Katika hatua nyingine Rais wa Heshima wa Simba, Mohammed 'Mo' Dewji amewapongeza wachezaji na benchi la ufundi kutinga hatua ya makundi huku akiahidi kukaa na Mgunda kwa ajili ya kuweka mambo

INAENDELEA UK. 31

'GENERAL'...



Mfungaji wa bao pekee la Simba, 'General' Moses Phiri, akifurahia wakati timu yake ikishinda 1-0 dhidi ya Primeiro de Agosto katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **PICHA: SIMBA**

## Wapinzani wa Yanga Shirikisho hawa hapa

Na Adam Fungamwango

WAKATI Yanga ikitupwa kwenye Kombe la Shirikisho la Soka Afrika (CAF), baada ya kushindwa kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa, mpinzani wake wa hatua ya mtoano anatarajiwa kujulikana leo mchana katika droo inayotarajiwa kufanyika jijini Cairo, Misri.

Yanga ambayo juzi ilitolewa kwa jumla ya mabao 2-1, ikitoka sare ya bao 1-1 nchini Tanzania na kufungwa 1-0 dhidi ya Al Hilal ya Sudan, mechi ikichezwa Omdurman, Khartoum itacheza na moja kati ya timu 16 zilizofanikiwa kuvuka kwenye raundi ya pili ya michuano hiyo.

Timu hizo zinaongozwa na Bingwa Mtetezi, RS Berkane ya Morocco ambayo imefanikiwa kutinga hatua hiyo kwa bao la ugenini dhidi ya Kwara ya Nigeria, ikifungwa mabao 3-1 ugenini, kabla ya 'kupindua meza' kwa kushinda 2-0 nyumbani juzi.

Timu nyingine ambayo inaweza kukutana na Yanga ni Al Akhdar ya Libya ambayo iliitoa Azam FC juzi kwa jumla ya mabao 3-2, ikishinda nyumbani 3-0, lakini ikapoteza kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kwa mabao 2-0 ambayo hayakuwazuia kusonga mbele.

Zingine ambazo zinaweza kukutana na Yanga, itakayoanzia nyumbani ni Ashanti GB ya Guinea, Marumo Gallants na Royal AM zote za Afrika Kusini, SC Gagnoa ya Ivory Coast, CX Sfaxien ya Tunisia, St Eloi Lupopo na Motema Pembe zote za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Pyramids ya Misri, Diables Noirs ya Congo Brazzaville, Hearts of Oak ya Ghana, Club Africain ya Tunisia, Al Nasr ya Libya, USM Alger ya Algeria na Future ya Misri.

Rais wa Klabu hiyo, Injinia Hersi Said, alisema baada ya kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa, amewaahidi wa-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >